# MWENDELEZO WA TAMTHILIA YA MASHETANI (1971) KATIKA MASHETANI WAMERUDI (2016): UHAKIKI WA KIMWINGILIANOMATINI

**KENNETH MUGAMBI MUTUMA**

**Tasnifu iliyowasilshwa katika Shule ya Mafuzu ili kutosheleza baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUO KIKUU CHA CHUKA**

**OKTOBA 2024**

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya kutosheleza shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine.

Sahihi……………………………………… Tarehe 22/10/2024……………

Kenneth Mugambi Mutuma
AM12/51106/20

**Idhini**

Tasnifu hii imetahiniwa, ikapitishwa na kuwasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu.

Sahihi……………………………………… Tarehe 22/10/2024……………

Dkt. Allan Mugambi
Chuo Kikuu cha Chuka

Sahihi……………………………………… Tarehe 22/10/2024……………

Dkt. Dorcas Musyimi
Chuo Kikuu cha Chuka

CHUKA UNIVERSITY
RECEIVED
23 OCT
P.O. Box 109-60400, CHUKA

**HATIMILIKI**

©2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kuiga, kuhifadhi kwa njia yoyote bila idhini kutoka kwa mwandishi au Chuo Kikuu cha Chuka.

## TABARUKU

Kazi hii namtabarukia wazazi wangu Samuel Mutuma na Judith Mugito.Tabaruku nyingine ni kwa Isaac M'Nkanata, Salome na Monica Mwitiambi kwa kuniunga mkono kwa hali na mali wakati wa kipindi kigumu nilipokuwa nikiendelea na masomo yangu. Nawatakia baraka za Mwenyezi mungu.

## SHUKRANI

Mafanikio ya utafiti huu yanahusisha watu wengi. Nitakosa fadhila iwapo sitawashukuru. Kwanza namshukuru Mungu kwa kunijalia dua njema. Pili natoa shukrani zangu za dhati kwa Chuo Kikuu cha Chuka kwa kunikuza na kunipa nafasi ya kutangamana na jumuiya ya wasomi tangu nilipoanza shahada ya uzamili. Aidha, nawashukuru wasimamizi wangu Dkt Allan Mugambi na Dkt Dorcas Musyimi kwa kunishika mkono na kunielekeza katika tasnia hii ya kitaaluma.

Ninatoa shukrani kwa wahadhiri wangu katika kiwango cha uzamili. Hawa ni pamoja na Dkt Allan Mugambi, Dkt Dorcas Musyimi, Dkt Mary Kanyua, Dkt Onesmus Ntiba na Dkt Shadrack Kirimi. Marafiki wengine ambao walinifaa katika tasnia hii ni pamoja na: Dkt Stepthen Micheni, Prof Nancy Mbaka, Dr Beatrice Micheni, Lilly Mbugua na Dr Kawira Kamwara kwa Mwongozo niliyopata kwao umenifaa katika kazi hii. Hatimaye, shukrani kwa dada zangu Wendy Nkatha, Ivyonne Gacheri, Skitter Kagwiria, Cecilia, Emily Nkatha na Pierra Mwendwa kwa kunihimiza kuendeleza masomo yangu. Kuna wengine ambao walinifaa ingawa sijaweza kuwataja. Naomba radhi na kuwashukuru kwa dhati. Nawatakia dua njema kutoka kwa Mungu.

Mwisho nawashukuru wazamilii wenzangu tulioanza safari hii pamoja. Hawa ni pamoja na Lemmy Muriuki, Evans Kinoti, Mercy Muthoni, Justine Monene, Justine Ireri, Austine, Martin Karani na Paul Thuranira. Nawashukuru wote kwa kunitakia mema katika safari hii. Mungu awabariki nyote.

**IKISIRI**

Utafiti huu ulichunguza mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (*1971*) katika *Mashetani Wamerudi* (*2016*). Malengo ya utafiti huu yalikuwa: kuchunguza mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani* (Hussien, 1971) katika *Mashetani Wamerudi* (Mohamed, *2016*), Kutathimini athari za mwendelezo wa mtindo katika *Mashetani* kwenye *Mashetani Wamerudi* na kubainisha viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1986). Mwingilianomatini ni dhana inayoonyesha kutegemeana, kuhusiana na kuathiriana kwa matini. Hii ina maana kuwa kazi za fasihi hurejelea na kuendeleza kazi tangulizi. Kulingana na Kristeva kazi ya fasihi huonyesha kuathiriana na matini nyingine, huzigeuza na kuziendeleza kwa ubunifu. Mihimili iliyoongoza utafiti huu ni pamoja na: matini yoyote ile ni madadiliko ya mpangilio wa matini nyingine, kazi za fasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi. Matini za fasihi huchota, kunukuu na kuiga kazi nyingine. Data ya utafiti ilipatikana maktbani kutokana na usomaji na uchambuzi wa matini teule. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* kwa sababu matini hizi zinadhihirisha mwingiliano wa aina fulani. Vipengele vinavyodhihirisha mwingilianomatini vilibainishwa na kuchanganuliwa ili kuonyesha mwendelezo wa kimatini uliopo. Utafiti huu umedhihirisha kwamba kuna mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi*. Imebainika kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameiga, amerejelea na kuendeleza tamthilia ya *Mashetani* katika kiwango cha maudhui, mtindo na viwango vya kimwingilianomatini. Matokeo ya utafiti huu yaliashiria kuwa kuna mwendelezo wa maudhui ya Ukoloni mamboleo, elimu ya kibwege, utabaka na ufisadi ni baadhi ya masual makuu amabyo yanajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Katika lengo la pili utafiti umethibitisha kuwa Said Mohamed amerejelea na kuiga mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake. Matumizi ya mtindo wa usimulizi, nyimbo, majigambo, ushairi na maigizo ni baadhi ya vipengele vya kiutunzi ambavyo vimetumika kama malighafi ya kiutunzi katika kazi ya Said Mohamed. Hatimaye, utafiti huu ulibainisha kuwa kuna urejelezi wa moja kwa moja wa tamthilia ya *Mashetani* kupitia njia zifuatazo: Urejelezi wa matini za Kihistoria, urejelezi wa kiutohozi pamoja na uigaji. Matokeo ya utafiti huu yataweka msingi kwa waandishi na walimu wa fasihi katika kuonyesha jinsi fasihi inavyoingiliana kwa kurejelea vipindi tofauti vya kihistoria na kiutamanduni.

# ABSTRACT

This study aims at establishing the textual continuity in the plays *Mashetani* (1971) by Ebrahim Hussein and *Mashetani Wamerudi* (2016) by Said Ahmed Mohamed. This concept of intertextuality serves as a foundation for analyzing *Mashetani* (1971) and *Mashetani Wamerudi* (2016). The current work therefore, targeted this barely researched area by evaluating the extent to which *Mashetani Wamerudi* has been echoed and referenced by *Mashetani*. The study was guided by the following objectives: to examine the continuity of thematic interactions between *Mashetani* (1971) and *Mashetani Wamerudi* (2016), to evaluate stylistic influences portrayed by the authors of *Mashetani* and *Mashetani Wamerudi and* to determine types of intertextualities between *Mashetani* (*1971*) and *Mashetani Wamerudi* (2016). This study was guided by Julia Kristeva's intertextuality theory (1986). Intertextuality refers to the way texts are connected to and influenced by each other. Most texts draw on, reuse, and are shaped by other works, creating a web of interrelated texts. Julia Kristeva's theory posits that all art is derived from reinterpreting, modifying, and imitating existing texts. adheres to several tenets that, each text is a product and rearrangement of preceding texts, literary works are referenced and influenced by the cultural systems established by earlier texts, each text contributes to the understanding of related texts, with new texts building upon and responding to earlier ones, and literary texts engage in borrowing, referencing, altering, and mimicking other texts through intertextuality. The study established that there are thematic continuity and stylistic devices have contributed to types of intertextualities between *Mashetani* and *Mashetani Wamerudi.* The research employed content and textual analysis as its methodology and was conducted in a library setting. Data was collected through an in-depth reading of the selected plays. Research results indicate that the author of *Mashetani Wamerudi* has replicated, alluded to, and cited *Mashetani* in terms of thematic consistency, styles, and types of intertextualities. The study's findings revealed a continuation of themes related to neo-colonialism, education, casteism, and corruption in *Mashetani Wamerudi*. The findings also demonstrated that Said Mohamed has imitated and referenced his predecessor's writing styles. Elements such as narration, drama, songs and poetry have been utilized in Said Mohamed's work. Lastly, the study identified direct references to *Mashetani* Play through historical text references and imitation. This study will establish the groundwork for writers and educators to illustrate how literature interacts by referencing different historical and cultural periods in literary texts.

## YALIYOMO

**UNGAMO NA IDHINI** .......... **ii**

**HATIMILIKI** .......... **iii**

**TABARUKU** .......... **iv**

**SHUKRANI** .......... **v**

**IKISIRI** .......... **vi**

**ABSTRACT** .......... **vii**

**YALIYOMO** .......... **viii**

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI** .......... **1**

1.1 Usuli wa Mada .......... 1

1.2 Suala la Utafiti .......... 8

1.3 Madhumuni ya Utafiti .......... 9

1.4 Maswali ya Utafiti .......... 9

1.5 Sababu za Kuchagua Mada .......... 9

1.6 Umuhimu wa Utafiti .......... 10

1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti .......... 11

1.8 Maelezo ya Istilahi .......... 12

**SURA YA PILI: MWAUO WA MAANDISHI** .......... **13**

2.1 Historia Fupi ya Ebrahim Hussein .......... 13

2.2 Historia Fupi ya Uandishi wa Said Ahmed Mohamed .......... 13

2.3 Historia Fupi ya Tamthilia .......... 15

2.4 Maudhui na Mwingilianomatini .......... 17

2.5 Mtindo na mwingilianomatini .......... 21

2.6 Viwango vya Kimwingilianomatini katika fasihi .......... 25

2.7 Misingi ya Kinadharia .......... 27

2.8 Hitimisho .......... 33

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI** .......... **34**

3.1 Eneo la Utafiti .......... 34

3.2 Uteuzi wa Sampuli .......... 34

3.3 Ukusanyaji wa Data .......... 34

3.4 Uchanganuzi wa Data.....35
3.5 Uwasilishaji wa Matokeo.....35
3.6 Maadili ya Utafiti.....35

**SURA YA NNE: MWENDELEZO WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TEULE.....36**
4.0 Utangulizi.....36
4.1 Utandawazi kama Tapo la Ukoloni Mamboleo.....36
4.1.1 Elimu ya Kibwege.....43
4.1.2 Utabaka.....47
4.1.3 Ufisadi.....52
4.2 Hitimisho.....57

**SURA YA TANO: ATHARI ZA MTINDO KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI.....58**
5.0 Utangulizi.....58
5.1 Dhana ya Mtindo.....58
5.1.1 Matumizi ya Usimulizi.....59
5.1.2 Matumizi ya Majigambo.....60
5.1.3 Matumizi ya Taswira.....63
5.1.4 Matumizi ya Mtindo wa Kishairi.....65
5.1.5 Matumizi ya Nyimbo.....67
5.1.6 Mtindo Katika Kiwango cha Wahusika.....70
5.1.6.1 Maelezo ya Wahusika Wengine.....71
5.1.6.2 Mazungumzo au Matendo ya Wahusika wengine......72
5.1.6.3 Mbinu ya Kiutohozi.....73
5.1.7 Mandhari ya Kiutunzi.....75
5.2 Hitimisho.....77

**SURA YA SITA: VIWANGO VYA MWINGILIANOMATINI BAINA YA TAMTHILIA TEULE.....78**
6.0 Utangulizi.....78
6.1 Urejelezi.....78
6.1.1 Urejelezi wa Tamthilia Tangulizi ya Mashetani.....78

6.1.2 Urejelezi wa matini za Kihistoria ........ 80
6.1.3 Urejelezi wa Moja kwa Moja ........ 82
6.1.4 Urejelezi wa Kiutohozi ........ 84
6.1.5 Urejelezi wa Mila na Desturi za Kigeni ........ 87
6.2 Uigaji ........ 89
6.3 Hitimisho ........ 92

**SURA YA SABA: MUKTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 93**
7.1 Muktasari ........ 93
7.2 Matokeo ya Utafiti ........ 94
7.3 Mapendekezo ya Utafiti wa baadaye ........ 95

**MAREJELEO ........ 96**
**VIAMBATISHO ........ 101**
Kiambatisho 1: Barua ya Kumtambulisha Mtafiti kutoka Chuo kikuu cha Chuka ........ 101
Kiambatisho 2: Barua ya Idhini ya Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka ........ 102
Kiambatisho 3: Kibali cha Utafiti cha NACOSTI ........ 103

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa Mada

Mwandishi wa matini ya kifasihi huwa na jukumu la kuelimisha hadhira yake kutokana na masuala yanayomwathiri katika maisha. Mwandishi hufanya hivi kwa kuteua kipera kimoja atakachoshughulikia ili kufanikisha dhamira yake. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999), lugha anayotumia mwandishi ndiyo mzizi katika kazi ya fasihi. Lugha huwa ni malighafi muhimu ambayo msanii hutumia ili kubuni kazi yake. Lugha ya fasihi huwa na sifa fulani. Mwandishi hutumia vikolezo fulani ili kutia kazi yake ladha fulani. Kwa hivyo, lugha hujidhihirisha kupitia vipengele vya fani na mbinu nyingine za lugha. Fasihi kama sanaa inayotumia lugha kwa ubunifu huwasilisha ujumbe ambao hujenga dhamira ya mwandishi. Wamitila (2003), anaeleza kuwa waandishi wengi katika harakati za kushughulikia masuala yanayoathiri jamii matini zao hushughulikia mambo yanayoonyesha mfanano wa aina fulani, hali ambayo huchangia kuwepo kwa matini tofauti kimtindo na kifani.

Mwendelezo wa kazi za fasihi ni mbinu ambayo imekumbatiwa na waandishi wa kazi za fasihi katika karne ya ishirini na moja. Mbinu hii imetumika kama kipengele cha kiutunzi na huwa na misingi yake katika kazi za awali (Cuddon, 2013). Mwendelezo wa matini ni mojawapo wa mbinu za uandishi katika tamthilia za kibaadausasa. Hata hivyo, mtindo huu umeanza kuleta mabadiliko makubwa katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Mojawapo wa mabadiliko haya yanadhihirika kupitia matumizi mengi ya nadharia ya mwingilianomatini (Mohamed, 2002)

Mwingilianomatini kwa mujibu wa Kristeva (1986) hushikiria kuwa matini za kifasihi huonyesha mwingiliano baina matini za fasihi zilizotangulia. Hakuna matini ya fasihi inayoweza kuangaliwa kivyake bila kutegemeana au kuathiriana na matini zilizotangulia. Mara nyingi mwendelezo wa kimatini huwa kama kigezo sahili kinachotumika kama misingi ya kujenga na kupanua usimulizi wa matini ya awali. Kwa hivyo, kazi ya fasihi huchunguzwa katika mwanga wa kutegemeana na kuathiriana. Kristeva (keshatajwa) anasisitiza kwamba mwingilianomatinini humpa mwandishi nafasi ya kujenga kazi yake kwa kuihusisha na matini ya awali. Matini za baadaye humpa mtunzi au msomaji ufasili wa kazi iliyotangulia. Wafula (2007), anaeleza kuwa

mtunzi wa matini anaweza akamtaja mtangulizi wake akiwa na lengo la kutumia kazi yake kama mwendelezo wa matini yake. Kazi ya fasihi iliyobuniwa huwa na misingi kuendeleza kazi ya awali. Matini ya baadaye huwa ni msingi wa mawazo ya awali. Kwa mfano, katika utafiti huu dhana hii ya mwendelezo imejitokeza katika tamthilia ya *Mashetani*. Katika tamthilia hii, Shetani ameendelezwa kama mhusika bapa ambaye habadiriki katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Mtunzi wa kazi ya fasihi huwa na mtindo tofauti kutegemea utanzu wa fasihi. Mtunzi anaweza kuiga na kuendeleza mtindo fulani kutoka kwa waandishi waliotangulia. Mtindo huu wa uandishi ambapo matini inarejelea matini nyingine umeanza kuwa maarufu katika fasihi. Mojawapo ya mabadiliko haya yanadhihirika kupitia matumizi ya mwingilianomatini (Mohamed, 2002). Mwingilianomatini umetumika kama mbinu ya mtindo wa uandishi kudhihirisha namna urejeleaji wa matini umejitokeza katika kazi za fasihi. Urejeleaji huu aghalabu huitenga kimaksudi hadhira isiyobobea katika fani mbalimbali na huzifanya kazi hizi kuwa ngumu kusomeka na kueleweka. Data ya utafiti inadhihirisha kuwa dhana ya mwendelezo katika tamthilia hujitokeza wakati ambapo, mwandishi wa matini huwa amegundua kwamba kuna hadhira ambayo mwandishi wa matini ya awali hakushughulikia kikamilifu katika kazi na angependa kuendeleza kazi kama kimelea cha matini ya awali.

Mwingilianomatini hutumiwa kama njia ya kumtambua msomaji kama mshiriki katika mchakato kubuni kazi ya kifasihi (Childs & Fowler, 2006). Kazi yoyote ya kifasihi hujumuisha wahusika watatu; mwandishi, matini na msomaji. Kwa kuwa mwandishi ndiye mpangaji wa mawazo, msomaji ana nafasi muhimu ya kuweza kung'amua maana inayotokana na yale ambayo mwandishi ameyapanga. Kauli hii inaungwa mkono na Lemaster (2012) anaposema kwamba iwapo mwandishi amerejelea matini nyingine katika kazi yake, ufasiri wa maana husika itakayopatikana katika matini itakuwa ni mwendelezo wa kazi ya awali. Aidha, itategemea iwapo msomaji anafahamu matini hizo zilizorejelewa au la. Iwapo msomaji hajawahi kupatana na matini hizo zilizorejelewa, atakuwa na ufasiri mwingine ambao unaweza kukubalika. Ni kutokana na huu uwezo wa msomaji wa kuweza kung'amua maana katika matini ya kifasihi ambapo msomaji anachukuliwa kama mhusika muhimu katika kazi ya sanaa.

Waandishi hutunga kazi zilizo na mfanano wa aina fulani katika kueleza dhamira zao. Dhamira zinazoibuliwa hazitokani na ombwe tupu kwa sababu lugha na mazingira waliokulia ni vitu viwili ambavyo havitengani. Ponera (2014), anaeleza kuwa, bali na waandishi kuathiriwa na lugha, historia pia huchangia katika uandishi wa matini za baadaye. Watunzi waliokulia katika vipindi tofauti vya kihistoria huenda wakaathiriana katika dhamira zao. Uhusiano huu wa kihistoria huchangia katika uathiriano na usomekaji wa matini zinazoibukia kwa kuiruhusu matini tangulizi iiathiri kwa kiwango fulani kupitia usimulizi wa matukio, dhamira na maudhui. Kauli hii inaungwa mkono na (Mningo, 2015) anaposema kwamba, matini za kifasihi huweza kuathiriana na kuingiliana na kazi zingine za kipindi fulani cha kiwakati na kimazingira. Mwandishi wa kazi ya fasihi huwa anawakilisha kipindi fulani cha historia. Kwa hivyo, historia na mazingiria ya kiutunzi huwa ni vipengle vinavyoibua dhana ya mwingilianomatini. Umwngilianomatini unaojitokeza huwa ni mbinu inayotumiwa na watunzi kuendeleza kazi za awali (Yenjela, 2015). Kwa mujibu wa data ya utafiti huu, dhana ya mwendelezo wa kazi za fasihi unapatikana kupitia mtindo wa kiutunzi katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Mwingilianomatini huvuta makini ya msomaji wa matini ya fasihi kwa kiwango fulani kwenye kazi zilizotangulia kwa sababu matini ya fasihi huwa inahusiana kazi zilizotangulia. Mwandishi huwa amenukuu, ameiga na kugeuza au kurejelea kazi tangulizi. Watunzi wa kazi za fasihi wanaweza kutumia lugha tofauti kurejelea kitu kimoja au kurejelea matukio mbalimbali katika jamii zao Wamitila (2008). Aidha, mwandishi anaweza kuwa ameathiriwa na matukio fulani katika kazi tangulizi na kisha akamua kuendeleza mgogoro huu katika matini yake. Umwingilanomatini unadhihirika kupitia katika sampuli teule za utafiti huu kwa sababu Said Mohamed ameiga na kurejelea baadhi ya wahusika na mandhari ya kiutunzi kama inavyodhihirika katika kazi ya awali ya Ebrahim Hussein.

Mwanaisimu Ferdnard de Suassure anaeleza kuwa ili kufanikisha ujumbe, mtunzi wa matini hana budi kurejelea matini za awali ili kuwasilisha ishara yake. Kwa kufanya hivi kazi inayoundwa itakuwa kama mwangwi wa matini inayohusiana nayo. Kwa hivyo, ili kuhakiki matini lengwa, mwandishi hurejelea matini ya awali inayohusiana nayo ili kurahisisha kazi inayorejelewa. Mawazo yake yanalandana na ya Clayton

(2012), anaposema kuwa waandishi wa kazi za hutumia mwingilianomatini kuvuruga imani ya awali. Matini za fasihi huonyesha namna matini husika ilivyoathiriwa na matini tangulizi kupitia matumizi ya mwingilianomatini, na hulenga kuziandika upya matini hizo za awali kwa njia ya kubeza. Hivyo basi, waandishi hutumia vipengele vya matini za awali kama malighafi ya kuunda na kuandika kazi zao. Hii ina maaana kwamba, mbinu ya mwingilianomatini hutumiwa kuhakiki mawazo ya waandishi maarufu ili kutafuta njia mbadala ya kuzisoma kazi zile na kupindua usomaji uliozoeleka wa kazi hizo. ( Ahmadian na wengine,2013)

Kwa mujibu wa Nwagbara (2015), kazi za fasihi huathiriana na kurejeleana kwa njia mbalimbali jambo ambalo hufanya matini ya fasihi kuwa na mwingiliano. Matini mbalimbali huingiliana na kuathiriana. Mwingiliano huu huweza kuangaliwa katika mkabala wa mwingilianomatini ambao hulinganisha na kulinganua kazi mbalimbali za fasihi. Naye Kilingo (2019) anasema kwamba mwingilianomatini huchanganua fasihi mbalimbali kwa kuzilinganisha, pale ambapo matini zinaingiliana hudhihirika bayana na tofauti huonekana. Aidha, uchunguzi wa kina wa kazi yoyote utaonyesha athari ya moja kwa moja au athari fiche ya maingiliano haya. Fasihi huathiriana kwa njia mbalimbali kama vile: maudhui, wahusika na matumizi ya lugha. Kutokana na mawazo haya, mtafiti alichunguza mwendelezo baina ya matini teule.

Matini za fasihi zinaingiliana na kupiga mwangwi katika matini za fasihi za awali. Kwa hivyo, kazi za fasihi huwa na sifa za kazi nyingine za fasihi. Waandishi wa matini za fasihi wanaweza kuwa wamekulia katika mazingira na historia tofauti lakini wakazitunga kazi zinazoathiriana kimtindo na kimaudhui Bakhtin (1981). Ufafanuzi sawa na huu umetolewa na Wamitila (2003) anaposema kwamba mwandishi anapoanza mchakato wa kutunga kazi yake hujiingiiza kwenye mwingiliano wa aina fulani na matini zilizotangulia. Kazi yoyote ya kifasihi huweza kuwapo mwendelezo wa kimtindo na kimaudhui wa namna fulani. Mwandishi anaweza akatunga kazi yake kwa kuegemeza mtindo wa kiutunzi katika matini ya awali. Kwa hivyo, mwandishi wa matini ya baadaye sio lazima awe amesoma kazi ya awali ili kuelewa maana inayotokana na kazi iliyotangulia kazi yake. Kazi za fasihi huweza kuchukua mtindo na muundo sawa ijapokuwa hakuna uhusiano uliopo. Kwa hivyo, waandishi wanaweza kuathiriana kwa hali sawa kihistoria na kimazingira. Naye Mningo (2015), anaeleza

kuwa waandishi wanaweza kuibua mtindo na mbinu zinazofanana, huku mwingiliano unaotokea ukiwa tofauti. Suala la kimsingi hata hivyo, ni kule kurejelea au kuendeleza jambo husika katika kazi za watunzi mbalimbali. Mwandishi anaweza kuwa na dhima inayowiana na mwandishi wa kazi zilizotangulia kazi yake. Masuala yanayorejelewa na katika kazi zao ni yale yale ya awali.

Kwa mujibu wa Kristeva (1978), kazi ya fasihi hubuniwa kutokana na misingi ya kazi zilizotangulia. Kwa hvyo mwandishi anapobuni kazi yake hujikita katika urejelezi wa kazi mbalimbali ili kujenga matini yenye ukamilifu. Mwandishi anaweza akarejelea mawazo ya kazi za awali moja kwa moja ili kujenga matini iliyo na ukaribiano wa kimawazo kazi yake. Kristeva anaeleza kuwa kazi inayobuniwa inatokana na kanuni zilizowekwa na matini ya awali. Kazi ya fasihi huundwa kutokana na historia ya mwandishi. Kwa hivyo, waandishi waliokulia katika vipindi tofauti vya kihistoria na kimazingira wanaweza kuathiriana kimawazo katika mchakato wa kiutunzi. Vilevile, kuna vipengele vya khistoria ambavyo huwa vinarudiwarudiwa katika matini ya sasa kutokana na jinsi mwandishi alivyorejelea historia yake kwa kuunganisha matukio yaliyojiri ili yawiane na matini ya sasa. Urejelezi wa matukio kihistoria katika kazi ya fasihi ni jambo ambalo linaweza kukubalika.

Kila matini huwa ni mkusanyiko wa matini zilizotungwa hapo awali. Kazi ya fasihi huwa inajibizana na kusemezana na kazi nyingine. Hii ina maana kuwa kazi ya fasihi huundwa kutokana na kazi za awali, huku kazi ya sasa ikiwa kama msingi wa kuunda kazi za baadaye (Bell & Halliday, 2003). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa ni vigumu kupata matini ya fasihi yenye uasilia. Asili ni dhana ya kinasibu kwa kuwa kazi za fasihi zina mipaka inayoweza kuvunjwa. Hali hii hurusu matini fulani kuingiliana na kutegemeana na nyingine. Mawazo ya wataalamu hawa ni muhimu katika kuchunguza jinsi ambavyo tamthila ya *Mashetani* ilivyoendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kwa kuzingatia athari za mwingilianomatini. Maoni ya wataalamu hawa ni muhimu katika kubaini kuwa hakuna matini ambayo haihusiani na nyingine kupitia vipengele mbalimbali vya fasihi. Mtazamo wa Ahmadian (2010) unaashiria kuwa mwingiliano wa matini za fasihi ni jambo la kawaida katika mchakato wa utunzi wa kazi ya fasihi. Mwandishi huwa amechota na kuiga baadhi ya vipengele vya utunzi kutoka kwa matini iliyotangulia na kutumia vipengele hivyo kiubunifu katika kazi yake.

Hii ina maana kuwa mtunzi wa matini anapaswa kuwa na uelewa jinsi matini zinavyoingiliana, ufahamu huu utamsaidia katika kubuni matini mpya ya fasihi.

Waandishi wa kazi za fasihi huweza kuathiriana katika tungo zao kupitia usimulizi, usawiri wa wahusika, matumizi ya lugha, mandhari na mpangilio wa matukio. Ni kupitia mawanda haya ambapo mwandishi huwa ameendeleza kazi ya mtangulizi wake Kilingo (2019). Lugha kama sanaa ya uandishi inaweza kuonekana kupitia jinsi mwandishi anavyounda matini yake. Kilingo anaona kwamba kuna waandishi wa matini za fasihi ambao huiga mtindo wa mwandishi na kisha kuendeleza mtindo ule katika matini zao. Kwa hivyo, waandishi wanaweza kuathiriana katika mtindo wao wa kuwasilisha dhamira. Kwa mfano, katika utafiti huu dhana ya mwendelezo imejitokeza kutokana na jinsi Said Mohamed alivyokumbatia mtindo wa usimulizi kama mtindo wa kiutunzi.

Mwingilianomatini unaweza kujitokeza kupitia urejelezi wa matini mbalimbali. Matini za fasihi huweza kurejeleana ili kukamilisha wazo fulani. Hali hii hujitokeza wakati ambapo matini huathiriana kimtindo. Lugha iliyotumika katika kazi ya awali inaweza kuathiri matini za baadaye. Kulingana na mtazamo wa Ongorora (2020), lugha ya mwandishi ni ya kihisia na huwa inabeba mkabala wa mwandishi. Lugha hutumiwa kuwasilisha ujumbe, mbali na kuwasilisha ujumbe hutumiwa kisanaa kumshawishi na kuamuathiri msomaji wa matini ya fasihi kutokana na jinsi mwandishi alivyofinyanga lugha yake kwa njia mbalimbali. Mazoea ya mwandishi kutumia mtindo tofauti katika uandishi wake huwa unaashiria kiwango chake katika uteuzi wa msamiati na fani mbalimbali za lugha. Mwandishi huwa ametawaliwa na mambo kama vile mtazamo wake, mazingira ya uandishi na historia yake. Ni kwa maoni haya, utafiti huu uliangazia ni kwa kiwango gani Said Mohamed ameendeleza mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake katika tamthilia ya *Mashetani*

Macha (2013), anadhihirisha kwamba mahali ambapo matini mbili au zaidi zinaingiliana panadhihirisha ukaribiano mkubwa kati ya kazi za fasihi zinazochunguzwa. Kinyume na haya, kazi zinazotengana kimtindo na kimaudhui panadhirisha tofauti baina kazi zinazohusika. Macha (keshatajwa) anaeleza kuwa mwangwi wa kimatini huashiria kuwa kazi ya fasihi imeazima matamko kutoka kwa

matini nyingine. Mwingilianomatini unaweza kutokea kisinkronia ambapo kazi za fasihi zilizotungwa katika vipindi tofauti vya kihistoria zinaweza kuchota malighafi ya utunzi kwa njia inayoathiriana. Kiprotich na wenzake (2021), wanaeleza kuwa waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuathiriana kupitia usimulizi wa matukio wakati wa kutunga kazi zao. Kwa hivyo, maandishi ni kipengele kinachoendeleza mwingiliano baina ya waandishi katika sanaa ya uandishi. Maelezo ya wataalamu hawa ni muhimu kubainisha kuwa kazi za mwendelezo ni kazi madhubuti zinazotokana na kazi asili au za jadi. Kwa hivyo, tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* imelazimika kuingiliana kimtindo na kimaudhui na tamthilia tangulizi ya *Mashetani* ili iweze kwenda na usasa na upya wa matini za baadaye.

Masatu na wengine (2020), wanasema kwamba mwingilianomatini ni dhana inayotumiwa kuhakiki kazi za fasihi ili kutathmini kuwepo kwa athari za mwingilianomatini. Matini zinaweza kufanana kimtindo na kimaudhui kati ya kazi mbalimbali. Kwa waandishi wanaotumia mwingilianomatini huonyesha namna kazi za fasihi huathiriana kupitia matini za awali na hulenga kuziandika upya kazi hizo za awali na wakati mwingine kwa njia ya kubeza. Mwendelezo katika kazi za fasihi unaweza kutokea kidainkronia ambapo matini zilizotungwa mahali pamoja na hujitenga historia na kimazingira hulinganishwa. Waandishi wa ubaadausasa katika tamthilia ya Kiswahili hutumia mwingilianomatini kuyahakiki na kuendeleza mawazo ya kazi za awali ili kutafuta njia mbadala ya kuzisoma kazi hizo na kupindua usomaji wa uliozoeleka wa matini hizo (Garci, 2015)

Kwa mujibu wa Deigner (2005), kuna aina nyingi za mwingilianomatini ambazo watunzi wa matini za fasihi wanakumbatia katika utunzi wa matini. Kulingana naye, kuna aina tatu za mwingilianomatini. Aina ya kwanza inahusu urejeleaji dhahiri wa kazi nyingine ambapo mwandishi anataja waziwazi kazi yenyewe, wahusika au mwandishi wa kazi anayoirejelea. Aina hii huchunguza nukuu za moja kwa moja za kazi tangulizi. Aina ya pili, anaeleza kuwa mwandishi anaweza kurejelea kazi ya mwandishi mwingine kwa njia isiyo dhahiri bila kumweleza msomaji kuwa mawazo hayo yametokana na matini nyingine. Hivyo mwandishi wa kazi ya fasihi anaweza kurejelea jambo lililo kando na kazi anayowasilisha kwa hadhira yake. Urejeleaji wa aina hii hujulikana kama urejeleaji usiyo-dhahiri. Aina ya tatu, inahusu uhusiano wa

matini tofauti katika kiwango cha ploti na maudhui. Aina hii ya mwingilianomatini inarejelewa kama mwingilianomatini-linganifu kuonyesha ulinganifu wa matini moja na nyingine katika kiwango cha ploti na maudhui. Utafiti huu ilibainisha viwango vya mwingilianomatini vilivyoendelezwa katika tamthilia za *Mashetani Wamerudi* (2016).

Pitio la maandishi lilibainisha kwamba tafiti za awali ziliangazia suala mwingilianomatini katika tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu ulichunguza tamthilia mbili teule. Aidha, utafiti ulilenga kuziba pengo hili kwa kuchunguza mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Mtafiti alichunguza mwendelezo wa maudhui katika tamthilia ya *Mashetani* ulivyoathiri Said Mohamed katika utunzi wa tamthilia yake. Kazi hizi zilitumia mada zilizo na dhana ya mwendelezo katika ujenzi wa maudhui, mtindo na viwango vya kimwingilianomatini. Vilevile, katika mada za kazi teule kulikuwa na dhana ya mwendelezo ambayo ni mbinu ya uandishi iliyotawala utafiti huu.

### 1.2 Suala la Utafiti

Matini mbalimbali za fasihi zinaweza kuingiliana kwa namna moja au nyingine. Hili ni jambo la kawaida ambalo hutokea katika fasihi za ulimwengu. Aidha, mwandishi mmoja anaweza kumwathiri mwingine kwa njia moja au nyingine licha ya tofauti za wakati, umri, eneo au utamaduni. Hali hii ndiyo humwezesha mhakiki kuelewa matini fulani kwa kuihusisha na matini nyingine za awali alizodurusu. Tafiti zilizotangulia zimeshughulikia mwingilianomatini kwa kuegemea wahusika na fani. Uchunguzi huu unadhamiria kuonyesha kwamba hakuna utafiti wa kimwingilianomatini kuhusu kazi zinazolenga tapo la kihistoria kimazingira umefanyika hapo awali. Kuna haja ya kufahamu uhusiano uliopo baina ya tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016), matini ambazo zinawakilisha vipindi tofauti vya kihistoria. Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Mwangwi wa *Mashetani* unasikika unaposoma tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kama ilivyo katika tamthilia tangulizi ya *Mashetani*. Licha ya kwamba kazi hizi zina tofauti za kihistoria na kimazingira kuna uwezekano masuala au matukio katika kazi ya E. Hussein yanajitokeza na kuendelezwa katika kazi iliyofuatilia ya Said Ahmed Mohamed. Utafiti huu, ulidhamiria kuchunguza

mwendelezo huu kwa kuangazia viwango vya taathira, mtindo na maudhui baina ya tamthilia teule.

### 1.3 Madhumuni ya Utafiti

i. Kuchunguza mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetan*i (1971) katika *Mashetani Wamerudi* (2016)
ii. Kutathmini athari za kimtindo katika *Mashetani* (1971) kwenye *Mashetani Wamerudi* (2016)
iii. Kubainisha viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016)

### 1.4 Maswali ya Utafiti

i. Mwendelezo wa maudhui ya tamthlia ya *Mashetani* unajitokeza vipi katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*?
ii. Je, kuna athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* zinazojitokeza kwenye tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*?
iii. Je, tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinadhirisha viwango vya kimwingilianomatini?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Uteuzi wa mada hii ya utafiti kimsingi ulichochewa na misingi kwamba matini za fasihi huathiriana na kuchangizana. Ebrahim Hussein ni mwandishi ambaye ameleta taathira kubwa katika utunzi wa tamthilia. Athari zake zinaonekana katika watunzi wa baadaye kama vile Said Ahmed Mohamed. Tamthilia ya *Mashetani* ina taswira ya kipindi cha ukoloni na tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* inaonyesha tapo jipya la historia ya utandawazi ambalo halijaangaziwa katika tamthilia ya *Mashetani* (1971). Katika tamthilia ya *Mashetani*, Ebrahim Hussein aliangazia mwelekeo wa nchi za kiafrika baada ya kupata uhuru. Naye mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anashughulikia mifumo iliyobuniwa na mkoloni ili kuendeleza dhamira yake ya unyanyasaji na udikteta kupitia mifumo ya kiuchumi, kibiashara na siasa. Kwa hivyo, tamthilia hizi zina mpito wa kiwakati takribani miongo mitano. Utafiti huu ulichunguza mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) katika *Mashetani wamerudi* (2016). Utafiti huu umedhihirisha kwamba kuna tafiti chache ambazo zimefanywa kuhusiana na tamthilia

ya *Mashetani Wamerudi* hasa kuhusiana na suala mwingilianomatini. Jicho la tahakiki limebainisha kuwa waandishi wa tamthilia wameibuka na mbinu mpya ya utunzi wa tamthilia ambayo ni mwendelezo wa kazi za awali. Kwa hivyo, mwandishi anaweza kutaja na kuendeleza mawazo ya mwandishi fulani katika matini yake. Ni kwa msingi huu utafiti huu umedhibitisha viwango vya mwingilianomatini vilivyoendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

Waandishi wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) wameandika tamthlia zao katika vipindi tofauti vya kihistoria na kimazingira, jambo ambalo mtafiti alibainisha aliamua kutafiti zaidi kuhusu namna ambavyo kazi teule zinavyoathiriana. Isitoshe, kazi zimebainisha mwendelezo wa kimtindo na kimaudhui katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu umedhihirisha kuwa kazi ya Said Mohamed ni mwendelezo wa matini tangulizi ya *Mashetani* (1971)

**1.6 Umuhimu wa Utafiti**

Taaluma ya fasihi inaweza kufaidika kutokana na mchango wa matokeo ya utafiti huu, kwa sababu utawapa wanafunzi, walimu wa fasihi na wataalamu wa fasihi ujuzi wa kuhakiki tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu ni mchango katika mtaala mpya wa umilisi katika kuwapa wanafunzi na wakuza mitaala mbinu za kuimarisha tamthilia zinazopendekezwa katika mtaala mpya wa elimu hasa katika taaluma ya fasihi linganishi.

Utafiti huu pia umechangia katika kuonyesha jinsi Said Ahmed Mohamed ameathiriwa na kufaidi pakubwa mbinu za kiutunzi kutokana na usomaji wa tamthilia ya awali ya *Mashetani* katika uandishi wake. Utafiti huu utachangia katika usomaji wa tamthilia ya Kiswahili kwa kuonyesha matini za watunzi wanaoegemea nadharia ya mwingilianomatini katika kutunga kazi zao kwa kuongeza maarifa ya fasihi hasa kwa wasomi wanapohakiki dhana ya mtindo, usimulizi na uhusika katika tamthilia. Vilevile, waandishi watanufaika kutokana na kufichuka kwa dhana ya mwendelezo kama mbinu mpya katika uandishi wa matini za fasihi.

### 1.7 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Suala la mwingilianomatini ni pana, utafiti huu ulihusisha tamthilia mbili za Kiswahili zinazowakilisha vipindi tofauti vya kihistoria ili kubainisha uhusiano uliopo baina ya tamthlia ya *Mashetan*i (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Ebrahim Hussein aliaminika kwa kutunga kazi zilizo na taathira kubwa katika utunzi wa baadaye hasa tamthilia ya *Kinjenketile* (1969), *Jogoo Kijijni* (1976) na *Arusi* (1980) zinaonyesha taswira ya Kikoloni. Naye Said Mohamed amebuni tamthilia kama vile *Amezidi* (1995), *Pungwa* (1988) na *Kivuli Kinaishi* (1990). Tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) ziliteuliwa huku *Mashetani* inawakilisha yaliyomo katika kipindi cha ukoloni nayo tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* inawakilisha karne ya kisasa ikiangazia athari za ukoloni mamboleo hasa athari ya utandawazi. Utafiti huu ulijikita katika kutathimini athari za mwingilianomatini baina ya tamthilia mbili ili kuchunguza jinsi zinavyohusiana. Mwendelezo wa kimaudhui na kimtindo una ukaribiano wa kihistoria katika jamii zilizosawiriwa ulichunguzwa ili kutimiza malengo ya utafiti huu.

## 1.8 Maelezo ya Istilahi

**Matini:** Ni kazi za fasihi za Kiswahili zilizoandikwa au kusemwa

**Mwanda:** Ni istilahi inayotumiwa kuonyesha na kuelezea upana wa kimahusiko wa matini ya fasihi.

**Mwangwi:** Neno hili linatumika katika fasihi kumaanisha kwamba kazi ya fasihi inamrejesha msomaji katika kazi nyingine aliyotangulia kusoma kwa usasa.

**Mwengo:** Ni istilahi inayotumiwa kurejelea arufu au rihi ya kitu fulani katika muktadha wa kazi za fasihi zilizoandikwa.

**Mwingiliano Matini:** Ni kuhusiana kwa kazi za fasihi pale ambapo matini au zinarejeleana na matini mbalimbali kupitia mbinu za uandishi.

**Matini Teule:** Kazi zilizoteueliwa kwa minajili ya kufanya utafiti ambazo ni tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MAANDISHI

## 2.1 Historia Fupi ya Ebrahim Hussein

Ebrahim Hussein anajulikana kwa utunzi wa tamthilia ya *Mashetani* na *Kinjekitile* ambazo zimo miongoni mwa tamthilia nne alizochapisha. Hussein anafahamika sana katika uandishi wa tamthilia ya *Mashetani* (1971), aliibua mtindo mpya katika uandishi kutokana na jinsi alivyotumia wahusika na utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Ebrahim Hussein alizaliwa wilayani Lindi, Tanzania mwaka wa 1943, Hussein alijulikana kwa umaarufu wake wa kuandika mchezo wa maigizo Afrika Mashariki. Ni msomi na nguli wa fasihi ya Kiswahili, pia alipata kazi kama mhadhiri wa kufunza sanaa ya Maigizo Chuo kikuu nchini Tanzania. Mnamo mwaka wa 1975 hadi 1985 hadi kustaafu kwake mwaka wa 1988 ambapo alishida tuzo ya mwandishi bora wa tamthilia ya Kiswahili nchini Tanzania. Ebrahim Hussein alipata tuzo ya UWAVITA ambayo hupewa waandishi nguli wa tamthilia ya Kiswahili, mwandishi huyu amekuwa kwenye ulingo kwa muda mrefu na kazi zake zinasomwa katika kila pembe ya Afrika Mashariki. Pia Hussein anajulikana kwa mchezo wa kuigiza, *Alikiona,* (1967) na *Wakati wa Ukuta* (1969), kazi hizi zilihusu mada ya mgongano na mabadiliko. Baadaye alitunga kazi ya Sokomoko mwaka huo huo. Vile vile mchezo *Kinjekitile* ulitolewa mwaka wa 1969.

Mnamo mwaka wa 1971, alichapisha tamthilia ya *Mashetani*, tamthilia ambayo inahusiana na kuonyesha jinsi siasa na uchumi zinavyoingiliana. Pia tamthilia hii imejengwa kwa kutumia jazanda ili kuonyesha mgogoro uliopo baada ya kupata uhuru, kauli hii inaonyesha jinsi viongozi fulani ambao walitumia nafasi zao kisiasa kuwadhulumu raia wao. Kazi zingine za Hussein zinazojulikana kama vile; *Arusi* (1980). *Jogoo Kijijini* (1976) na *Ngao ya Jadi* (1976), vilevile alitunga tamthilia ya *Kwenye Ukingo wa Thim* iliyochapishwa 1988 inayoonyesha mvutano katika jamii pamoja na harakati za kuleta mabadiliko. Kwa kifupi, Ebrahim Hussein ni miongoni mwa waandishi tajika na ambaye aliweka misingi mipya ya kiutunzi kama kama vile matumizi ya fasihi simulizi katika uandishi wa tamthilia.

## 2.2 Historia Fupi ya Uandishi wa Said Ahmed Mohamed

Said Ahmed Mohamed anajulikana katika uandishi wa tungo mbalimbali za fasihi kama vile, riwaya, ushairi, hadithi fupi na tamthilia. Said `Mohamed alizaliwa mwaka wa

1947 katika Mwembeladu, Pemba. Japo alizaliwa Mwembeladu, alianzia masomo yake katika shule ya msingi ya Wete Boys huko Pemba wakati wa ukoloni. Katika mwaka wa 1963-1966, alijiunga na shule ya Upili wakati wa ukoloni iliyoitwa Kings George the vi. Baada ya kufaulu, alijiunga na chuo cha mafunzo ya Ualimu cha Nkurumah hadi mwaka wa 1967-1968. Baada ya masomo ya chuo kikuu kukamilika alifunza shule ya Msingi ya Kizimbani huko Pemba. Baadaye aliamua kusoma masomo ya Sanaa ambapo alijitosa katika uga wa Kiswahili, siasa na sayansi. Said Ahmed Mohamed alipata nafasi ya kuingia Chuo kikuu cha Dar es Salaam kati ya mwaka wa 1976 ambapo alisomea Fasihi ya Kiafrika masomo mengine. Baada ya kukamilisha masomo ya chuo kikuu alirejelea nyumbani Zanzibar na kuwa mwalimu mkuu katika shule ya Hamamuni, Unguja kati ya mwaka wa 1981, alirudi chuo kikuu cha Dar es Salaam kwa kusomea ya shahada ya Uzamili (Isimu). Ni mwaka huo pia alikwenda Ujerumani na kusomea shahada ya Uzamivu na kuhitimu mwaka wa 1984 katika chuo kikuu cha Lepzing.

Baada ya kuhitimu shahada ya Uzamifu alirudi nyumbani na kuwa mkurungenzi wa TAKILUKI katika mwaka wa 1985-1987. Katika mwaka wa 1987, alipata kibali cha kufanya kazi katika chuo kikuu cha Eldoret katika Idara ya Kiswahili.Baadaye aliamua kuhamia chuo kikuu cha Nairobi mwaka wa 1987 na kuwa mkuu wa Idara ya Kiswahili. Hatimaye, aliondoka na kuelekea Japani alikofanya kazi mwaka wa 1990-1997 kabla ya kuhamia Ujerumani katika chuo kikuu cha Beyreuth kati ya mwaka wa 1997-2012.

Said Ahmed Mohamed alianza kutunga shairi linalojulikana kama "*Sauti ya Unguja".* Shairi lake la kwanza kupelekwa Redioni lilikuwa, *Nimfunge ndege Gani Nimpate Salama?* Hatimaye alijitosa katika kazi za kinathari (hadithi), hadithi yake ya kwanza kutunga ilijulikana kama *Mzee Hamisi Leo Wapi*, hadithi aliipeleka BBC, hadithi zake fupi alizipeleka katika kituo cha Idhaa ya Kiswahili ya BBC, ambapo hadithi zake zilishinda mwaka wa 1970. Vilevile aliandika *vitabu vya misemo, vita vya Hekima, methali* na *misemo ya mshanga.* Said Ahmed Mohamed alianza kutunga riwaya, riwaya yake ya kwanza ilikuwa *Asali Chungu* (1994) kisha akatunga shairi, *Sikate Tamaa (*1980) na baadaye riwaya ya *Dunia mti mkavu* na *Utengano* (1980*), Jicho la Ndani* (2008), *Nyuso za Mwanamke* (2010), *Babu Alipofufuka* (2001), *Tata za Asumini* (1990), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), *Mhanga Nafsi yangu* (2011), *Dunia Yao* (2006),

*Dunia Mti Mkavu* (1980) na vingine kadha. Hivi karibuni alitunga tamthilia ya kisasa yenye anwani ya *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwa hakika kazi za S.A Mohamed zimetafitiwa sana. Hata hivyo, tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* haijapata kutafitiwa katika mkabala wa mwendelezo wa kimwingilianomatini. Hata hivyo, utafiti huu ulihusisha tamthilia mbili, *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016), tamthilia zitachunguzwa kwa kuzingatia nadharia ya Mwingilianomatini.

## 2.3 Historia Fupi ya Tamthilia

Tamthilia ni utanzu wa fasihi andishi katika lugha ya Kiswahili (Wafula, 1999) Mtaalamu huyu anaeleza kuwa tamthilia ya Kiswahili ina historia ndefu nchini Kenya ambapo ilianza kushughulikiwa katika miaka ya Hamsini. Tamthilia ya Kiswahili inahusishwa pakubwa na majilio ya wakoloni ambao walijenga misingi ya tamthilia ya Kiswahili nchini Kenya na Afrika Mashariki kwa jumla. Tamthilia ya kwanza ya Kiswahili ilitungwa na Hyslop 1945. Kazi yake iliyojulikana kwa jina *Akili Mali* ni kiungo muhimu katika historia ya tamthilia ya Kiswahili. Kazi zingine alizotunga ni pamoja na; *Afadhali Mchawi, Mchimba Kisima na Kukopa Harusi Kulipa Matanga,* zilizotolewa katika mwaka wa 1974.

Henry Kuria, ambaye alikuwa mwanafunzi wa Hyslop alitunga tamthilia yake kwa jina *Nakupenda lakini* katika mwaka wa 1953. Tamthilia hii ya Kuria iliigizwa na wanafunzi wa shule ya upili ya Alliance na kuendelea kuimarisha tamthilia ya Kiswahili. Hatimaye, Gerishon Ngugi aliandika tamthilia ya *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi* katika mwaka wa 1961. Kazi hizi zilikuwa muhimu katika kuweka msingi wa tamthilia ya Kiswahili nchini Kenya. Aidha, zilichapishwa kabla ya uhuru nchini Kenya.

Baada ya uhuru nchini Kenya kulishuhudiwa uchapishaji wa tamthilia mbalimbali, kwa mfano tamthilia mbili za Ebrahim Huseein kwa jina *Wakati wa Ukuta* (1967) na *Alikiona* (1969) zilichapishwa katika mwaka wa 1969. Baadaye tafsiri nyingi za tamthilia zilitolewa katika mwaka huo huo wa 1969, kwa mfano, '*Tufani*, S.S Mushi, Julias Kaizari na *Mabepari* wa *Venisi* (1967) J.K. Nyerere katika mwaka huu. Ebrahim Hussein alichapisha tamthilia ya *Kinjekitile,* (1969). Vipawa vya kutunga tamthilia vilizidi kubainika mnamo mwaka wa 1971 ambapo Hussein alijitoma tena uwanjani na kudhibiti baharia ya utunzi wa tamthilia kwa kutoa tamthilia ya *Mashetani*. Hussein

aliweka mtindo wa aina yake katika tamthilia ya Kiswahili. Pamoja na tamthilia ya *Mashetani* kuchapishwa katika mwaka wa 1971, kazi nyingine kama Mfalme Juha ya Forouk Topan pia zilitolewa. Ni wakati huu ambapo tafsiri mashuhuri ya *Mfalme Edipode* ilipotoka, tafsiri hiyo ilitolewa na S.S Mushi.

Mnano mwaka wa 1977, Ebrahim Ngozi alitunga tamthilia ya *Machozi ya Mwanamke* huku Katalambulla akichapisha tamthilia mbili: *Unono* na *Mizani ya Imani Yangu*. Tafsiri ya *Mzalendo Kamathi* ilitafsiriwa na Ngugi wa Thiong'o wakiwa na Micere Mugo katika mwaka wa 1978. Tamthilia ya *Mkwara na Uhehe,* ilitolewa katika mwaka 1979 na M.M. Mulokozi. Katika mwaka huo huo, Felix Osodo alitoa mchezo wake *'Hatari kwa Usalama* uliowavutia wengi. Kitabu cha *Mkaguzi mkuu wa Serikali* kilichotafsiriwa na Christon Mwakasaka pia kilichapishwa mnamo mwaka wa 1979 na kuwavutia wasomaji.

Miaka ya 1990, tamthilia zilizochapishwa ziliimarika kimtindo na kimaudhui, tamthila katika miaka hii zilitumia mbinu ya mtindo wa uchangamano katika kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Tamthilia hizi zilijihusisha na maudhui ya baada-ukoloni na kuchunguza athari za kutegemea mataifa ya nchi za kigeni ili kuendesha uchumi wa mataifa ya Kiafrika (Wamitila, 2002). Kutokana na orodha ya baadhi ya tamthilia zilizoandikwa kuweka msisitizo kadha katika mifumo ya uongozi wa mataifa machanga ya Kiafrika, inasadifu kwamba pia tamthilia hizi ziliangazia masuala ya kihistoria yaliowahi kutokea Afrika ya Mashariki. Aidha, mitindo inayotumiwa na watunzi wa tamthilia imekuzwa kulingana na ujumbe unaokusudiwa kuwasilishwa. Katika karne ya ishirini na moja, utunzi wa tamthilia umeimarika pakubwa kiufundi na kifani kutokana jinsi waandishi wanavyotumia lugha kuwasilisha dhamira zao. Baadhi ya waandishi wa tamthilia ya Kiswahili wamejitoma katika utunzi wa tamthilia zenye maudhui yanayoangazia masuala ambayo yanaathiri jamii ya kisasa hasa utandawazi, uongozi, teknolojia, uhifadhi wa mazingira, na haki za kibinadamu. Ukaribiano huu wa kidhamira huathiri usomekaji wa kazi ya fasihi na kuiruhusu matini tangulizi na kuonekana kama mwendelezo wa aina fulani ikilinganishwa na matini za baadaye. Ni katika mawanda haya, utafiti huu umedhihirisha ni kwa kiwango gani matini tangulizi (*Mashetani,* 1971) iliathiri *Mashetani Wamerudi,* S.A Mohamed.

## 2.4 Maudhui na Mwingilianomatini

Suala la mazingira na utamaduni huathiri utunzi wa matini ya fasihi. Athari za kimazingira huwa na mchango mkubwa katika kazi ya fasihi. Waandishi waliokulia katika mazingira yanayowiana huathiriana katika tungo zao. Mazingira huibua sifa za kimwingilianomatini baina ya watunzi wa matini za fasihi. Vipengele vinavyoathiriana ni maudhui, mtindo na usawiri wa matukio. Wamitila (2002), anaeleza kwamba mwandishi anapoanza kutunga kazi yake huwa ameathiriwa na mazingira yanayomzunguka. Kwa hivyo, matini yake huwa imeathiriwa kwa kiwango fulani kwa sababu huwa waandishi wanatumia lugha ile ile kurejelea matukio ya mazingira yanayowazunguka. Wamitila (keshatajwa) anaeleza kuwa jambo linawatofautisha waandishi waliokulia mazingira yanayofanana ni historia yao pamoja na urejeleaji wa muktadha wa matukio. Kwa hivyo, utafiti wa Wamitila unadhihirisha kwamba mazingira ni kipengele muhimu katika utunzi wa matini ya fasihi. Hata hivyo, mwandishi wa matini hawezi kujitenga na mazingira yake wakati wa kubuni matini yake. Kuna vipengele ambavyo hujitokeza bila kukusudia kwa sababu mwandishi huwa ni zao la historia inayomzingira. Tofauti na utafiti huu ni kwamba utafiti huu ulibainisha jinsi ambavyo matini teule zinaathiriana kwa kuangazia mwendelezo wa kimaudhui katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Wamitila (2003), anasema kwamba mwingilianomatini unajitokeza katika viwango vingi kupitia usimulizi wa matukio, usawiri wa mazingira na msuko wa kazi yake. Hata hivyo, mwandishi anaweza akalizungumzia suala ambalo mwenzake alizungumzia kwa namna ambayo labda anaendeleza, anapinga au anakosoa. Wafula (2007), anasema mwingilianomatini ni kipengele chenye uhusiano mkubwa na usemezano, unapochunguza mwangwi wa kidhamira. Aidha, kazi za zamani hupiga mwangwi katika matini za fasihi zilizopo. Katika matini zilizopo kuna urejeleaji wa kazi nyingine unaweza kuwa wa moja na mtindo wa mtunzi fulani. Hali hii hutokea wakati ambapo mwandishi huwa amechota na kuendeleza mtindo wa uandishi wa mwandishi aliyemtangulia. Hali hii hutokea kwa sababu lugha ni kipengele ambacho hakijifungi na mazingira. Huwa wanaathiriana kimatini na kimtindo na hata kiwahusika. Wafula (keshatajwa) anaashiria kwamba, wakati unaposoma matini fulani ya kifasihi, unaona mwendelezo wa kimaudhui na kimtindo. Maelezo haya yalifaa utafiti huu katika kubainisha matukio yaliyomo katika kazi Hussein ambayo yanavyopiga mwangwi na

kuendeleza masuala fulani ya kimaudhui na kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Wafula (2007), anaeleza kuwa kitendo cha kazi za zamani kupiga mwangwi katika kazi zilizopo ni cha kimwingilianomatini, kwa kuwa upo mwendelezo wa baadhi ya mawazo ya kazi za mwandishi mmoja dhidi ya mwingine. Matini za fasihi zinaathiriana na hutagusana na kazi nyingine za kifasihi. Hoja anayoibua Wafula (keshatajwa) ni kuwa mwendelezo wa kazi za awali ni mbinu inayotumiwa na waandishi kuonyesha kwamba kazi zao zimetokana na usomaji wa kazi za awali. Vilevile, mwendelezo hujitokeza kuonyesha kwamba kazi zinazobuniwa zinaathiriana katika ujenzi wa mtindo na maudhui. Kwa hivyo, matini itakayobuniwa itakuwa na miundo yanayoashiria urejelezi wa tungo za awali. Utafiti huu uliangazia mawazo ambayo yanajadiliwa katika tamthilia teule ya *Mashetani* ya E. Hussein na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Kazi za kiubunifu huwa na sifa ya kimwingilianomatini kutokana na sauti tofauti zinazoingiliana na kazi zilizotangulia katika mawanda ya kimwingilianomatini Lemaster (2012). Kazi ya fasihi inayofuatilia huwa na misingi yake kutoka kwa kazi ya awali. Utafiti wa Lemaster (keshatajwa) unaonyesha kuwa matini za fasihi huwa zinaathiriana na kurejeleana kimadhui na kidhamira katika usimulizi wa matukio. Hii ina maana kuwa matini ya fasihi huonyesha mtindo wa kiusemi ambao huonyesha ukaribiano na matini tangulizi. Utafiti wa Lemaster (keshatajwa), ulifaa utafiti huu katika kubainisha kuwa matini za fasihi zina ukaribiano na matini zilizotangulia kwa njia moja au nyingine. Tofauti ni kuwa utafiti huu ulionyesha jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameiga mtindo wa usimulizi kama mbinu ya kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Mwingilianomatini katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) *na Kijiba cha Moyo* (2016) ulishughulikiwa na Ngesa (2014). Anaonyesha kwamba historia huchangia katika mwingilianomatini; historia ni dhana isiyojifunga katika mawanda ya kiwakati na kimaeneo katika fasihi. Aidha, alibaini kwamba mwandishi wa tamthlia ya *Kijiba cha Moyo*, aliathiriwa na matini tangulizi ya *Mashetani* kutokana na jinsi Ebrahim Hussein alivyotumia kipengele cha lugha kufanikisha dhamira yake. Alionyesha ithibati

kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Kijiba cha Moyo* ( 2009) alichota, kumnukuu na kuiga baadhi ya vipengele vya mtangulizi wake E. Hussein katika tamthilia ya *Mashetani*. Aidha, ufafanuzi na maelezo yake kuhusu nadharia ya mwingilianomatini ulifaa utafiti huu katika kuelewa mihimili ya nadharia hii. Utafiti wa Ngesa (keshatajwa) ni dira kuwa waandishi wa matini za fasihi wanaweza kuathiriana kupitia kipengele cha kihistoria. Tofauti na utafiti hii ni kuwa ulibainisha mwendelezo wa maudhui katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Utafiti wa Adam (2015) ulibainisha kuwa kuna nyanja mbalimbali za mwingilianomatini ambazo huwa zinaathiri wandishi wa matini ya fasihi katika mawanda kama vile urejelezi wa wahusika, mawanda ya mandhari, matukio na jalada la kitabu. Aina nyingine ya mwinginomatini unaonyesha kuathiriana na kuingiliana kwa matini ya kifasihi. Kwa hivyo, mtafiti aliona kuna haja ya kuchunguza mwingiliano wa vipengele vya lugha katika tamthilia ya Kiswahili. Adam (keshatajwa) anaonyesha kwamba matini za kifasihi huundwa kutokana na matini zilizotangulia, hakuna matini ya fasihi inayoweza kudai kuwa imekamilika bila kuhusishwa na matini nyingine ya kifasihi. Aidha, kazi za fasihi huhusiana kwa njia mbalimbali. Vilevile, matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana. Hata hivyo, mawazo ya Adam (keshatajwa) yalifaa utafiti huu kubainisha viwango vya kimwingilianomatini vinavyoibuliwa na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi.*

Bosibori (2016) ameshughulikia mwingilianomatini katika tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege, 2009*)* na *Mkaguzi Mkuu wa Serikali Gogola, (*1979). Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Aligundua kwamba tamthilia hizi zinaingiliana na kuathiriana ki-mandhari. Alithibitisha kwamba maudhui katika tamthilia alizotafitia zinaathiriana na kuchangiana ili kuleta ukamilifu wa matini. Alitambua kuwa mandhari huchangia katika utunzi wa kazi za fasihi. Ingawa kuna mfanano wa kimandhari katika kazi alizotafitia, tofauti inajitokeza kwa sababu matini alizotafitia zilitungwa katika katika kipindi fulani cha kihistoria lakini zikaathiriana kimandhari kutokana na jinsi waandishi walivyosawiri wahusika ili kuwasilisha dhamira yake. Sawia na utafiti wake utafiti huu unatumia nadharia ya mwinglianomatini. Tofauti ni kuwa, utafiti huu ulichunguza mwendelezo wa kimaudhui baina ya tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016)

Korir na wenzake (2019) walichunguza vipengele vya mwingilianomatini katika ujenzi wa maudhui ya umaskini katika riwaya ya *Bina-Adam* na *Musaleo*, utafiti ambao uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Walitumia nadharia hii kubainisha uhusiano uliopo wa maudhui ya umaskini katika riwaya hizi. Waligundua kwamba waandishi wa matini za fasihi wamechangamkia nadharia ya mwingilianomatini katika ujenzi wa dhamira zao. Aidha, wahakiki hawa wanasawiri maudhui ya umaskini na kuonyesha jinsi yanavyoingiliana na kukamilishana katika riwaya hizi mbili, wanaonyesha kwamba mwingiliano huu unasababishwa na uhalisia wa matukio yanayotendeka Afrika. Kwa hivyo, utafiti wao una umuhimu kwa sababu unajenga misingi katika kuelewa jinsi nadharia ya mwingilianomatini inavyotumia ujenzi wa maudhui katika tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu hata hivyo, ni tofauti kwa kuwa ulichunguza mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi*.

Kilingo (2019) aliangazia mwingilianomatini katika tamthilia ya *Kifo Kisimani* na *Utenzi wa Fumo Liyongo*. Aligundua kwamba kuna vipengele vya kimwingilianomatini vinavyoaingiliana katika matini hizi mbili. Vipengele vinavyodhihirisha mwingilianomatini ni kama vile; dhamira, maudhui, usimulizi, uhusika na mandhari. Kilingo anaonyesha kuwa Kithaka Wa Mberia katika matini yake ameathirika pakubwa na utenzi wa Fumo Liyongo. Aligundua kwamba matini tangulizi huwa inamwathiri mwandishi katika vipengele vya kimwingilianomatini ambapo athari hizo zinaonekana katika Kifo Kisimani. Utafiti wake unarejelewa kwa sababu vipengele alivyoibua huwa na ukuruba katika kuonyesha jinsi fasihi inavyoathiriana kupitia vipengele mbalimbali. Tofauti ni kuwa, utafiti huu ulibainisha viwango vya kimwingilianomatini katika tamthilia mbili *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) za Kiswahili zilizoandikwa katika vipindi tofauti vya kihistoria.

Mwingilianomatini katika tamthilia ya *Utangamano Wetu Ushidi Wetu* ulishughulikiwa na Masatu (2020). Anaeleza kwamba mwingilianomatini ni mbinu inayotumiwa kutalii kazi za fasihi kisanyansi katika kubaini kuwepo kwa athari za unukuzi na uchopekaji wa mbinu za kifani, kimtindo na kimaudhui katika katika matini za fasihi. Matokeo ya utafiti wake yalithibitisha kuwepo kwa mwingilianomatini unaofungamana na historia, utamaduni na malezi ya mtunzi wa kazi ya fasihi. Kulingana na Masatu, kazi za fasihi

huonyesha ukaribiano wa moja kwa moja katika matini. Ukaribiano huu hutambulika kama mwendelezo wa kimatini. Katika utafiti wake alibaini kwamba mwingilianomatini hufungamana na historia ya mwandishi wa matini kwa namna moja au nyingine. Matokeo ya utafiti wake yalimwongoza mtafiti katika kubainisha kuwa waandishi waliokulia katika mazingira sawa lakini wakatengwa na historia wanaweza kutunga kazi zao kwa njia inayoingiliana kimaudhui. Mwingiliano unaotokea katika kazi zao huwa ni mwendelezo ya masuala na matukio yaliyojiri katika kazi ya awali. Utafiti huu ulitathmini kuwapo kwa mwendelezo kimaudhui ni kiwango gani katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

## 2.5 Mtindo na mwingilianomatini

Nkwera (1977), aliangazia "Utunzi wa Ebrahim Hussein kama mtunzi wa tamthilia" kuwa tamthilia za awali za Hussein zilionyesha athari ya Breitch katika kazi zake. Anaeleza Hussein kama mwandishi ambaye alikiuka kanuni za Ki-aristotle katika uandishi wa tamthilia ya Kiswahili. Nkwera anaendelea kueleza kuwa Hussein alizikiuka taratibu za Kimagharibi katika utunzi wa maonyesho ya jukwaani. Utafiti wa Nkwera (keshatajwa) unaonyesha Hussein ameathiriwa na utanzu wa fasihi simulizi katika matini zake za kifasihi. Kwa hivyo, Hussein amefanikiwa kutumia utanzu wa fasihi simulizi katika kazi zake. Maelezo haya ni mwanga kwa sababu yalifaa katika kuonyesha ni kwa kiwango gani mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amerejelea na kuendeleza matumizi ya fasihi simulizi katika kazi yake.

King'ei (1987) alishughulikia Usanifu wa Lugha katika Utunzi wa Ebrahim Hussein. alibainisha kuwa Hussein ndiye mwandishi ambaye amefaulu kutumia mtindo wa utanzu wa fasihi simulizi katika tungo zake. Ebrahim Hussein ni mwanabadiliko katika utanzu wa tamthilia ya Kiswahili hasa katika matumizi ya fasihi simulizi. Taathira za Ebrahim Hussein zinabainika katika kazi za watunzi wa baadaye wa tamthilia ya Kiswahili kwa kuwa kuna watunzi ambao wameiga na kuendeleza baadhi ya mbinu za uandishi katika tungo zao suala ambalo linaibua dhana ya mwendelezo katika tamthilia ya Kiswahili. Utafiti huu ulibainisha iwapo utanzu wa fasihi simulizi umeendelezwa kama mbinu ya kiutunzi katika watunzi wa baadaye kama vile Said Ahmed Mohamed ambaye tamthilia yake inachunguzwa katika utafiti huu.

Njoroge (1997) alishughulikia vipengele vya kimwingilianomatini katika riwaya za *Tata* za *Asumini* (1990) na *Rosa Mistika* (1971). Aliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Alitalii vipengele vya mwinglilianomatini kama vile maudhui, mandhari, ploti na wahusika. Njoroge alionyesha jinsi riwaya hizi zinavyotofautiana katika kipengele cha wahusika na ploti. Utafiti wa Njoroge (keshatajwa) ulifaa utafiti huu kwa sababu unaonyesha jinsi kazi za fasihi zinavyoingiliana na kukamilishana kupitia dhana ya mwingilianomatini. Utafiti huu ulichunguza mwendelezo wa kimaudhui na kimtindo unavyoingiliana katika tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Ricard (2000), alihakiki kazi mbalimbali za Ebrahim Hussein kwa kuangazia dhana ya mtindo katika utunzi wa tamthilia ya Kiswahili. Katika uhakiki wake, Ricard (keshatajwa) ameonyesha kuwa waandishi wa tamthilia ya Kiswahili wanaosifika sana katika uandishi wa tamthilia na ambao wameleta taathira kubwa ni Ebrahim Hussein. naye Matundura (2012) anasema kuwa *Mashetani* (1971) ni tamthilia ya upeo wa juu kulingana na jinsi mwandishi alitumia fani na vipengele vingine vya lugha katika kufanikisha dhamira yake. Mara nyingi waandishi wa kazi za fasihi huathiriana na kuendeleza vipengele mbalimbali vya kiutunzi katika matini zao. Kauli za watafiti hawa ni muhimu kuthibitisha kuwa, kazi za kimwendelezo ni mbinu mpya inayotumika katika uandishi wa matini za fasihi. Tofauti ni kwamba utafiti huu ulitathmini athari za mwendelezo wa mtindo wa uandishi katika tamthlia ya *Mashetani Wamerudi*.

Njoroge (2022) aliangazia vipengele vya mwingilianomatini katika tamthlia *Kinjeketile* na *Majira ya Utasa* alibainisha kwamba vipengele vya kimwingilianomatini kama vile wahusika, maudhui na mandhari huwa vinahitilafiana katika matini za kifasihi. Njoroge alibainisha kwamba tamthilia hizi zinatofautiana katika kiwango cha wahusika na ploti. Kulingana naye, waandishi wa tamthlia hizi wameathiriana katika kiwango cha wahusika na maudhui katika matini zao. Wahusika katika kazi hizi wamekuzwa na kuendelezwa katika njia ambayo inaonyesha ukaribiano wa aina fulani. Kazi hizi zinaonyesha tofauti kupitia kipengele cha usimulizi. Njoroge anaona kuwa mtunzi wa matini ya fasihi huwa na jukumu la kuamua mtindo ambao atatumia katika kazi yake. Kuna waandishi ambao huwa wanaiga na kuendeleza mtindo wa mwandishi fulani katika kazi zao. Tofauti ni kwamba, utafiti huu ulichunguza ni kiwango gani mwandishi

wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ameiga na kuendeleza mbinu za uandishi za mtangulizi wake katika tamthilia ya *Mashetani* (1971)

Wanyela (2007) alitafiti kuhusu matumizi ya mtindo wa ushairi unavyojitokeza katika tamthilia ya Kiswahili. Katika utafiti huu aliangazia tamthilia tatu za Kiswahili *Kilio Cha Haki* (Mazrui), *Mama Ee* (Mwachofi), na *Amezidi* (Mohamed). Alionyesha namna matumizi ya mtindo wa ushairi unavyojitokeza katika utunzi wa tamthilia ili kuonyesha ujumbe wa mwandishi. Utafiti huu ulionyesha jinsi ushairi unavyochangia katika kuibua na kufanikisha uwasilishaji wa dhamira ya mwandishi. Aligundua kuwa waandishi wa tamthilia wamekumbatia ushairi kama mbinu ya kiutunzi katika kukuza ujumbe na wahusika. Utafiti wake ulidhihirisha kwamba mwandishi huwa anatumia utanzu wa ushairi ili kuzindua jamii ya kisasa. Utafiti wa Wanyela (keshatajwa) ulifaa utafiti huu katika kutathmini mwendelezo wa athari za kimtindo katika matini za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.

Ireri (2011) alishughulikia mwingilianomatini katika tamthilia za *Kinjeketile* (1969) na *Mzalendo Kimathi* (1978). Akirejelea Utendi wa kimasimulizi alionyesha jinsi mafanikio ya kihistoria na kitamaduni yalileta mwamko mpya kutokana na jinsi waafrika walijitoa kishujaa kipigania haki zao. Pia alidhihirisha kuwa watunzi wa tamthilia hizi walisawiri wahusika kwa njia zinazofanana kutokana na juhudi zao za kupigana na ukoloni. Pia alisawiri matukio ya kihistoria katika kuonyesha jinsi alivyowasawiri wahusika kuonyesha nafasi zao za kuleta umoja na ukombozi kutoka kwa mkoloni. Tamthilia hizi zinaelezea hali halisi iliyotokea wakati wa ukoloni katika Afrika Mashariki. Ireri (keshatajwa) ameonyesha kipengele cha kimwingilianomatini kwa kuwalinganisha wahusika mbalimbali katika kazi yake. Utafiti wake ulichangia katika kupata maarifa kuhusu matukio au masuala yanayoweza kuziathiri jamii ya sasa, yaliyowahi kuathiri jamii ya awali kwa njia moja au nyingine. Kwa hivyo, masuala haya yanaathiri watunzi tofauti na hivyo kuibuka na mtindo wa uandishi unaofanana. Tofauti ni kwamba, utafiti huu ulichunguza matumizi ya mwingilianomatini katika kubainisha ni kiwango gani viwango vya kimwingilianomatini vimerejelewa na kuendelezwa katika tamthilia teule.

Mningo (2015) aliangazia tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo. Alihusisha tamthilia ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi* (1988) na *Fumo Liyongo* (2009). Alibainisha jinsi mtunzi wa matini hizi alivyofumbata mbinu ya uingilianomatini katika matini ili kuibua dhamira zanazosawiriwa na tamthilia hizo. Kwa ujumla, aligundua kwamba tamthilia zinaonyesha ukaribiano zaidi wa kiutunzi kuliko kutofautiana kutokana na jinsi mwandishi alivyotumia mbinu ya mwingilianomatini katika ujenzi wa dhamira. Mningo (keshatajwa) alibainisha kwamba mbinu ya mwingilianomatini imehusika pakubwa katika ujenzi wa tamthilia. Vipengele vya fasihi simulizi vinavyoibua mwingiliano ni kama vile; ushairi, visakale na nyimbo. Utafiti wake ulilejerewa kwa sababu vipengele vya fasihi simulizi vilivyoibuliwa katika utafiti wake vimetumika na kuendelezwa katika utunzi wa tamthilia teule. Tofauti ni kwamba utafiti umechunguza ni kwa kiwango gani mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) amethiriwa na kufaidi mbinu za uandishi katika tamthilia ya *Mashetani* (1971).

Saleh (2015) ameshughulikia matumizi ya utanzu wa fasihi simulizi katika kazi mbili za Shabban Robert; *Adili* na *Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad*. Aliangazia matini hizi mbili kwa kuongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Utafiti wake ulithibitisha kuwa matini hizi mbili zinafanana katika vipengele vya fasihi simulizi kama vile ushairi, masimulizi na semi. Pia anaonyesha kwamba, matini hizi zinalandana na kuathiriana katika matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi, ingawa vipengele hivi vya fasihi simulizi havijatumika vyote kuna mfanano ambao umetumika kujenga dhamira ya mwandishi. Alibainisha kwamba, ijapokuwa matini hizi zilitungwa na mwandishi mmoja, kuna mwingiliano baina ya kazi hizi. Aidha, utafiti huu wa Saleh (keshatajwa) ulirejelewa kwa sababu vipengele vya fasihi simulizi kama vile ushairi vimetumika katika tamthilia teule, kwa hivyo utafiti huu uliangazia jinsi vipengele hivi vimetumika na mwandishi katika kufanikisha dhamira yake. Tofauti na kazi yake iliyorejelewa, utafiti huu ulibainisha viwango vya kimwingilianomatini katika tamthilia teule.

Salum (2018) ameangazia tathmini ya vipengele vya fasihi simulizi katika utunzi wa Ebrahim Hussein. Utafiti wake ulihusisha tamthilia za *Ngao ya Jadi, Jogoo Kijijini na Mashetani*. Alitambua kwamba tamthilia hizi zinafanana kupitia vipengele vya fasihi

simulizi kama vile: Matumizi ya wahusika wa kisimulizi, mtindo wa ishara, nyimbo na ngano. Salum anaona kuwa matumizi ya vipengele vya fasihi simulizi ilitumika katika kufanikisha dhamira yake. Anaonyesha kuwa tofauti inayojitokeza katika tamthilia teule ni matumizi ya mianzo na miisho huwa tofauti. Kwa hivyo, kazi za Ebrahim Hussein zimesheheni athari za kimtindo za fasihi simulizi. Utafiti wa Salum ulifaa huu katika kubainisha athari za Ebrahim Hussein katika waandishi wa baadaye. Tofauti ni kwamba utafiti umechunguza athari za kimtindo katika tamthilia teule.

Mose na wenzake (2020) walichunguza taswira katika tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika tamthilia nne za Kiswahili mathlan: *Mashetani, Pungwa, Ngoma ya Ng'wanamalundi*. Waligundua kwamba kuna ukuruba katika mwingiliano wa kimtindo na kimaudhui baina ya tungo hizi kwa sababu watunzi hawa wameathiriwa na tungo za E. Hussein. Walibainisha kwamba waandishi wa kazi hizi walikumbatia utanzu wa sanaa ya jadi katika kazi zao. Vilevile, walibainisha kwamba matini zilichotwa na waandishi wa kijadi kwa sababu ya kuiga malighafi ya utunzi katika matini zao. Wanaonyesha kwamba kazi zilizorejelewa zinaonyesha ukaribiano kutokana na jinsia watunzi hawa wamekumbatia dhana ya kimwingilianomatini kutokana na urejelezi wa kazi ya awali. Hata hivyo, utafiti wa wataalamu hawa ni muhimu katika kazi hii kwa sababu unaonyesha kitaswira jinsi tamthilia ya Kiswahili inavyoingiliana na sanaa ya kijadi katika mawanda ya kimwingilianomatini. Utafiti huu ni muhimu katika kubainisha jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* alivyorejelea na kuendeleza mtindo wa uandishi wa mtangulizi wake Ebrahimi Hussein. Hata hivyo, utafiti huu ni tofauti kwa sababu ulitathmini za athari za kazi ya Ebrahim Hussein, *Mashetani* (1971) ilivyoendelezwa kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016).

**2.6 Viwango vya Kimwingilianomatini katika fasihi**

Nduti (2000), ameteua baadhi ya filamu za drama zinazowasilishwa katika mashindano ya shule nchini Kenya. Alihakiki baadhi ya filamu kama vile: *Zeinabu Rudi Nyumbani* (2008) na *Billy Mbilikimo*, *Chasing Moses* (2009) na *Alexander Kostantarus* na *The village Cassanova* (2010) na Simon Nduti. Katika kazi hizi, alitafiti vipengele vya mwingilianomatini kutokana na kazi mbalimbali zinazowasilishwa katika filamu teule. Kulingana na Nduti (keshatajwa), filamu za drama huwa zinaathiriana kwa sababu

huwa zinaangazia masuala mbalimbali ya kijamii na kiutamaduni. Filamu hizi huwa zimeundwa kwa namna ambayo huwa ni kazi tofauti lakini zinatokana na marekebisho ya filamu za awali. Kwa kuwa mtindo wa uwasilishaji wa filamu za drama huwa tofauti lakini masuala yanayoibuliwa huwa yanaathiriana na matukio mbalimbali katika jamii. Utafiti wa Nduti umechunguza suala la mwingiliano jambo ambalo lilichunganuliwa katika utafiti huu. Hata hivyo, utafiti kuhusu mwendelezo wa viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia ya Kiswahili haujangaaziwa katika tamthilia teule.

Nzuki (2003), amehakiki uingiliano wa matini katika diwani za *Mchezo wa Karate* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Alizingatia nadharia ya Sosholojia kuonyesha jinsi waandishi wa kazi za fasihi wanavyoathiriana katika kipengele cha fani na maudhui. Utafiti wake ulibainisha kuwa mwandishi anapobuni kazi yake huwa ameathiriwa na mazingira ya kiutunzi. Amethibitisha kuwa mazingira ni kipengele muhimu kinachoibua dhamira ya mwandishi kutokana na jinsi kipengele cha fani kimetumika katika kukuza dhamira ya kazi yake. Utafiti wake ulifaa huu kwa kuwa ulisaidia katika kuelewa mazingira ya kiutunzi ni dhana inayoibua mwingilianomatini katika kazi za fasihi. Utafiti wake uliegemea kiwango cha uingiliano baina ya matini zilizotungwa katika vipindi tofauti vya kimazingira. Utafiti wa Nzuki (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa kuwa ulitafitia viwango vya kimwingilianomatini baina ya tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi.*

Kehinde (2003), alitafitia matumizi ya mwingilianomatini katika riwaya zilizotungwa na Chinua Achebe. Utafiti wake uliteua riwaya za *Things Fall Apart* na *Arrow of God*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Utafiti wa Kehinde (keshatajwa) ulithibitisha kwamba Chinua Achebe aliathiriwa na usomaji wa matini zilizotangulia, matini ambazo Chinua Achebe alirejelea katika utunzi wake ni pamoja na: *King Solomon's Mines* (Rider Haggard) *Heart of Darkness* (Joseph Conrad) na *Mister Johnson* (Joyce Cary). Utafiti wa Kehinde ulithihirisha kwamba Chinua Achebe alirejelea na kuchota baadhi ya mbinu za kiutunzi kutoka kwa kazi za awali alizotangusana nazo katika uandishi wa kazi zake. Urejelezi wa matini za awali unaonyesha taathira kutokana na jinsi Chunua Achebe alivyoendeleza mbinu za lugha na maudhui katika ujenzi wa dhamira ya ukoloni. Utafiti wa Kehinde (keshatajwa) ulifaa huu kwa sababu ulibainisha kuwa mwandishi wa matini ya fasihi huathiriwa na

kazi alizotangusana hapo awali. Tofauti na utafiti huu ni kuwa ulibainisha mwendelezo wa viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia zilizoteuliwa.

Deigner (2005), amehakiki uingiliano wa kazi teuele za Euphrase Kezilahabi ambazo ni: *Nagona na Mzingile* na *Ziraini na Zirani* ya Wiliam Mkufya. Utafiti wake uliangazia kipengele cha msuko akiongozwa na nadharia ya mwingilianomatini. Alibainisha kuwa waandishi wa matini za fasihi hubuni kazi zao kwa kuziegemeza na kazi za awali. Deigner alionyesha kuwa, matini hizi zinaathiriana katika kipengele cha maudhui kutokana na jinsi mwandishi alivyotumia mtindo unaofanana hasa kipengele cha msuko katika ujenzi wa maudhui. Kazi hii ya Deigner (keshatajwa) ni muhimu katika kubainisha kuwa waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuathiriana katika kipengele cha msuko katika uwasilishaji wa dhamira katika kazi zao. Utafiti wa Deigner (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa sababu ulibainisha mwendelezo wa viwango vya kimwingilianomatini katika tamthilia teule.

Peter (2015), aliangazia Uingiliano katika kazi za wanafunzi eneo la Tharaka Nithi Kaunti. Utafiti huu ulibainisha kuwa mwingilianomatini umejitokeza katika matini ambazo wanafunzi wamekumbana nazo hapo awali. Utafiti wa Peter (keshatajwa) umethibitisha kuwa wanafunzi wengi wameathiriwa na kazi za fasihi kutokana na jinsi wamezirejelea katika uandishi. Matokeo ya utafiti wake yalibainisha kuwa kuna taathira uliyoachwa na kazi ambazo wanafunzi wamesoma na kuzidurusu hasa za fasihi zinazojitokeza katika kazi za nathari wanazotunga wanafunzi. Utafiti wa Peter unalingana na huu kwa kiwango fulani kwa sababu uliangazia uingiliano kama kipengele kinachoibua mwingilianomatini. Tofauti inayojitokeza ni kuwa utafiti huu ulibainisha mwendelezo wa viwango vya kimwingilianomatini katika tamthilia teule za Kiswahili.

### 2.7 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na Julia Kristeva (1986). Suala la mwingilianomatini limetafitiwa na wataalamu mbalimbali (Kristeva, 1986, Bakhtin, 1981, Allen, 2000, na Deigner, 2005) wataalamu hawa wamebainisha kuwa msomaji wa kipekee nimwandishi anayesoma matini nyingine ya fasihi na kuiona kazi hiyo kama kazi anayojisoma. Kazi iliyotangulia inajipata katika

kazi ya sasa, baadhi ya sehemu ya kazi ya awali huwa na uwezo wa kuathiri kazi ya sasa na kuwa wigo wa kazi ya awali. Eagleton (1983) anaeleza kuwa, matini za fasihi huwa kwa kiwango fulani zimeandikwa tena na waandishi ambao mara nyingi hawatambui kwamba wametunga kazi zao kama za wengine. Kulingana naye hukuna usomaji wa matini ya fasihi ambao ni asilia: kila usomaji huwa wa kusoma matini ambayo imeandikwa tena. Mwingilianomatini unaweza kuonekana kama upanuaji wa mawazo kama dhana ya kisasa inayotumika kuchukua nafasi ya kuathiriana kupitia usomaji na utunzi wa kazi yenyewe.

Mwingilianomatini ni dhana inayotumiwa kuelezea kwamba maana ya matini inatokana na matini nyingine. Waandishi wa kazi za fasihi hawatungi kazi zao kutokana na mawazo yao, wanazitunga kazi zao kutokana nakazi iliyotangulia. Kwa hivyo utunzi wa kazi za fasihi ni mseto wa maumbo na matukio mbalimbali. Sauti zilizopo kwenye matini wakati huu zinaweza kuwa mwangwi wa sauti za wakati uliopita, mwangwi wa sauti nyingine mbalimbali. Julia kristeva ndiye mwasisi wa nadharia hii baada ya kuiboresha nadharia ya Usemezano ya Mikhail Bakhtin miaka ya 1960. Mwasisi huyu anaona kwamba hakuna kazi yoyote ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake bila kuhusishwa matini nyingine. Mwingilianomatini, kwa hivyo, ni hali ambapo matini fulani huomba mawazo yake kutoka kwa kazi zingine au zilizotangulia. Mahali ambapo matini mbili au zaidi zinapoingiliana na kuwa na sifa zinazofanana kama vile usawiri wa matukio na maudhui. Kristeva anakiri kuwa mwingilianomatini na hali ambapo matini moja husomwa katika mwanga wa matini nyingine. Anafafanua kuwa lazima kuwe na kazi ya fasihi inayohusiana na nayo katika mtindo mbalimbali kama vile muundo, ujenzi wa wahusika, dhamira pamoja na vipengele vya lugha. Hii ina maana kwamba matini ya kifasihi hupata maana kwa sababu kuna vipengele fulani vya matini hiyo vinavyohusiana na matini tangulizi.

Kristeva (1969) anaeleza kuwa matini huwa zinategemeana na kuhusiana na kazi za fasihi zilizopo au zilizotangulia. Matini ya fasihi ni mkusanyiko wa kazi kadhaa zinaohusiana na kuingiliana kimatini. Waandishi wa matini za kifasihi huunda kazi kutokana na kuathiriwa na matini ambazo walitangulia kusoma. Kauli hii ina maana kwamba watunzi wa matini za fasihi hawabuni matini zao kutokana ubunifu wao bali ni kutokana na kuathiriwa na mkusanyiko wa kazi walizotangulia kusoma. Maelezo

haya ya Kristeva yalichangia katika utafiti kwa sababu yalikuwa mwanga katika kuchunguza mwendelezo wa *Mashetani* (1971) katika *Mashetani Wamerudi* (2016)

Kwa mujibu wa Plotell na Charney (1978) mwingilianomatini unasisitiza kwamba kazi za kifasihi zilizoandikwa au zilizosemwa zinaweza kuchukuliwa kuwa matini moja na yenye kujibizana kila moja ikikamilishwa na nyingine, kwa hivyo, kazi za fasihi zinachota maana kutokana na matini nyingine katika upeo wa kuingiliana na matini tangulizi. Dhana ya mwingilianomatini inaeleza kwamba kazi za fasihi kuchukuliwa kama matini moja ambapo kazi hizi huingiliana na nyingine katika usemezano. Hivi ni kusema kwamba hakuna kazi ya fasihi inayojitokeza kivyake bila kuhusishwa na kazi ya awali. Kauli hii ya wataalamu hawa ina maana kwamba matini ya kisanaa haitokani na mawazo ya mwandishi mmoja tu bali ni matokeo ya jinsi kazi hizo zinavyohusiana na kazi mbalimbali ili kuleta ukamilifu wa maana.

Kwa mtazamo wa Bosibori (2016) msomaji wa matini za kifasihi hastahili kujifunga katika matini moja pekee ila anafaa kuzisoma na kuelewa matini zilizotangulia. Kazi ya kifasihi huundwa kutokana na matini za kisanaa zilizotangulia. Aidha, anafafanua kwamba matini moja inaweza kuingiliana na kuhusiana na matini tangulizi ili kuonyesha uhusiano uliopo baina ya matini zilizoitangulia, uhusiano huu ndio unarejelewa kama ‘mwanda wa kimwingilianomatini’ mwanda hapa ukirejelea maana ya upana wa mtindo na maudhui, uhusika, mandhari na dhamira. Msingi huu wa nadharia ya mwingilianomatini ulifaa katika utafiti katika kubainisha jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) kufaidi na kuendeleza mtindo wa uandishii za Ebrahim Hussein ambaye ni mtangulizi wake katika tamthilia ya *Mashetani* (1971)

Matini huwa inaundwa kutokana na maandishi kadha yaliyotolewa kutoka kwa tamanduni nyingi ambazo huwa zinaingia katika mahusiano kupitia dayolojia au usemezamo wa aina fulani (Bakhtin, 1981). Mhakiki huyu anaona kwamba mwandishi wa matini kama mtu ambaye ameathiriwa na jamii, utamaduni wake na mila. Anaendelea kusema kwamba mwandishi wa kazi ya fasihi huwa hajifungi tu katika matini moja, ila kazi yake inatokana na matini nyingine, maana ya kazi ya fasihi huwa imekamilika kutokana na kuhusiana na kazi zilizotangulia matini hiyo. Bakhtin

anamaanisha kwamba matini huwa na sauti tofauti zinazoathiriana na kupiga mwangwi wa matini bunilizi tangulizi. Kulingana na Bakhtin (keshatajwa) kila matini ya fasihi huwa ni mwendelezo wa matini ya awali. Kwa hivyo, kazi za kifasihi huingiliana na kukamilishana na hakuna kazi ya fasihi ambayo inajitosheleza bila kuhusishwa na kazi nyingine. Utafiti huu ulitathmini iwapo kuna athari za moja kwa moja za kimtindo na kimaudhui zinatokana na matini za *Mashetani* (1970) na *Mashetani Wamerudi* (2016).

Kulingana na Bakhtin (1986) mtindo wa uashiriaji kama mbinu za lugha huwa ni jibu la matini za awali. Kwa hivyo, matini iliyoandikwa huwa na upekee kwa vile matini inayochunguzwa inahusishwa na matini nyingine ya awali. Bahktin anashikiria kwamba matini huwa zinaingiliana na zinaweza kuchanganuliwa pamoja ni mchakato ambao unakubalika. Anaongeza kuwa, uhusiano baina ya matini moja na nyingine ni kitu ambacho mwandishi hawezi kuepuka ambapo mwandishi huwa amechota au kunukuu mwandishi aliyetangulia katika uandishi wake. Wakati mwandishi anapoandika kazi yake huwa kuna na mawazo yanayomjia na ambayo ni mwangwi wa matini zilizotangulia ambazo huwa zinasemezana. Ni kutokana na mwingilianomatini ambapo kuna usemezano baina ya matini nyingine. Mwandishi anaweza akataumia maneno au usemi wa mwandishi mwingine katika kazi yake. Maelekezo haya yalifaa katika utafiti huu katika kubainisha maana za matini zinazochunguzwa. Kwa mfano utafiti huu ulichunguza mwendelezo wa kimtindo ulitumika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

Allen (2000) anaeleza kuwa mwingilianomatini ni njia ya kufasiri matini inayolenga wazo la juu. Matini za kifasihi husomwa katika mwanga wa matini na hakuna matini inayotokana na ombwe tupu. Nadharia hii inashikiria kwamba maana ya kazi ya fasihi haipatikani katika matini yenyewe. Matini ya fasihi inajengwa kutokana na mseto wa matini zilizotangulia. Hii ina maana kuwa kazi ya fasihi huwa inarejelea wazo, tukio au utanzu wa fasihi kwa njia moja au nyingine. Nadharia hii inahusisha ukopaji wa maneno kutoka kwa matini mbalimbali. Kila mwandishi kabla ya kuandika kazi yake huwa kwanza amesoma kazi mbalimbali kabla ya kuzamia mchakato mzima wa uandishi wa kazi ya fasihi. Yeye hufanya hivi kwa kurejelea baadhi ya kazi za waandishi wengine waliotangulia. Allen (keshatajwa) anaendelea kusema kwamba mwandishi pia anaweza kuwa ameathiriwa kupitia njia mbalimbali. Utafiti huu

ulibainisha iwapo kuna mwendelezo wa kimtindo na kimaudhui unaotokea baina ya tamthilia teule ni wa kimaksudi na ulisababishwa na usomaji tamthilia ya *Mashetani* (1971).

Waandishi wa matini za fasihi hawaegemei maneno waliochagua kutokana na mifumo ya lugha, ila wana jukumu la kuchagua lugha watakayotumia katika ujenzi wa msuko, mbinu za uandishi na namna ya usimulizi wa matukio katika kazi zao (Zengin, 2019). Mwandishi wa kazi ya fasihi hujipata katika mifumo miwili ambayo ni; mifumo ya kiisimu na mifumo ya kifasihi. Ingawa kazi ya fasihi huonekana kutokana na kuhusishwa na mila na utamaduni wa jamii, kuna vipengele ambavyo mwandishi wa matini hawezi kuvitenganisha na jamii. Mwandishi huingiliana na kutagusana na jamii aliyokulia na kuathiriwa kwa njia mbalimbali (Clayton, 2012). Baadhi ya vipengele vinavyojitokeza katika jamii ni kama vile; utamaduni, mila na vipengele vya fasihi simulizi kama nyimbo. Kauli za wataalamu zinadhihirisha kuwa wakati mwandishi anatunga kazi yake huwa uhuru wa kurejelea na kuendeleza matukio aliyokumbana nayo katika ujenzi wa matini wa matini mpya.

Kwa kutumia Nadharia ya Mwingilianomatini, mihimili mikuu ifuatayo itaongoza utafiti huu:

i. Kazi ya fasihi huwa inarejelea mawazo ya mwandishi mwingine kwa kunakili matini tangulizi katika mawanda kimaudhui na kimtindo. Kwa hivyo, mtunzi wa matini ya fasihi huwa amechota na kuiga kazi ya mwandishi aliyetangulia. Mtunzi hufanya hivi kwa kuiga mtindo wa mwandishi. Hii ni kwa sababu kazi ya fasihi huhusishwa na matini nyingine inayohusiana nayo. Kwa hivyo mwandishi anapounda matini yake, hufanya hivyo kwa kusoma kazi nyingine. Matini zilizotangulia huweka misingi na kanuni kwa kazi za baadaye. Mhimili huu ulisaidia katika usomaji na uelewa wa kazi teule ili kuweza kujibu maswali ya utafiti.
ii. Msomaji au mwandishi wa kazi ya fasihi huwa kama kikamilisho cha matini tangulizi. Kwa hivyo, mwandishi huwa amebadili, kuunda na kueleza upya kazi yake kwa kiwango cha juu ili kuambatanisha matini yake iwiane kwa namna fulani na mwandishi aliyemtangulia katika mtindo ili kujenga matini yenye ukamilifu.

Mhimili huu ulitumika katika kuchunguza na kuathamini mwendelezo wa kimaudhui na kimtindo katika mataini teule.

iii. Mwandishi wa matini ya fasihi hugeuza uasili wa kazi tangulizi ili kuonyesha mabadiliko ambayo yamefanyiwa kazi ambazo zinaingiliana na kuchangiana kwa kiwango fulani, hufanya hivi katika urejelezi wa mtindo wa uashiriaji wa mwingilianomatini. Mwandishi wa kazi ya fasihi hujihusisha na kukusanya na kupanga yaliyokuwepo hapo awali ili kuunda matini nyingine. Mhimili huu una mchango katika kutathmini ni kwa kiwango gani tamthlia ya *Mashetani Wamerudi* (2016) ni mwendelezo wa tamthlia ya *Mashetani* (1971)

iv. Matini ya fasihi haiwezi kuangaliwa kivyake, matini za fasihi huundwa na kazi zilizotangulia. Hii ina maana kuwa matini za kifasihi huwa hazijitegemei ili kuleta maana inayojitosheleza. Matini hupata maana kamili kwa kuhusishwa na matini nyingine ya awali. Mhimili huu ulisaidia katika kuhakiki jinsi tamthilia zilizoteuliwa.

Kutokana na misingi hii, mwingilianomatini ni nadharia stadi za kitaaluma zinazochunguza, na kubainisha uhusiano uliyopo kati ya matini moja na matini nyingine, ili kubaini athari za moja kwa moja au kimwangwi zinazotokana na kazi hizo kuingiliana na kukamilishana. Kauli hii ina maana kuwa nadharia ya mwingilianomatini ni mwongozo unatumiwa kuchunguza wa kazi za sanaa, kisayansi katika kuonyesha kuwepo kwa athari ya uchopekaji ama usemezano; yaani kufanana kifani na kimaudhui kati ya matini moja na matini nyingine. Kufanana huko ni kule kwa moja kwa moja au kuwapo kwa ukaribiano.

Kwa kuongozwa na mihimili hii, mtafiti alichunguza na kutathmini vipengele vya kimtindo na kimaudhui vilivyoibuliwa katika tamthilia za *Mashetani* na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu umebainisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa na tamthilia tangulizi ya *Mashetani*. Said Mohamed amerejelea na kuendeleza maudhui na mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake Ebrahim Husein katika kile kinachorejelewa kama mwanda wa kimwingilianomatini, mwanda hapa ukirejelea mwingiliano wa kimaudhui na kimtindo.

### 2.8 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia historia ya Ebrahim Husein na Said Mohamed, mwauo wa maandshi, nadharia na mihimili ya mwingilianomatini. Mihimili ya nadharia hii ilitumika kueleza data ya utafiti huu, kuchunguza mwendelezo wa kimaudhu, kutathmini athari na viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwa hivyo, nadharia hii ilifaa kuchunguza mwingiliano uliopo baina ya kazi hizi mbili.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika maktabani. Ulihusisha uhakiki wa tamthilia teule za Ebrahim Hussein na Said Ahmed Mohamed. Maktaba zilizotumiwa kufanyia utafiti huu ni zile za Chuo Kikuu cha Chuka na Chuo Kikuu cha Kenyatta. Utafiti huu ulihusisha usomaji wa matini na vitabu mbalimbali vinavyohusiana na mada ya utafiti. Mbali na utafiti wa maktabani, mtafiti alidurusu majarida, tasnifu, machapisho pamoja na mtandao ili kupekua masuala yanayohusiana na utafiti huu. Matini zilizochunguzwa zilimwezesha mtafiti kupanua maarifa kuhusu mwingilianomatini

## 3.2 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa kimaksudi ulitumiwa kuteua tamthilia mbili teule. Mathalan: *Mashetani* (Hussein, 1971) na *Mashetani Wamerudi* (Mohamed, 2016). Tamthilia hizi ziliteuliwa kutokana na mambo kadhaa. Suala la kimsingi ni kuwa tamthilia zote mbili zina anwani inayofanana na kuna uwezekano kuwa zinaingiliana na kuathiriana kwa njia mbalimbali. Aidha, Mohamed (2016) ambaye ni mmoja wa waandishi wa tamthilia inayochunguzwa ameathiriwa na tamthilia tangulizi ya *Mashetani* (Hussein, 1971) kwa njia mbalimbali. Kwa hivyo, utafiti huu uliteua tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ili kuchunguza mwendelezo uliopo ni wa aina gani.

## 3.3 Ukusanyaji wa Data

Mtafiti alisoma tamthilia zilizoteuliwa na kuchunguza jinsi mwendelezo baina ya matini unavyojitokeza katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* katika usawiri wa maudhui na mtindo. Utafiti vilevile ulichunguza namna mwandishi alivyokumbatia dhana ya mwendelezo wa kimaudhui kama inavyojitokeza katika kiwango cha elimu, utabaka na ufisadi na kuendeleza masuala na matukio makuu katika tamthilia ya *Mashetani*. Aidha, utafiti ulichunguza vile mtindo unavyodhihirisha kuwa Said Mohamed ameiga na kuendeleza mtindo wa kiutunzi uliotumika katika tamthilia ya *Mashetani*. Pia, utafiti ulibainisha viwango vya kimwingilianomatini na kufichua kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* alikuwa amerejea malighafi ya kazi tangulizi kwa njia inayofanana.

### 3.4 Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu ni wa kimaelezo uliolenga kuchanganua mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi.* Uchanganuzi wa data iliyopatikana ulifanywa kuambatana na malengo ya utafiti ambayo ni: kuchunguza mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi*, kutathmini athari za mtindo katika *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* na kubainisha viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia teule. Uchangunuzi wa data ulifanywa kwa kuzingatia nadharia ya mwingilianomatini ili kueleza kuwa kazi za kimwendelezo zinaweza kukubalika kifasihi. Athari za mwendelezo wa kimtindo zilichanganuliwa kutoka kwa tamthilia teule kwa kutumia mtindo wa kimaelezo.

### 3.5 Uwasilishaji wa Matokeo

Data ya utafiti huu iliwasilishwa kupitia mbinu ya kimaelezo baada ya kukusanywa na kuchanganuliwa. Mtafiti alihakikisha kuwa kila kipengele kilichohitaji kuchunguzwa kinajitegemea kulingana na malengo ya utafiti. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kimaandishi katika sura tofauti kwa kuzingatia suala la utafiti.

### 3.6 Maadili ya Utafiti

Kuna maadili ambayo mtafiti anapaswa kuzingatia ambayo ni muhimu katika utafiti (Kothari, 2009). Suala la maadili katika utafiti linarejelea uendelezaji wa kanuni zinazofaa na kutambulika kwa ukweli katika kundi husika. Mtafiti aliwasilisha pendekezo la utafiti katika kamati ya maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka ili kutathmini uhalisi wa pendekezo la utafiti na kisha kupendekeza kibali cha kufanya utafiti. Hatimaye, mtafiti aliandika barua ili kujitambulisha na kuomba kibali cha kukusanya data kutoka kwa Tume ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Uvumbuzi. Hata hivyo, mtafiti aliorodhesha na kutambua kazi za waandishi na wataalamu wengine katika nukuu na marejeleo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# MWENDELEZO WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA TEULE

## 4.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi* ili kuonyesha namna mwandishi wa alivyoendeleza masuala na matukio makuu katika kazi yake. Sehemu hii ililenga kuchunguza mwendelezo wa kimaudhui baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*.

## 4.1 Utandawazi kama Tapo la Ukoloni Mamboleo

Ukoloni mamboleo ni hali ambapo mataifa yaliyokuwa yakitawala mataifa ya Kiafrika bado yanaendelea kitawala kiuchumi, kielimu, kiutamaduni na kisiasa hata baada ya kuondoka (Kingei, 1987). Tapo hili la ukoloni limekuwa donda sugu barani Afrika. Wakati ambapo mataifa ya kigeni yalikuwa yakitawala bara la Afrika walimiliki taasisi mbalimbali kwa manufaa yao wenyewe. Hatimaye, ukoloni mamboleo umechukua mkondo tofauti katika karne ya ishirini na moja. Wakoloni waliondoka lakini wamebuni mbinu mpya ili kuendeleza uthibiti wa bara la Afrika. Waandishi wa tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wamethibitisha kwamba mfumo wa kikoloni haukuwa na lengo lolote la kufaidi mataifa ya bara la Afrika ila waliendelea kunyakua raslimali za mataifa ya Kiafrika. Kwa mfano: mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameamua kuendeleza historia ya ukoloni mkogwe katika kazi yake. Katika tamthilia yake ametumia dhana ya utandawazi kuonyesha jinsi ukoloni mamboleo umechukua mkondo tofauti katika bara la Afrika.

Ukoloni mamboleo umeendelezwa kupitia taasisi mbalimbali kama vile: tapo la utandawazi, Shirika la Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani. Mashirika haya yanatumiwa kutoa mikopo kwa masharti ili kuendeleza dhuluma na ukandamizaji wa mataifa ya Dunia ya Tatu. Utandawazi ni neno linalotokana na maneno mawili “tanda’’ na “wazi” ni mfumo wa kimataifa unaorahisisha mawasiliano na mahusiano katika nyanja za kisiasa, kibiashara, na kielimu uliojikita katika maendeleo ya teknohama (Kevogo, 2018). Kwa namna hii mataifa changa katika bara la Afrika yameachwa nyuma katika kukubali nyenzo hii katika jamii zao. Taathira ya utandawazi hujitokeza wazi katika mazingira na utamanduni wa jamii husika. Jamii ya Kiafrika imekubali mabadiliko ya sayansi na teknolojia na kukubali uhusiano kati ya wanajamii ili

kuendeleza asasi kama vile elimu, mazungumzo na mawasiliano. Kazi ya fasihi iliyobuniwa huwa na upekee kwa vile matini inayochunguzwa inahusiswa na kazi nyingine ya awali. Kwa hivyo, wakati matini za fasihi zinapoingiliana na kurejeleana huibua dhana ya mwendelezo wa kimatini (Bakhtin,1986). Data ya utafiti huu imedhihirisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameendeleza dhana ya ukoloni kama ilivyoangaziwa katika kazi ya awali ya *Mashetani*. Said Mohamed ameibua tapo la utandawazi kama mbinu anayotumia mkoloni kuendeleza ukoloni mamboleo

Waandishi wa tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wanarejeleana na kuingiliana katika masuala ambayo yanadhihirisha jinsi kazi zao zinakamilishana hasa kwa kusawiri jinsi mataifa ya Afrika yalivyochukua mkondo mpya baada ya kupata uhuru. Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amerejelea kazi ya Hussein na kudokeza kwamba kazi yake inalenga kuendeleza historia iliyoachwa wazi na mtangulizi wake Ebrahim Hussein. Kulingana na Said Mohamed, dharura iliyomshawishi kutunga tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni kuendeleza tapo jipya la historia ya utandawazi ambayo imesambazwa katika kila pembe ya dunia. Mohamed anaonyesha kwamba mpaka sasa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* hajaweza kutunga kazi inayogonga tapo la utandawazi ambalo linaangazia jinsi mataifa yaliyostawi kiuchumi na kisiasa yanavyothibiti mataifa changa ya Kiafrika na kuendeleza ukoloni mambo leo kupitia asasi mbalimbali. Tazama kielelezo:

> …Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani*, alijadili yale aliyoyaona mapema kuhusu mwelekeo wa nchi zetu za Kiafrika zilivyoanza kuchukua mkondo mbaya hasa - kiuchumi, kijamii, kisiasa, kielimu, kisayansi, kiteknolojia na kiutamanduni…
>
> "…***dharura nyingine ambayo inajifichua ni dharura ya mwandishi Hussein ambayo labda angeiendeleza tamthilia ya Mashetani katika tapo la historia ya utandawaazi ambayo limesambazwa kila pande la dunia nzima…Hussein mpaka sasa hajaandika au hajatoa tamthilia inayogonga kwenye usasa mpya wa utandawazi***, ambao ni mfumo wa dunia wenye mchanganyiko wa siasa, uchumi, usafiri, biashara, uhaulishaji wa fedha kwa kasi, Uanahabari, Ugenini, Ukimbizi wa makundi kwa makundi ya watu kuelekea nchi za ng'ambo…"(Utangulizi *Mashetani Wamerudi*, iv)

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed amedhihirisha kuwepo ukoloni mamboleo. Mwandishi anaonyesha dhuluma anazopitia Mwafrika katika

juhudi za kujikomboa. Mohamed anaona kuwa, Hussein angeendeleza tamthilia yake kuonyesha jinsi tapo jipya la historia ya utandawazi limeendelezwa kama taratibu ya kumthibiti Mwafrika. Mataifa yaliyostawi kiuchumi na kisiasa yanaendelea kuathiri matukio mbalimbali kama vile; elimu na uchumi kwa sababu yanamiliki nyenzo za uzalishaji mali katika bara la Afrika. Umwingilianomatini husisitiza kwamba kazi za fasihi zilizoandikwa zinaweza kuchukuliwa kama matini moja yenye kujibizana kila moja ikikamilishwa na nyingine (Plotell na wengine, 1978), Hii ina maana kuwa kazi za fasihi hurejeleana na kuendeleza dhamira katika matini za baadaye. Utafiti huu umetambua kuwa taswira inayosawiriwa na Said Mohamed ni ile inayoonyesha kuwa utandawazi ni mbinu inayotumiwa na Shetani kuendeleza mfumo wake wa uongozi katika mataifa ya Afrika. Mwandishi anaonyesha taswira hii kupitia lugha ya wahusika yenye dhamira ya utandawazi.

Mwandishi anaonyesha kuwa utandawazi una manufaa kwa sababu umerahisisha uendeshaji wa shughuli mbalimbali za kibiashara, na kuchangia katika kueneza utamaduni katika mataifa ya Kiafrika. Said Mohamed katika tamthilia yake anaonyesha taswira kamili ya utandawazi kama nguvu zinazovunjilia mbali mipaka katika mataifa ya Afrika na kuleta makundi mbalimbali kwa misingi ya kupalilia utabaka miongoni mwa wananchi. Anaona kwamba utandawazi umegawanya jamii katika makundi mawili. Kundi lenye kutawala (waliona nguvu) na makundi tawaliwa yasiyo na nguvu. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anaonyesha taswira jinsi jamii ilivyogawanyika katika misingi ya kiuchumi. Mgogoro uliopo katika jamii unaonyesha jinsi mwafrika alivyokengeuka na kusababisha mgogoro wa kiuchumi kama anavyoeleza mwandishi katika kielelezo hiki:

Sauti ya Mtu: Mnasemaje hadhira! Mnasemaje? ***Si mnajua majumba makubwa ya kifahali yanayojengwa na mtu mmoja***? Majumba ya kiasi cha sabini ya tatu. Majumba makubwa makubwa aliyoyajenga mtu mmoja. ***Kisha tazameni kibanda kile kidogo.*** Kimesismama tisti. Ndani atatoka mtetezi. Atakuja Profesa Hafi-Leo-Wala Kesho mtetezi. Pole pole ataingia uwanjani-uwanja wa ***utandawazi. Katika uwanja karibu na kibanda,*** lipo shina la mbuyu. Linaanza kutoa chipukizi. Zinazoota chipukizi. Miaka mingi imepita. ***Kumbukeni U-colony!*** Ambao upo mpaka leo. ***Ukoloni! Au kifungo cha maisha***… (*Mashetani Wamerudi*, Uk. 2)

KITARU: Kwa nini?

JUMA: Sababu nyingi?
KITARU: ***Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono***? (*Mashetani*, Uk. 56)

Katika vielelezo vilivyorejelewa hapo juu, mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* anaonyesha jinsi mataifa yaliostawi kiuchumi yamegawanya jamii katika makundi tofauti, huku kila kundi likiwakilisha jamii fulani. Makundi (mataifa yaliyostawi) yanatumia nguvu zao kukandamiza mataifa katika ulimwengu wa tatu. Lengo la Hussein ni kuonyesha kuwa ukoloni mkongwe kama kichochoro cha kuzingatia maswala kadha. Anaonyesha mienendo ya binadamu baada ya kutoweka kwa ukoloni mkongwe. Hussein anaonyesha taswira kwamba binandamu wanaopatikana katika matabaka mbalimbali yamesababishwa kiuchumi ili bianadamu daima abakie kama mtumwa wa binadamu mwenzake, utengano huu huwa unasababisha uhasama na hawewezi kutangamana kamwe. ***"Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono''*** Kutotangamana huku kunatokana na tofauti za kiuchumi: pia kunaonyeshwa kutokana na fikra za ukoloni. Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* anaonyesha jinsi wafrika walivyoiga fikra za mkoloni na kuendeleza dhuluma dhidi ya Wafrika wenzao kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki:

MTU 1: Wewe…wewe sijui namna gani. Unajiwekaweka nyuma kama mkia. Bwana huu **sasa ni wakati wa mwafrika** sasa lazima ale vizuri, ake mahali pazuri, avae vizuri…nataka tuwaone wafrika wana ndege, meli zao wenyewe, mashamba makubwa. (*Mashetani*, Uk43-44)

Kulingana na mwandishi wa *Mashetani*, MTU I anawakilisha haja ya watu kibinafsi wakati ambapo uhuru unapaswa kuleta usawa kati ya watu wote. Ni dhihirisho kwamba unasadiki imani za kibepari "sasa ni wakati wetu" ina maana kwamba wakati wa wanajamii wengine umepita au bado haujafika. Hizi ni fikra za unyonyaji za kuwatala walio chini yao. Huu ni ukoloni mamboleo.

Kwa upande wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anaonyesha jinsi utambulisho wa jamii ulivyozorota kutokana na kupokonywa nguvu za kiuchumi na mataifa yaliyostawi. Nguvu zinazogawanya jamii katika matabaka kiuchumi na kisiasa. Mwandishi anaonyesha taswira kuhusu majirani wanaoishi katika vibanda na huku

wengine wakiishi katika majumba makubwa ya kifahari. Falsafa ya Said Mohamed ni kuonyesha kwamba, ijapokuwa mkoloni aliondoka, aliacha mbegu ya ukoloni katika fikra za mwanadamu lakini upande mwingine akabuni mbinu mpya ya kuendeleza udhalimu huo ambayo ni utandawazi. Ukoloni mamboleo umeendelea kutawala mataifa ya Afrika na kuingilia katika kila sekta ya serikali kama alivyoeleza Said Mohamed. Tazama kielelezo ;

> Kijana: Pana mashetani hapa.
> Prof: Ndiyo. Walikuwepo. ***Wakafanya hawapo kwa ujanja wao***. ***Sasa wapo waziwazi***. Wamesharudi… Wamesharudi… Wamesharudi. Nakwambia wamerudi! (*Mashetani Wamerudi*, Uk 7)

> KITARU: Huoni, ***lakini kama kila kitendo kina alama ya shetani*** na kila mtu ana nafsi ya shetani. (*Mashetani*, Uk)

Tamthilia hizi zinadhihirisha kwamba, ingawa shetani aliondoka, kila taasisi inayoendesha shughuli katika bara la Afrika ina alama za shetani. Taasisi zilizorejewa ni elimu, uchumi na siasa. Kwa hivyo, ubepari wa shetani umeingilia kila kipengele na kuathiri maisha ya kila siku kama anavyosema Kitaru. Utunzi wa kazi za fasihi ni mseto wa maumbo na matukio mbalimbali. Matini za fasihi zinaweza kuhusiana katika mtindo wa urejelezi wa maudhui. Kazi ya faishi huambatana na mwingiliano uliopo baina matukio yalivyorejelewa katika kazi ya awali (Kristeva, 1969). Matokeo ya utafiti huu yamethibitisha kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* kutokana na jinsi mwandishi alivyoangazia suala la ukoloni mamboleo. Utandawazi ni dhana iliyobuniwa kuwalikisha ukoloni mkongwe ili kuthibiti mataifa ya Afrika kielimu, kisiasa na kiuchumi. Said Mohamed anasisitiza kwamba mashetani bado wapo anaposema kwamba ***pana mashetani hapa''*** Ebrahim Hussein na Said Mohamed wametumia taswira tofauti kuonyesha jinsi shetani alivyotawala mataifa ya Kiafrika baada ya kupata uhuru. Katika karne hii wamejibadilisha sura na kubuni mbinu mpya kama anavyosema mwandishi…*umepewa jina mpya*…*linaloitwa utandawazi*." (katika *Mashetani Wamerudi*, uk 10). Mwandishi anaonyesha kuwa uhuru wa mataifa ya Kiafrika umetawaliwa na utandawazi unaotawala idara mbalimbali katika jamii. Kwa hivyo, jamii ya Kiafrika imelazimika kufuata mkondo unaovuma wakati wa sasa. Mfano huu unadhihirisha ukoloni mbamboleo katika mataifa mengi ya Kiafrika.

Ukoloni mamboleo unarejelewa kama nyenzo au njia inayothibiti na kuongoza mataifa ya Afrika kwa sababu yana uwezo wa kiuchumi na kisiasa kunyonya rasilimali ya bara

la Afrika. Kwa hivyo dhana ya utandawazi imetumika kama jazanda kuwakilisha mataifa yalio na uwezo duniani. Hali hii inabainika kupitia kielelezo hiki:

> Sheta: Ukweli wa kwamba hatuko katika **mfumo wa zamani wa unyonyaji wa ukoloni mamboleo**
>
> Prof: Tokea lini unyonyaji umeondoka katika dunia yenu na yetu? (Anacheka kicheko cha hasira) (*Mashetani Wamerudi*, Uk 18)
>
> Sheta: Wewe huna fadhila. Sisi wadau tunatoa pesa nyingi ili kuwekeza uchumi wetu na wenu maskini
>
> Prof: (*Anacheka kwa nguvu*) **Hizo pesa mnazotupa ni tone la asali analofyonza chozi.** Kisha *kasma* kubwa zinazaliwa na wakubwa. (*Kimya halafu*). Lakini nyinyi mnapokea malisho ndani ya matumbo yenu ya tembo, **kwa uzito wa mabilioni mangapi ya rasilimali na pesa** sijui. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 19)
>
> Mzee Jumai; **Hamwishi kukusanya na kuiba nguvu zetu kwa kutumia sheria?**
>
> Sheta: Tunanunua na kuuza. Ndiyo maisha yetu. Bila hivyo tutakufa! je, kununua na kuua ni jambo la haramu?
>
> Mzee Kitarua: Juu juu ni halali. Chini chini ni haramu. Bila mikataba na sheria zenu za ujanja hamwezi kwenda mbele tena. Kumbuka kwamba nyinyi mna maslahi na sisi tuna maslahi yetu pia. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 45)

Kulingana na kielelezo hapo juu, mwendelezo unaotokea hapa ni kuwa mataifa yaliyostawi kiuchumi yanatumia uwezo wao kiuchumi kughilibu na kunyonya mataifa katika Dunia ya Tatu kwa kuweka sheria kali ili kuendeleza ukatili na ukandamizaji bara la Afrika. Mwandishi anaonyesha taswira jinsi bara la Afrika limebebeshwa mzigo mzito ambao hawawezi kuukabili. Mwandishi anarejelea kasma kwa maana kuwa pesa zinazotokana na mataifa yaliostawi kiuchumi huwa ni fedha zilizotengewa idara fulani kama vile usafiri. Kasma inaangaziwa hapa inaashiria kuwa hizo fedha huwa zinapokelewa ila matunda yake hoyaonekani ndipo Prof katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anasema kuwa ni "*ni tone la asali analofyonza chozi*" Prof hafurahishwi na maendeleo yasiyokuwa na mashiko dhahiri.

Said Mohamed amerejelea wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* kuonyesha sheria zilizowekwa kuongoza biashara baina ya mataifa kuwa ni taswira inayoonyesha mataifa ya Kiafrika yanavyodhulumiwa. Haijulakani wazi kuwa ni utandawazi bali mwandishi anaonyesha kwamba mataifa ya kigeni yanaingia katika mikataba ili yachimbe rasilimali na madini ambapo faida kubwa inatumiwa kuongeza mapato katika mataifa

ya kigeni. Mwandishi anaonyesha taathira ya utandawazi inavyoathiri Afrika kiuchumi kwa kupokea malipo duni.

Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anaonyesha taathira ya utandawazi katika mataifa ya Afrika. Mwandishi anaelekeza hasira yake kwa kila ambacho anakiona kuwa nchi za Kiafrika zimekubali matumizi ya utandawazi bila kuzingatia athari zinazotokana na utandawazi katika jamii. Mwandishi anaonyesha kwamba utandawazi hauna faida yoyote na unatumika kwa njia mbaya hasa uigaji wa utamaduni wa kigeni. Mwandishi anaonyesha hali hii kufuatia kielelezo hiki:

> Msichana: … kusema ukweli kila mtu huiga. Nchi huiga. Kila jamii huiga. Kila utamanduni huiga. Kila asilia hufuatilia yafanywao. Lakini tukubali kizuri na tukiache kibaya. Hasa utamanduni unaopeperushwa na vyombo vya mawasiliano ya teknolojia za kisasa kwa jina la utandawazi. *Tumezipoteza mila na desturi zetu nzuri*. Wazazi hawawezi kuwatazama tena watoto wao na watoto hawajali mbele ya wazazi wao wasione ishara ya ngono. Ikiwa wenzetu wanafanya njia kuepusha watoto wasione ishara za ngono, kwa nini sisi tufuate mabaya pia… (*Mashetani Wamerudi*, uk 36).

Kulingana na mwandishi, utandawazi katika dunia ya sasa umevuka mipaka isiyojali mila na desturi za jamii. Kulingana na Said Mohamed, utandawazi umevunja mkinzano wa wanajamii kiutamanduni. Mipaka iliyokuwepo kabla ya ujio wa mkoloni imevunjwa na hakuna jamii ambayo inaweza kukili kwamba utamanduni wake umebakia kama ilivyokuwa kabla ya wakoloni. Kwa hivyo, utandawazi umejitokeza kama chanzo cha kudhoofika kwa mila na desturi za Wafrika kwa sababu jamii imeiga utamanduni wa kigeni.

Tamthilia hizi mbili zimedhihirisha kwamba utandawazi ni tatizo kubwa iwapo hakuna mikatati itawekwa kuthibiti hali hii. Imebainika wazi kuwa mashetani wapo katika mataifa mengi ya Kiafrika kutokana na jinsi waandishi hawa wamesawiri mbinu anazotumia shetani kuendeleza udhalimu mbele ya Mwafrika. Shetani amebuni nyenzo mpya anayotumia kumnyanyasa binadamu. Kulingana na mwandishi, utandawazi umejitokeza katika vipande tofauti kama vile, misaada, mikopo, biashara na shughuli za kisiasa. Lengo la mwandishi hapa ni kuonyesha bayana kwamba mkoloni amebuni dhana ya utandawazi na kufanya maisha kuwa magumu kwa sababu umevunjilia mbali

mipaka iliyokuwepo hasa kwa kuzingatia mila na desturi za jamii za Kiafrika kwa kusababisha utegemezi, ufisadi na ongezeko la mikopo.

### 4.1.1 Elimu ya Kibwege

Tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinarejeleana kutokana na jinsi zinavyosawiri maudhui ya elimu. Elimu ya kikoloni imemgeuza mwafrika kwa kumfanya awe chini yake daima. Elimu anayopata shuleni na hata katika vyuo vikuu bado haijamfaidi chochote. Mwandishi wa matini anaweza akamtaja na kurejelea kazi ya mtangulizi wake akiwa na lengo la kutumia kazi yake kama msingi wa kazi yake. Kazi ya fasihi huundwa kama njia ya kuendeleza kazi ya awali (Wafula, 2007). Kwa hivyo, matini ya baadaye ni kikamilisho cha mawazo ya kazi tangulizi. Utafiti huu umedhihirsha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ametumia malighafi ya matini ya awali kama msingi wa kazi yake kutokana na jinsi alivyorejelea na kuendeleza maudhui ya elimu katika kazi yake.

Mfumo wa elimu unaotumika katika bara la Afrika umemfanya Mwafrika awe kikaragosi cha Shetani. Ili Shetani awe na uwezo juu ya binadamu anatumia mbinu mpya kumtamalaki kwa ujanja wake na kumkengeusha. Mwandishi anaonyesha kuwa mwafrika anafanywa asiwe na uwezo wa kujifikiria au kufanya maamuzi yake. Mwandishi anaonyesha taashira hii kupitia kielelezo hiki:

| | |
|---|---|
| SHETANI: | Hebu nikunong'enezee, maana siri yenyewe ni kwa lugha ya Kishetani…Liseme neno nililokufunza |
| BINADAMU: | Gashalazeritwas |
| SHETANI: | Liseme nikusikie. |
| BINADAMU: | Geshalazeritwas |
| SHETANI: | Sema kwa dhati yako |
| BINADAMU: | (Anasema kwa dhati) Gashalazeritwas |

Hussein anaonyesha kuwa baada ya Mwafrika kufunzwa lugha mpya na mkoloni, alianza kumtumikia kulingana na jinsi ngoma ilivyochezwa na mtawala wake. Kulingana na Mugambi (1983) '**Geshalazeritwas** ni neno la kiingereza lenye maana kwamba "*Gush it all as it was''* Ina maaana kwamba Mwafrika anapaswa kutupilia mbali utamaduni wake ili awe kiumbe anayestahiki mbele ya Shetani. Kulingana na Hussein elimu ambayo mwafrika alipata ilimfanya awe mtumwa mbele shetani.

Tamthilia hizi mbili zinarejeleana kuonyesha jinsi mkoloni anazidhulumu nchi za Afrika na kuzitawala kupitia mfumo wa elimu ambayo haikidhi mahitaji ya Mwafrika. Hussein anaona kuna haja ya kubadilisha mfumo wa elimu unaotumika katika mataifa mengi ya Afrika. Mhusika Kitaru na Mzee Kitarua bado hawajashuhudia maendeleo yoyote katika mataifa yao hata baada ya kupata elimu ya mkoloni. Mwandishi anaieleza hali kupitia kielelezo hiki. Tazama:

KITARU: Sielewi namna gani au kwa nini nimesoma *Law* katika university. Toka kuanza kusomasoma hivi vitabu vya historia hii, mawazo yangu yamebadilika bwana. Ingewezekana, ningebadilisha ***Faculty***. Haki tena.

JUMA: Haya sasa, mnatutania sasa? Mshahara mkubwa mnapata nyinyi. Heshima, nyinyi. Ubwana, ndiyo wenu. Nani anataka kusikiliza hadithi. Hata grandmother anazijua. (*Mashetani*, Uk 56)

Mzee Kitarua: ***Mpaka sasa hatuwezi hata kutengeneza sindano***! Iko wapi elimu ya matakwa yetu? Iwapi elimu ya falsafa yetu? Kwa nini tunaendelea na mafunzo yanayotoka mbali pasipo kutazama karibu yetu? (*Mashetani Wamerudi*, Uk 42)

Data ya utafiti huu ilioyesha kuwa wahusika Kitaru, Juma na Mzee Jumai walifanikisha mwendelezo wa maudhui ya elimu kutokana na mawazo ya matini teule. Kazi teule zilikuwa na mwangwi kuwa zinarejeleana kutokana na jinsi waandishi walivyosawiri maudhui yao. Kulingana na mhimili wa nadharia ya mwingilianomatini, waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuingiliana na kurejeleana kutokana na jinsi wamekuza dhamira katika kazi zao ( Kristeva, 1981). Upya unaojitokeza katika matini hizi ni kuwa waandishi wanazungumzia ukosefu wa maendeleo katika Mataifa ya Kiafrika. Mwandishi wa *Mashetani* anaona kwamba mataifa katika bara la Afrika yamejengwa kutokana na misingi ya elimu iliyowekewa na mkoloni. Kutokana na hali hii bara la Afrika bado halijashuhudia ubunifu wowote kutokana na elimu ya kikoloni. Hii ni kwa sababu wamekuwa mateka kabisa kutokana na elimu ya mkoloni na wanajiona kama viumbe duni mbele ya mtawala. Hivyo, Kitaru anaona kuwa elimu aliyopata haijamfaidi chochote na angependa kubadilisha hali hii. Kulingana na mtazamo wa Hussein ni kwamba, katika bara la Afrika kuna uigaji wa mfumo wa elimu unatumiwa katika mataifa ya kigeni, lakini elimu wanayopata ni uigaji tu wa teknolojia. Kwa hivyo, hakuna maendeleo yanayoshuhudiwa barani Afrika. Mwafrika anabakia kuwa anategemea usaidizi wa misaada isiyofaa mahitaji yao.

Said Mohamed anaamini kwamba mfumo wa elimu unaopatikana katika mataifa ya Afrika unatokana na uongozi potovu kama inavyodhihirika katika kilelezo hiki..*tena hakuna mwongozo wala msisitizo wa serikali kuendeleza ajira za sekta ya biashara za makampuni au za watu binafsi*..”(*Mashetani Wamerudi*, Uk 57) Baadala ya viongozi kuhimiza uvumbuzi wa teknolojia asilia inayochukuana na mazingira anuwai ya Mwafrika, viongozi waliochukua hatamu za uongozi wanasisitiza uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za kigeni. Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anaonyesha taswira kuwa hadi leo Afrika hakuna ubunifu unashuhudiwa. Mzee Kitarua anasema kuwa “***Mpaka sasa hatuwezi hata kutengeneza sindano”*** (katika *Mashetani Wamerudi,* uk 42) haya ndio masaibu yanayokumba Afrika kwa ujumla. Tamthilia hizi zinarejeleana kwa sababu waandishi wanakejeli maendeleo wanayojivunia Wafrika, hawajagundua lolote kama inavyodhihirika katika vielelezo hivi:

> Kijana 4: “Wananchi watukufu. Nyinyi hasa ndio watukufu. Mimi nataka kutoa dukuduku lililo moyoni. Kwanza elimu tuliyonayo nchini mwetu. ***Elimu hii tulirithi kutoka kwa wakoloni.*** Bila shaka wakoloni hawakuwa na nia ya kutueleimisha sisi kwa ajili ya kupiga hatua na kwenda mbele katika nchi na maisha yetu. ***Elimu tuliyonayo sasa ni elimu inayotandazwa kwa wingi wa nadharia kuliko vitendo vinavyotumiwa kujenga na kutengeneza vifaa na mashine***. Ingawa vyuo vikuu vyetu vinafundisha somo la uhandisi bado hatujaunganisha vitendo vinavyoweza kutupa mapato kwa kutumia mashine na vifaa mbalimbali...” (*Mashetani Wamerudi,* Uk 59)
>
> JUMA: Ungekuwa mjinga ungefanya hivyo. Lakini wewe mjanja. Unajua; fanya kazi leo, pata pesa nyingi. Mi ninatoka kesho university, nakukanyanga chini.
>
> KITARU: Sitakubali hata kidogo. University sio factory inayotoa vipande vya kupatia mshahara mkubwa au inayotoa tikiti ya kuingia katika nyumba ya ubwana. ***University ni pahali pa elimu, pa ujuzi. Ukitaka kujijua hasa… (****Mashetani,* Uk 17)

Mwandishi anadhamiria kuonyesha taswira kamili kuhusu mfumo wa elimu katika bara la Afrika. Utafiti huu umedhihirisha kuwa mwandishi wa tamthlia ya *Mashetani Wamerudi* ameendeleza maudhui ya elimu kwa sababu ameonyesha kwamba elimu ambayo Wafrika walirithi kutoka kwa mkoloni haina manufaa kwao hasa kwa ulimwengu unaowazunguka. Kwa mtazamo wake, elimu wanayoipokea wafrika ni ya kinadharia tu, hawamudu kuunda au kuvumbua chochote kutokana na elimu ya kigeni.

‘…***Elimu tuliyonayo sasa ni elimu inayotandazwa kwa wingi wa nadharia kuliko vitendo vinavyotumiwa kujenga na kutengeneza vifaa na mashine***” Ingawa Kinyume na haya, katika vyuo vikuu, mafunzo ni ya nadharia tu na hakuna vitendo vinavyoambatana na nadharia hizo. Kulingana na Said Mohamed wahandisi waliosoma katika vyuo vikuu hawajatengeneza chochote kwa sababu elimu yao imekita katika nadharia isiyoambatana na uhalisia au matatizo yanayokumba jamii husika. Mfumo wa elimu unaotumiwa unaonyesha kwamba Wafrika hawajatoka katika kivuli cha mkoloni. Hali hii inaonyesha jinsi Juma anavyopendezwa na mfumo wa kuwatala kutumia mbinu za mkoloni, kulingana na Kitaru, Chuo Kikuu ni mahali pa kupata elimu, mahali pa kujijua na kujisaka. Kwa upande wa Kitaru, anaonyesha jinsi alivyobadilika tangu aanze kusoma vitabu vya historia. Mshabaha kati ya waandishi ulionyesha kuwa nadharia ya mwingilianomatini ni mbinu mojawapo ya ubunifu inayotumiwa na waandishi kuonyesha kuwa wamerejelea na kuendeleza matukio yaliyojiri aidha kwa njia ya moja kwa moja au mwangwi wa matini moja unadhihirika katika kazi zingine kwa kutumia mtindo unaofanana kuwasilisha dhamira yao (Wamitila, 2003)

Kwa mtazamo wa Hussein, Kitaru hafikiri kwamba ameingia Chuo Kikuu ili apate mshahara au cheo kikubwa, au mawazo ya kishetani mahali pa kuondoa fikra za kishetani. Said Mohamed anarejelea mazungumzo kati ya Kitaru na Juma katika kazi yake ili kuonyesha mabadiliko ambayo Juma amepitia ili kukubali kwamba wakati ule alikuwa ameongozwa na fikra za kishetani. Kwa upande wa *Mashetani Wamerudi,* Said Mohamed anaonyesha jinsi elimu ya kikoloni imeleta mgawanyiko wa kitabaka katika jamii. Kitarua anasema kuwa alikuwa amefundishwa fikra za kishetani ili kwenda mbele na kupalilia uozo wa shetani ambao ulikuwa wa kukandamiza, kudhalilisha, kuchukua vitu vya watu na kuvunja sheria. Wakati umefika sasa wa kukomesha nguvu za shetani. Kitarua na Jumai sasa wanakubaliana sasa ni vyema kushirikiana na wanaharakati wengine kama vile Prof kukomesha utamanduni wa ukoloni mamboleo. Mihimili ya nadharia ya mwingilianomatini hudhihirisha kwamba mwandishi wa kazi ya fasihi kuathiriana kupitia mtindo wa usimulizi wa matukio na dhamira mablimbali. Usimulizi wa matukio katika kazi za baadaye huwa ni mwendelezo au mfuatilizo wa kazi za awali (Kiprotich na wenzake, 2021). Kwa hivyo, kazi za kimwendelezo ni madhubuti na zinaweza kukubalika katika fasihi ya kiswahili.

Said Mohamed anaona kwamba wakati umefika kuupiga usarifu mfumo wa elimu unaotumika katika mataifa changa ya Kiafrika. Anaeleza kuwa mwafrika amenyimwa uwezo wake na ataonekana kama mhusika asiyeweza kuleta mabadiliko yoyote katika jamii yake iwapo ataendelea kukumbatia elimu ya kigeni. Kinyume na haya, katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anamsawiri Mwafrika kama mwanamapinduzi anayeweza kuleta mageuzi katika taifa lake. Kijana 4 anaona kuwa…kama alivyosema kijana mwenzangu bila kukubali nafsi zetu hatuendi mbali…" (*Mashetani Wamerudi*, Uk 59) muktadha huu unaweza kumbadilisha mwafrika na kumtwika jukumu kama mtawaliwa kuwa yeye mwenyewe anaweza kujinasua kutokana na mazingira yake.

### 4.1.2 Utabaka

Utabaka katika bara la Afrika ulikuwepo lakini haukuwa na ushindani mkubwa kama ulivyokuzwa wakati wa ukoloni na baada ukoloni. Utabaka ni hali ya ukuzaji wa mali au mfumo wa ubepari ambapo mali humilikiwa na kundi la wachache. Wamitila (2006) anaeleza kuwa matajiri ndio wanaowakilisha tabaka la juu huku tabaka la chini nalo likiwakilishwa na wanyonge katika jamii. Tabaka la juu ndio hujumuisha viongozi huku tabaka la chini linajumuisha wanyonge. Naye Eagleton (2011) anasema kwamba mfumo wa kibepari huchangia katika unyonyaji na ukandamizaji na huchangia katika utabaka katika jamii. Ubepari huwa na viwango katika jamii na hutofautina kutokana na kazi ambazo wanajamii wanajihusisha nazo. Kwa kawaida tabaka la juu ndio huwakandamiza wanajamii kiuchumi na kisiasa. Kwa hivyo, dhuluma za kitabaka husababishwa na mifumo ya kisiasa na kiuchumi ambapo wanajamii wa tabaka chini wanadhulumiwa na wanajamii wa tabala la juu. Eagleton anapendekeza mfumo wa kiuchumi unaoweza kudhibitiwa na wanajamii wote bila kubaguana kwa misingi ya kitabaka. Anasema kwamba mfumo wa elimu mpya wa kiuchumi na kielimu unaweza kupunguza na kuleta taswira mpya katika jamii.

Karl Marx (1959), anaeleza kuwa dhuluma wanazopitia wanajamii hutokana na misingi ya kisiasa na kiuchumi, ambapo tabaka linalomiki nyenzo za uzalishaji mali huwa na nguvu kiuchumi. Tabaka la chini huwa la wanajamii wasio na uwezo kiuchumi ila wanategemea jasho lao ili kukidhi mahitaji ya kila siku. Tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinarejeleana kutokana na jinsi suala la utabaka limekuzwa na

kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mahali ambapo matini mbili au zaidi zinapotangusana huwa kuna mwingiliano wa kimaudhui na kidhamira Plottel na wengine (1983). Kazi ya fasihi inaweza kijidhihirisha na kazi nyingine kiwaziwazi na kuendeleza usimulizi wa matukio na masuala yaliyojiri katika kazi ya awali ili kujenga dhamira mpya yenye ukaribiano. Kwa hivyo suala maudhui ya utabaka yameendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kimaudhui.

Mgogoro wa utabaka unarejelewa na mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* katika kazi yake. Hussein anaonyesha dhuluma za ukoloni katika mataifa ya Afrika Mashariki baada ya kupata uhuru. Anaonyesha kuwa jambo la kwanza la serikali lilikuwa ni kunyakua mali ya umma. Mojawapo wa taathira zinazotokana na utabaka ni kuwa wananchi waliopoteza mali yao ikiwemo familia ya Juma. Familia ya Kitaru na ya Juma zilikuwa majirani. Kitaru na Juma walikuwa katika chuo kimoja lakini wanakuza mgogoro kutokana na historia ya familia zao. Mgororo huu unakuzwa na mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* kupitia kauli ya Mzee Jumai katika kupitia kielelezo hiki:

> Mzee Jumai: Waswahili husema, mpandangazi hushuka kinyume na msemo ule uliotandazwa kwa miaka mingi! Na kweli familia yetu yote haikushuka ngazini, bali iliporomka. Zaidi mimi ndiye niliyependa makubwa na madogo tele, kwa kufuata ukweli wa shetani. (*Mashetani Wamerudi*, uk 43)

Said Mohamed anatumia familia hizi mbili ili kuonyesha uhusiano uliopo baina ya familia katika muktadha wa kitabaka ambazo zinawakilisha jamii mbalimbali. Data ya utafiti huu imedhihirisha kuwa familia ya kina Kitaru ambayo imekuwa juu katika ngazi kiuchumi kabla ya kupata uhuru sasa iko chini. Nayo aila ya kina Kitaru imekuwa chini katika hatua ya kwenda mbele kiuchumi kabla ya uhuru imekuwa sasa ikielea juu baada ya mapinduzi. Historia inayozingira familia hizi mbili ni stihizai katika jamii ya kisasa. Kwa hivyo, mgororo huu wa utabaka umevuka mipaka na umekuzwa na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ambapo mwandishi ameamua kuendeleza historia kama inavyodhihirisha katika tamthilia ya Said Mohamed. Umwingiliano katika kazi za fasihi unasisistiza kuwa historia huchangia katika uandishi wa matini zinazoathiriana kimaudhui na kidhamira (Ponera, 2014). Utafiti huu umedhihirisha kuwa mgogoro huu unachangiwa kwa sababu wanajamii hawajasahau historia iliyopita. Mgogoro baina ya Kitaru na Juma ni jazanda ya utabaka unaopatikana katika umma kiuchumi na Kisiasa. Mgongano huu unadhihirika katika vielelezo hivi:

KITARU: Kwa nini?
JUMA: Sababu nyingi.
KITARU: Mojawapo?
JUMA: ***Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono.***
KITARU: Pili?
JUMA: Wewe unaishi leo. Mimi ninaishi jana. Tutakuwaje Marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha kesho yako. Mimi, kila leo yangu ni kidato cha jana zangu. Na kila nikienda huko, ninarudi na hadithi…hadithi za mashetani. (*Mashetani*, Uk,56)

Mzee Kitarua: …nilifundishwa na fikra za ushetani ili kwenda mbele kusikokuwa na mwisho: **Kunyonya, kubana, kukandamiza, kudhalilisha, kuchukua vitu vya watu, kulimbikiza, kuvunja sheria…**

Mzee Jumai: Haya yote si umesahau? Si unajua kwamba kabla ya nyinyi, sisi tulikuwepo katika kunyonya, kubana, kukandamiza, kudhalilisha, kuchukua vitu vya watu. kulimbikiza… ***Usisahahu. Sisi pia tilikuwa wapandangazi kabla ya nyinyi kuwa wapandangazi.*** Kwa hivyo usahau yaliyopita kama nilivyosahahu mimi. Mimi sasa nimeweka fikra ya kuwaelimisha vijana wetu kwa njia nyingine, njia ya umoja na kulinda nchi yetu. (*Mashetani Wamerudi,* Uk 41-42)

Mwandishi wa tamthilia *Mashetani* anadhamiria kuonyesha kuwa jamii zinazopatikana huwa zinawakilisha wanajamii wanaopatikina katika matabaka mbalimbali ya kisiasa na kiuchumi hawawezi kutanganamana pamoja, Kauli hii inarejelewa na Juma anaposema…***mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono"*** Hussein anaonyesha kuwa hali hii inachangiwa na tofauti za kiuchumi na kisiasa bali tofauti hizi zinatokana na fikra na mawazo ya kikoloni. Kwa hivyo, lengo la mwandishi ni kuonyesha kuwa mawazo ya kibinafsi ndio chanzo cha mgogoro baina ya Kitaru na Juma. Katika kazi za fasihi mwandishi huamua kubadilisha matukio mbalimbali kutegemeana na kazi yake ili kufanikisha ujenzi wa maudhui ya kazi teule.

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* anaonyesha jinsi taswira ilivyo kwa sababu tofauti iliyokuwepo baina ya Kitaru na Juma umekuzwa na kuendelezwa katika kazi hii. Mwandishi anaonyesha taswira halisi ya namna tabaka la juu linavyowanyanyasa na kuwadhulumu masikini kulingana na Mzee Jumai, wakati wa mashindano ya wizi na unyang'anyi. Kwa hivyo, mwenye nguvu (tabaka la juu) walifichua mbinu za kujinyakulia mali na kuwadhulumu wanyonge. Ushahidi wa Mzee Jumai na Kitarua unadhihirisha walikuwa wanawakilisha tabaka la juu kabla ya kupata

uhuru kwa kuwa mmoja wao alikuwa anawakilisha tabaka lake. Kutokana na ushahidi kuhusu namna walivyowadhulumu na kuwakandamiza wanyonge wa tabala la chini wote (Kitarua na Jumai) walikuwa wakifuatilia matukio yote yaliyojiri kabla na baada ya mapinduzi ya kujikomboa kiuchumi. Vilevile Said Mohamed anaonyesha juhudi za wazalendo wapya waliungana pamoja baada ya kugundua kwamba historia yao inachangia katika mgawanyiko wa jamii zao. Mzee Jumai aliyekuwa wakati huo anasema kwa; ***Kwa hivyo usahau yaliyopita kama nilivyosahahu mimi. Mimi sasa nimeweka fikra ya kuwaelimisha vijana wetu kwa njia nyingine, njia ya umoja na kulinda nchi yetu…" (***katika***, Mashetani Wamerudi, Uk 43)***

Said Mohamed anaonyesha tatizo lingine kuwa ni uchafu wa roho unaochangia utabaka katika jamii. Uchafu unarejelewa hapa na mwandishi ni dhuluma wanazopitia wanajamii kutokana shughuli zinazothibiti maisha ya kila siku. Mwandishi anaonyesha kuwa jamii zinazowakilisha tabaka la juu huwa na nguvu za kiuchumi na humiliki nyenzo za uzalishaji mali katika jamii. Hali hii imechangiwa na Wafrika walio na tamaa ya kunyakua mali ya umma na kuwanyanyasa kama watangulizi wao. Wafrika hawa wanarejewa na mwandishi kama "*uchafu wa roho''* katika kielelezo hiki. Tazama:

> Kijana 3: Tatizo jingine ni la uchafu. ***Uchafu wa roho zetu zinazotofautisha baina ya makundi ya wachache (tabaka la juu) na wengi (tabaka la wachache).*** Wachache wanaoipakata na kuifurahia nchi kwa sababu inawafaa kwa mapato na maslahi yao. Wengi wanaitemea mate na kuchukia nchi yetu kwa sababu haiwafai kwa ukosefu wa mapato. Pande zote hizi mbili zinataja ovyo neno la ufisadi lakini hakuna hata mmoja anayesema waziwazi au anayechukua hatua kali. Kwa namna hii, sehemu kubwa ya nchi imefyatuka kwa vile magoti ya nchi yenyewe yamevunjika (*Mashetani Wamerudi*, Uk 35)

Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa dhuluma wanazopitia wanajamii katika bara la Afrika hutekelezwa kutoka kwa upande wa watawala. Utafiti huu ulionyesha kuwa kazi za fasihi huwa na mwingilianiomatini kwa sababu kazi ya fasihi hufumwa kutokana na msemo wa urejelezi wa matukio katika kazi tangulizi (Bosibori, 2016). Tamthilia teule zilihusu jamii ya kiafrika ambayo ilikuwa na viongozi waliodhulumu wengine. Kazi ya Said Mohamed ni mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* kutokana na jinsi alivyoendeleza madhui ya utabaka katika kazi yake. Mwandishi anaonyesha jinsi utabaka ulivyokidhiri miongoni mwa wanajamii. Anaonyesha taswira kuhusu makundi

ya wachache (tabaka la juu) hutumia jasho la walio wengi kujinufaisha kiuchumi. Kulingana na Said Mohamed, ukosefu wa maadili ya kujari masilahi ya mwananchi wa kawaida yamechangiwa na uchafu wa roho na ufisadi. Hali hii inachangia utengano katika makundi ya wanajamii kwa sababu unaendelezwa na kundi la walio wachache.

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed anaonyesha kuwa ukombozi wa kiuchumi na kisiasa unahitajika ili kujinasua kutokana na unyonyaji unaoendelezwa na wawakilishi wa tabaka la juu. Katika matini teule, wanajamii wameanza kujigundua na kujisaka upya ili kujikomboa kutoka kwa minyororo ya ukoloni mamboleo. Wanajamii wa tabaka la chini wanashirikiana ili kuwaondoa viongozi na vibaraka wa shetani uongozi kwa kupigania haki na usawa wa kisiasa na kiuchumi kama inavyodhirika katika vielelezo: Tazama

> Prof: Tushikane mtu kwa mtu. ***Kundi kwa kundi.*** Mwananchi kwa mwananchi. Nchi kwa nchi. Udhaifu umo katika kutawanyika. Umoja upo na mshikamano ni silaha yetu (*Mashetani Wamerudi*, Uk 20)

> BINADAMU: …Ukweli ni huu…. ***Kuna lile lipasalo kufanywa***, na yule apasaye kulifanya. Kuna kitendo na mtendaji. Vitu hivi ni kitu kimoja. Ninapoanza na kitendo, basi pale pale ninaanza na mtendaji. Kitendo kinajulikana: azimio lililo mbele yangu. Mtendaji ni mimi…. ***Ukweli lazima utafutwe. Lazima nisafiri, safari ndefu, nikajitafute, nijisake ili nijijue mimi ni nani***? Ili nijue maana ya kitendo changu. (*Mashetani*, Uk 12)

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, anaonyesha kuwa wanajamii wa tabaka la chini wanaungana pamoja ili kuondoa viongozi wakatili waliokuwa uongozini waliomiliki mfumo wa shetani (ubepari). Mfumo huu ulitumika kuwafaidi wachache waliokuwa mamlakani ilihali tabaka la chini linadhulumiwa jambo lililowapelekea kushirikiana pamoja kupigania mapinduzi mapya katika jamii. Mapinduzi katika jamii mpya iliyosawiriwa na Said Mohamed yaliongozwa na Prof ambapo anasisitiza ujenzi wa jamii mpya bila kubaguana kimakundi anaposema "**Tushikane mtu kwa mtu. *Kundi kwa kundi.* Mwananchi kwa mwananchi… (**kutoka *Mashetani, Uk 12)*

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani*, anaeleza kuwa kuna haja ya kujisaka na kujitambua ili kubaini chanzo cha mgawanyiko unashuhudiwa katika jamii yake. Anasema kuwa utengano wa kitabaka unaonyeshwa kupitia fikra alizonazo mwanadamu. Hussein anaona ni bora mwandamu kujua ukweli uliopo katika jamii yake. Mwandishi anaonyesha kwamba azimio jipya ndilo litaleta mapinduzi ya kisiasa na kiuchumi. Kwa mtazamo wake azimio hili atayelianzisha ni binadamu. Mabadiliko haya yote yataanza na binadamu bila kutawaliwa kimawazo na shetani.

Tamthilia hizi zinaingiliana hivi kwamba, baada ya Waafrika kutambua ukweli walianzisha azimio jipya ili kosa lisifanyike tena. Kulingana na watunzi hawa, huu ndio mwanzo wa safari ya kujitambua na kujijua ili kuelewa historia yao ili waweze kupigania mabadiliko. Katika tamthilia ya *Mashetani*, Binadamu (Kitaru) yumo katika harakati za kujaribu kuelewa hali yake katika jamii. Kitaru amezinduka na amegundua kwamba uhusiano wake na Shetani ni wa ukandamizaji. Mwandishi anaonyesha kwamba Kitaru amejua ukweli kwamba tofauti za kiuchumi, kitabaka na kisiasa zimesababishwa na Shetani. Kutokana na uchunguzi huu, imebainika kuwa dhuluma za kitabaka, kisiasa na kiuchumi katika vifungu vilivyorejelewa ni ishara kwamba kuna mwendelezo maudhui ya utabaka kwa sababu wahusika katika muktadha huu wamebanisha kwamba changamoto zinazowakabili zimesababishwa na uhusiano wao na Shetani.

**4.1.3 Ufisadi**

Data ya utafiti huu imedhihirisha mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameendeleza maudhui ya ufisadi katika kazi yake. Mwandishi anaonyesha jinsi ufisadi ulivyotumika kumgeuza mwafrika na kubadili mienendo baada ya mapinduzi. Ufisadi ni neno linalotumika kuonyesha maovu au uharibifu unaotendeka. Pia unaweza kurejelewa kama matumizi mabaya ya mamlaka katika afisi za umma au za kinafsi kwa manufaa yake mwenyewe. Katika mataifa mengi ya Afrika, ufisadi umekidhiri zaidi ikilinganishwa na nchi za kigeni. Ufisadi katika bara la Afrika unaonyeshwa kupitia tamaa ya uongozi na unyakuzi wa mali ya umma. Ukosefu wa sheria mwafaka hasa baada ya mataifa mengi kupata uhuru ulichangia pakubwa katika ufisadi (Kingei,1987). Idara na taasisi mbalimbali zilizoachiwa mwafrika baada ya uhuru ziliishia katika mikono ya viongozi mbadhirifu wasio jali maslahi wa watu. Kutokana na hali hii, bara

la Afrika halijaweza kujitawala na kujitegemea kijamii, kiuchumi, kielimu na kisiasa. Mataifa mengi ya bara la Afrika hayajapiga hatua kubwa kimaendeleo kwa sababu ya kushidwa kupigana na ufisadi. Mojawapo wa sifa ya mwingilianomatini ni kuwa kazi za fasihi zinapofanana katika urejelezi wa matukio, mawazo yaliyoibuliwa katika kazi ya awali huendelezwa katika matini ya baadaye (Kristeva, 1969). Kwa hivyo, kazi ya fasihi husomwa katika mwanga wa matini nyingine.

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* anaonyesha kuwa, punde tu baada ya mapinduzi viongozi waliochukua hatamu za uongozi walijawa na tamaa ya mali na ubinafsi wa wakoloni waliokuwa wakiongozwa na mawazo ya Shetani. Wafrika wengi waliongozwa na mawazo potovu na kuanza kuibia nchi zao ili kujilimbikizia mali iliyokuwa inamilikiwa na mkoloni. Katika muktadha huu kazi ya fasihi huwa inahusiana na utamaduni katika jamii husika kutokana na namna wanajamii inavyoendeleza imani zao katika utekelezi wa shughuli za kawaida. Kwa hivyo, matini ya fasihi huwa imesheheni imani na mawazo yanayotokana na kazi za awali ambao limejitokeza katika matini zinazochunguzwa. Katika tamthilia ya *Mashetani*, huu ndio ulikuwa wakati wa familia ya kina Juma ilikuwa ikielea juu kiuchumi kabla ya mapinduzi na mali yao kumilikiwa na asasi za serikali, sasa familia ya hii ipo chini kiuchumi. Kwa upande mwingine familia ya Kitaru iliyokuwa katika tabaka la chini kiuchumi imebadili sura na kupanda ngazi kiuchumi na kuwa katika tabaka la juu. Familia ya kitaru sasa imejipata katika ukwasi wa kiuchumi, inamiliki mali na hata magari mapya ya bei ghali yaliyonunuliwa na pesa za umma kama inavyodhihirika katika vielelezo hivi:

Baba Kitaru: (anaimba)
Papa pa pa pa pa
I like some money
Papa pa pa pa pa
***I like some money***
Papa pa pa pa pa
(Mama Kitaru anaingia)
**A very good life**
***A very beautiful wife.***
A very good life
MAMA KITARU: ***Gari mpya! Benz!***
(*Mashetani*, Uk 21-22)

Mzee Kitarua: Kwa hali hiyo hata marafiki zangu waliniita majina mengi…mapozi, mpandangazi, limbukeni, kupe,

***bwanyenye, mla mali ya umma… Aaa, orodha ndefu isiyokuwa na mwisho!***

Mzee Jumai: Haya yote si umesahau? Si unajua kwamba kabla ya nyinyi, sisi tulikuwepo katika kunyonyonya, kubana, kukandamiza, kudhalilisha, ***kuchukua viti vya watu***, kulimbikiza, Usisahau. Sisi tulikuwa wapandangazi kabla ya nyinyi kuwa wapandangazi… (*Mashetani Wamerudi*, Uk 41-42)

Umwingilianomatini unaojitokeza katika utafiti huu umedhihirisha jinsi ufisadi umekidhiri katika mataifa ya Afrika kutokana na ubadhirifu unaoshuhudiwa katika bara la Afrika. Viongozi wa walichanguliwa waliadhani kuwa maisha mazuri ni kunyakua mali ya umma na kuishi maisha mazuri kama inavyodhihirisha kutokana na vitendo vya Baba Kitaru…***I like some money…a very good life… a beautiful wife***. Katika wimbo wake anadhihirisha kuwa amekengeuka na kubadilisha tabia baada ya kuingia uongozini. Kulingana Hussein Baba Kitaru ni kielelezo cha viongozi wanaowakilisha bara Afrika wakiongozwa na tamaa ya kujitajirisha bila kujari maslahi ya wanamapinduzi. Kauli zake zinaonyesha kwamba pesa, magari mapya na bibi mzuri ndio uhuru aliyopigania. Hali hii inaonyesha ubadhirifu wa mali ya umma katika bara la Afrika. Licha ya kwamba pesa hizo zinatokana na wizi uliochangia katika kuanguka kwa miradi iliyotarajiwa kunufaisha wanajamii.

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed anadhihirisha kwamba Mzee Jumai na Mzee Kitarua wanakili kwamba waliongozwa na tamaa ya kupata mali ya umma. Kila mmoja aliongozwa na tamaa ya wizi. Kutokana na kauli ya Mzee Kitarua anaposema kwamba alikuwa ***mpandangazi***, ***bwanyenye*** na ***mla mali ya umma*** ni taashira inayoashiria jinsi walivyokengeuka baada kunyakua uhuru. Watunzi wa tamthilia teule wamedhihirisha kuwa katika mataifa mengi ya Kiafrika, ufisadi umekithiri na umesababisha kuporomoka kwa uchumi wa mataifa hayo kama ivyodhihirika katika katika vielelezo hivi. Tazama:

MTU 2: Jana hatukuwa wote pamoja, ***alipo akitusimulia Bwana Mathew juu ya kufungwa kwa ila kampuni.***

MTU 1: Aah, aah! Ndiyo, ndiyo, ndiyo, Aha! Kwani ndiye huyu bwana wenyewe?

MTU 2: Eeh, ***pesa chungu nzima bwana zimepotea***, lakini ndiyo haijulikani kuwa zimeibiwa au zimepotea katika mahasibu. (*Mashetani*, Uk 42-43)

Kijana 5: "…Na yote haya tunayokutana nayo, ndani ya utandawazi ni mambo ambayo yameharibu dunia kwa sababu za ibada za pesa. Ulevi na uasherati umekithiri. Dhuluma ndio mchezo wetu. ***Wizi, ufisadi na unyang'anyi umesamba. Kizazi ambacho hakina vipimo ndicho kinapendelewa. Watu hawamwabudu na hawamwogopi mungu. Sheria za nchi hazifuatwi wala hazitekelezwi***..." (*Mashetani Wamerudi*, Uk 60-61)

Data ya utafiti huu imethibitisha kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* kutokana na jinsi mwandishi alivyosawiri taswira kuhusu Afrika inavyoongozwa na viongozi wafisadi. Kuna ubadhilifu na uporaji wa fedha ambazo zimetengewa miradi katika jamii. Mwandishi wa *Mashetani*, anaonyesha jinsi ufisadi unavyochangia katika kuporomoka kwa kampuni za uwekezaji. Hali hii inadhihirisha jinsi pesa zinazotengewa miradi fulani zina zinapotea na kusababishwa kufungwa kwa makampuni ya uwekezaji katika mataifa ya Kiafrika. Said Mohamed katika tamthilia ya *Mashetani wamerudi* anaonyesha kwamba ukosefu wa sheria mwafaka ndio chanzo cha ufisadi. Mwandishi anaonyesha kuwa kuna sheria zilizotungwa lakini hazitekelezwi wala hazifuatwi na viongozi walio mamlakani.

MTU 1: WEWE…wewe sijui namna gani. Unajiwekaweka nyuma kama mkia. Bwana, huu sasa wakati wetu. ***Mwafrika sasa lazima ale vizuri, akae mahali pazuri…avae vizuri.*** Mimi ninakwambia bwana, hakuna kitu kinachonifurahisha kama kumwona mwenzangu kapata. Nikimwona Mwafrika vile ***ana gari hapa na kule*** ana ***nyumba*** hivi moja ehe…siyo'na maana ya kibanda. Hapana. Nikisema nyumba, ni nyumba hasa. Nyumba ya kiungwana- ***mabustani***, mazuri hivi…namna hii. Ah, moja. Maana wakati huu bwana, ni wakati wa kuendelea. Siyo kubakibaki nyuma. ***Nataka tuwaone Waafrika wana ndege, meli zao wenyewe, mashamba makubwa…mamna hii…mimi ninakwambia, we ngoja tu. Mimi! Hapana, mimi sifi maskini***… (*Mashetani*, Uk 43-44)

Kijana 3: ***Tatizo jingine ni la uchafu. Uchafu wa roho zetu zinazotofautisha baina ya makundi ya wachache na wengi.*** Wachache wanaoipakata na kufurahia nchi kwa sababu inawafaa kwa mapato na maslahi yao. Wengi wanaitemea mate na kuichukia nchi yetu kwa sababu haiwafai kwa ukosefu wa mapato. ***Pande zote mbili zinataja ovyo neno la 'ufisadi' lakini hakuna anayechukua hatua kali***… (*Mashetani Wamerudi*, Uk 35)

Data ya utafiti imebainisha kuwa tangu tamthilia ya *Mashetani* ilipotungwa na wakati ambapo tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ilipochapishwa suala la ufisadi limekuwa kero kubwa katika bara la Afrika. Said Mohamed ameendeleza suala la ufisadi katika kazi yake kwa kuonyesha kuwa hakuna mabadiliko ambayo yameshuhudiwa katika kukomesha ufisadi. Katika tamthilia ya *Mashetani*, wateja waliokuwa wakingoja vinywaji na vyakula walivyoagiza, wanawakilisha haja za watu waliojawa na ubinafsi wakati ambapo mapinduzi ya uhuru yanapaswa kuleta usawa katika jamii. Hawa wateja ni ishara kwamba mienendo ya ukoloni mamboleo imetawala fikra zao kupitia kauli zao **"*huu sasa ni wakati wetu*"** hii ina maana kwamba wakati wa wanajamii wengine umepita au wakati wao haujafika. Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* anaonyesha kwamba ubadhilifu wa mali ya umma umekita mizizi miongoni mwa wafanyikazi wa serikali. Viongozi hawa wanapora pesa ili kujifaidi wenyewe kwa kununua meli, mashamba, ndege na magari ya bei ghali. Kazi za fasihi zinaweza kulinganishwa na kazi zingine za kipindi fulani cha historia. Katika kila kipindi cha kihistoria huwa na kazi ambazo huwa na masuala yanayoibuliwa na kuendelezwa katika kazi za baadaye kulingana na mahitaji ya jamii (Mningo, 2015).

Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi*, anaeleza kuwa watu wamebadilisha mbinu, anaonyesha kuwa jambo jingine linalomkera ni uchafu wa miongoni mwa wanajamii. Mtunzi kupitia mhusika Kijana 3 katika kifungu hapo juu anafafanua jinsi Wafrika wamegawanyika katika makundi mawili kwa sababu ya uchafu wa roho. Uchafu unaorejelewa hapa ni ufisadi ambao umeleta mgawanyiko huu. Hii ndio sababu watu wanabaguana kwa misingi ya kitabaka, tabaka la walio wengi na wachache. Inadhihirika kuwa viongozi hawafanyi chochote kubadilisha hali hii. Kutokana na vifungu vilivyorejelewa katika tamthilia hizi, ni wazi kwamba wananchi wanafahamu tatizo kubwa katika mataifa yao ni ufisadi ambao umekidhiri katika taasisi na sekta mbalimbali za serikali. Wananchi wanaelewa kuwa uongozi katika nchi zao ni mbaya na wanaweza kuwaondoa mamlakani.

Data ya utafiti huu ilidhihirisha kuwa ufisadi huokea kutokana na haja ya wanajamii kuwa wabinafsi bila kujali masilahi ya wanajamii wengine. Kwa hivyo, ufisadi unaleta dhana ya mvutano kutokana jinsi waandishi walivyokuza mgogoro huu. Matini ya fasihi inaweza kujihusisha na kazi nyingine kutokana na jinsi mwandishi alivyorejelea,

kunukuu, kuiga ua kuendeleza matukio au masuala mahususi katika matini yake (Kristeva, 1981). Ili kusuruhisha baadhi ya migogoro inayojitokeza katika jamii kama vile ufisadi, waandishi wa kazi za fasihi hurejelea matukio yaliyowahi kutendeka katika jamii zao kwa njia inayoashiria ukaribiano wa aina fulani suala ambalo huibua dhana ya mwingilianomatini (Kehinde, 2003). Dhana ya mwendelezo wa kimatini katika kazi teule imejitokeza kwa sababu maudhui ya ufisadi yaliegemea urejelezi wa wahusika wanaoshabiana katika tamthilia teule.

### 4.2 Hitimisho

Sura hii ilichunguza mwendelezo wa kimaudhui na kuonyesha jinsi masuala makuu yalivyoendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* yalifanikisha ujenzi wa dhamira. Data ya utafiti katika sura hii ilidhihirisha kuwa Said Mohamed ameendeleza kazi ya mtangulizi wake kutokana na jinsi amekuza na kuendeleza dhana ya maudhui katika kazi yake. Katika ujenzi wa masuala hayo, maudhui ya ukoloni mamboleo yamejirudiarudia na kuendelezwa katika tamathilia ya *Mashetani Wamerudi*. Uchanganuzi wa data vilevile umethibitisha kuwa ufisadi, elimu ya kibwege na utabaka ni baadhi ya masuala makuu ambayo Said Mohamed aliendeleza katika kazi yake. Kazi teule zilibainisha haya na hivyo kuonyesha kuwa kazi za fasihi huiga na kuendeleza mawazo yake kutoka matini moja hadi nyingine na kusababisha mwanda wa kimwingilianomatini. Haya ni baadhi ya masuala ambayo yalionyesha kuwa waandishi wa kazi za fasihi wamebuni mbinu mpya katika utunzi wa kazi za fasihi ambayo ni mwendelezo wa kazi za awali. Kwa hivyo, mwingilianomatini hutilia mkazo kuwa kazi za fasihi zinaweza kujihusisha na matini nyingine.

# SURA YA TANO

# ATHARI ZA MTINDO KATIKA TAMTHILIA TEULE ZA KISWAHILI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inatoa tathmini ya dhana ya athari za mtindo katika tamthilia ya Kiswahili. Data katika sehemu hii imejikita katika madhumuni ya pili ya utafiti. Sura hii ilitathmini athari za mtindo katika tamthilia ya *Mashetani* kwenye *Mashetani Wamerudi*. Data ya utafiti huu ilionyesha kuwa kuna athari za mtindo zinazotokana na urejelezi wa kazi tangulizi kama inavyobainika katika kazi ya Said Mohamed. Baadhi ya athari zilizofichuka ni kuwa mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameiga na kurejelea baadhi ya vipengele vya kiutunzi ya mtangulizi wake. Mtindo wa urejelezi wa matukio na ujenzi wa wahusika umekuzwa na kuendelezwa katika tamthilia teule. Data ya utafiti huu ilichangua athari hizi kwa kina.

## 5.1 Dhana ya Mtindo

Mtindo ni ujuzi au ufundi wa kujieleza katika matini ya fasihi kwa kutumia vipengele mbalimbali vya lugha kama vile: taswira, tamathali za usemi, usawiri wahusika, uteuzi msamiati, mpangilio wa matukio na mandhari Njogu na Chimerah (1999). Katika fasihi, mtindo ni utaratibu unaotumiwa kumwezesha mwandishi kuwasilisha maudhui kwa kutumia na dhamira. Mtindo wa uandishi hutofautisha mwandishi mmoja na mwingine kutokana na jinsi alivyotumia vipengele vya lugha kujieleza. Utafiti huu uliongozwa na ufafanuzi wa Senkoro (1982) unaokidhi mahitaji ya utafiti huu kuwa mtindo katika matini ya fasihi ni upangaji wa maudhui na fani katika matini ya fasihi. Kuna aina mbili za mtindo kulingana Senkoro (Keshatajwa) kuna mtindo unaojitokeza kupitia jinsi mwandishi alivyoeleza fani na maudhui na pili kuna mtindo unadhihirika wakati mwandishi ametumia lugha ya ushairi katika tamthilia, riwaya, mtindo wa hotuba, na mtindo wa uandishi wa habari na mtindo wa kidhahania.

Coyle na wengine (1990) wanaeleza kuwa kila kazi ya fasihi hutoa maana yake katika kazi nyingine zilizotangulia, sio lazima iwe kazi ya awali, bali inaweza kuwa inatokana na matini zingine zinazotokana na kazi ambazo mwandishi alidurusu kabla ya kuandika kazi yake. Waitifaki wa nadharia ya mwingilianomatini wanaeleza kuwa kiwango kikuu cha marejeleo kati ya kazi moja na nyingine ni urejelezi wa mtindo wa kiutunzi baina ya mwandishi mmoja na mwingine ama matini zingine zilizoambatana na mtindo

wa matini inayoundwa (Wamitila, 2002). Mwingilianomatini katika utunzi wa kazi ya fasihi huonyesha jinsi mwandishi alivyoathiriwa kimtindo kutokana na jinsi alivyokuza maudhui na wahusika katika kazi yake. Utafiti huu unahusisha tamthilia mbili ili kuonyesha mwendelezo wa athari za kimtindo baina ya tamthilia zilizoteuliwa.

### 5.1.1 Matumizi ya Usimulizi

Eagleton (1983), akiangazia suala la mwingilianomatini anaeleza kuwa matini fulani ya fasihi inaweza kufanana na kuhusiana na nyingine kimtindo katika ujenzi wa dhamira. Analeza kuwa si ajabu kazi mbili za waandishi tofauti kuathiriana kimtindo hasa katika urejelezi wa matukio sawa yanayoendelezwa na wahusika kuwa na ukaribiano. Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa mtindo wa usimulizi wa matukio katika tamthilia ya *Mashetani* umeendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi.* Said Mohamed ametumia mtindo wa kiusimulizi ulitumika na Ebrahim kuonyesha mgogoro uliokuwepa baina ya familia ya Kitaru na Juma.

Maelezo haya ni muhimu kwa sababu data ya utafiti ilionyesha kuwa kuna athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Kazi ya Said Mohamed imeathiriwa na tamthilia ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein kutokana na jinsi alivyokumbatia mtindo wa usimulizi katika kazi yake. Mtindo wa kiutunzi baina ya watunzi hawa umetumiwa ili kuleta mvuto na kuteka akili za wasomaji kama inavyodhihirika katika vielelezo vifuatavyo. Tazama:

| | |
|---|---|
| JUMA: | Wananchi kwa mara nyingine chini ya mbuyu huu mimi Juma, na rafiki ya Kitaru, tutakuonyesheni mchezo wa Shetani na Binadamu. Mimi nitakuwa Shetani, na Kitaru, atakuwa Binadamu (*Mashetani*, Uk 1). |
| Sauti ya Mtu: | **Hapa na pale. Hapa uwanjani panapo kiti cha siasa. Tumesimama katika kitovu cha kisasa… Mnasemaje hadhira?... Si mnajua majumba makubwa ya kifahari yanayojengwa na mtu mmoja? Majumba ya kiasi cha sabini na tatu. Majumba makubwa aliyoyajenga mtu mmoja.** Kisha tazameni kibanda kile kidogo. Kimesimama tisti. Ndani atatoka mtetezi. Atakuja Profesa Hafi-Leo-Wala-Kesho mtetezi. Pole pole ataingia uwanjani-uwanja wa utandawazi. Katikati ya uwanja, karibu na kibanda, lipo shina la mbuyu. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 2) |

Mwandishi wa *Mashetani* ametumia usimulizi ili kuonyesha taswira ilivyokuwa katika mataifa mengi ya Kiafrika baada ya kujinyakulia uhuru. Ameonyesha mgawanyiko wa kitabaka uliokuwa kabla na baada ya mapinduzi. Mwandishi anaonyesha mkondo ambao mataifa mengi ya kiafrika yalichukua baada ya kupata uhuru. Kwa mtazamo wa Hussein, Bindamu na Shetani wanawakilisha jamii ya viongozi waliochukua nafasi za uongozi baada ya mapinduzi. Baadhi ya viongozi walitumiwa kama vibaraka wa Shetani kuendeleza uongozi wa kishetani (kikoloni).

Said Mohamed katika tamthilia yake ya *Mashetani Wamerudi* ameiga mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake Ebrahim Hussein kuonyesha mgawanyiko wa kitabaka katika jamii ya Kiafrika. Katika utangulizi wa tamthilia yake, Said Mohamed anaonyesha mwendelezo wa kimtindo kutokana na jinsi alivyotanguliza mgogoro wa kiuchumi katika kazi yake. Kwa mfano;… *Hapa na pale. Hapa uwanjani panapo kiti cha siasa. Tumesimama katika kitovu cha kisasa… Mnasemaje hadhira..? Si mnajua majumba makubwa ya kifahari yanayojengwa na mtu mmoja?...Majumba kiasi ya sabini cha sabini na tatu..”* (Katika *Mashetani Wamerudi*, Uk, 2). Mtindo huu wa kutanguliza matukio yatakayojiri katika jukwaa pia umetumika katika tamthilia ya *Mashetani.* Mwandishi anaonyesha mgawanyiko wa kisiasa, kielimu na kiuchumi katika bara la Afrika baada ya kumezwa na wimbi la utandawazi. Katika muktadha huu mwandishi ametumia dhana ya "utandawazi" ili kuonyesha mbinu ambayo Shetani ametumia ili kumghilibu Mwafrika nafasi yake ya kujiongoza. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anaiga mtindo wa mtangulizi wake Ebrahim Hussein katika kueleza hadhira matukio yatakayojiri jukwani. Katika matini za fasihi, maana ya kazi haipatikani katika kazi yenyewe, bali inajengwa katika mseto wa matini nyingine (Kehinde, 2003). Kwa hivyo mtunzi wa matini ya fasihi huwa ni kikamilisho cha matini ya awali.

### 5.1.2 Matumizi ya Majigambo

Utafiti huu umegundua kwamba Ebrahim Hussein na Said Mohamed wametumia majigambo kama kipengele cha fasihi simulizi katika tungo zao. Kwa mujibu wa Mulokozi (1996) majigambo ni mtindo wa kiutunzi unaotumiwa kama njia ya kujisifu au kujinaki kwa mtu kuhusu matendo au mambo ya kishujaa aliyowahi kufanya katika jamii. Kwa mujibu wa Abram (1981) mwingilianomatini ni mbinu inayotumiwa katika

utunzi wa matini za fasihi kudhihirisha mwangwi wa kazi ya fasihi na nyingine. Mwangwi katika fasihi unaweza kudhihirika kutokana na jinsi mwandishi ameathiriwa na msimbo ya kiutunzi unaofanana katika uwasilishaji wa maudhui na dhamira katika kazi yake. Hali hii ilidhihirika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ambapo Said Mohamed ameathiriwa na utanzu wa majigambo katika utanzu wa kazi yake. Kipera hiki kimejitokeza katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Utafiti huu umethibitisha haya kupitia dondoo hili katika *Mashetani*. Ebrahim Hussein ametumia mbinu ya majigambo kuonyesha jinsi Shetani anajigamba kupitia kielelezo hiki:

SHETANI: Unajua mimi nani?
Mimi Shetani.
Siyo jini wala kuhani
Uwezo wangu hauhifadhiki
Wema wangu hauhisabiki
Ubaya wangu hausemeki
Ninajenga
Ninabomoa
Ninatukuza
Ninadhalisha nitakavyo
Mimi nina nguvu na nguvu ni mimi
Mimi nina uwezo na uwezo ni mimi

Shetani anawakilisha viongozi wa kiafrika walioendeleza ukoloni mamboleo katika mataifa yao. vilevile, neno *Shetani* limetumiwa na mwandishi ni kikale katika fasihi simulizi. Shetani ametumika kama istiari kuonyesha majigambo ya mwafrika baada ya kujinyakulia uhuru. Kulingana na mwandishi ukoloni mkongwe umerudi na bara la Afrika linatawaliwa na shetani kupitia viongozi walichukua hatamu za uongozi. Hapa Shetani anajitapa kuwa yeye ana uwezo mkubwa wa kubomoa na kujenga.

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, utanzu wa majigambo umetumika kuonyesha historia iliyomzingira mwafrika baada ya kupata uhuru. Mwandishi anaonyesha kwamba ukoloni mamboleo upo katika kipindi cha sasa. Said Mohamed anarejelea ukoloni mamboleo kama utandawazi. Mtunzi anaonyesha jigambo hili kupitia mhusika Shetani kuonyesha jinsi Afrika inatawaliwa na nchi za kimagharibi. Kielelezo hiki ni majigambo ya shetani kuhusu bara la Afrika:

Sheta: Hapana nguvu yoyote ya kudhibiti, maana sisi tuko nchini mwetu tunabonyeza *remote control*. Kwani mmesahau kwamba utandawazi ndio *remote control* zaidi kuliko ukoloni mamboleo (*Mashetani Wamerudi*, Uk 61)

Allen (2000), anaeleza kuwa kazi za fasihi huathiriana na kuingiliana kupitia mtindo wa kiutunzi. Mwandishi wa kazi ya fasihi anaweza akarejelea na kuchota mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake. Matini ya awali huweka misingi kama kanuni kwa kazi za baadaye. Data imedhihirisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amerejelea na kuendeleza mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake Ebrahim Hussein kutokana na jinsi alivyotumia utanzu wa maigizo katika tamthilia yake. Utanzu wa maigizo umetumiwa kitaswira na Hussein katika *Mashetani* na kisha mtindo huo wa kiutunzi ukaendelezwa na Said Mohamed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Waandishi hawa wanarejeleana kimwingilianomatini kupitia wahusika Prof na Kijana kama inavyodhihirika kupitia vielelezo hivi:

| | |
|---|---|
| Kijana 1: | Pana Mashetani hapa? |
| Prof: | Ndiyo. Walikuwepo.Wakajifanya hawapo kwa ujanja wao. Sasa wapo waziwazi. Wamesharudi.. |
| Kijana 1: | Mashetani? Mashetani gani hao? |
| Prof: | Wale wale waliotuchezea mchezo wa maneno na dansi wa ***waltz*** huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao. Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wakweli. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 7) |
| BINADAMU: | Maombi yako yamekubaliwa. Sherehe itafanywa. |
| SHETANI: | Na vipi tutaisherekea? |
| BINADAMU: | Kwa **waltz** (*Mashetani*, Uk 7-8) |

Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anaonyesha kwamba baada ya kumwondoa mkoloni uongozini wakidhani kwamba ameondoka ni ishara kwamba mkoloni alibuni mbinu mpya ya kuendeleza utawala wake Afrika ndio maana Prof anasema …"*Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wakweli"* Said Mohamed na Ebrahim Hussein wanaingilina na kurejeleana kwa maneno *mchezo* na *waltz* katika kazi zao kuonyesha hali ilivyo katika mataifa mengi ya Kiafrika ambapo mkoloni amekita mizizi katika mataifa mengi ya Afrika. Kwa hivyo, uingiliano katika urejelezi wa sherehe za Waltz au mchezo zimetumiwa na watunzi kitaswira kuonyesha jinsi mkoloni alivyoingia katika maitaifa ya Kiafrika kwa njia inayoathiri idara mbalimbali kama vile: elimu, siasa na uchumi. Watunzi hawa wanaingiliana kupitia utanzu wa maigizo kuonyesha matatizo yanayokumba Afrika anayewakilishwa na mhusika BINADAMU kupitia mchezo wa *waltz*. Kwa hivyo, matini hizi zinaingiliana na kukamilishana kuonyesha kwamba tangu *Mashetani* (1971) ilipotungwa na wakati *Mashetani Wamerudi* (2016) ilipochapishwa na Said Mohamed zinaonyesha Afrika inaendelea

kuthibitiwa kupitia ukuloni mamboleo kwa sababu umedhihirisha kupitia vipindi vyote vya uhuru

### 5.1.3 Matumizi ya Taswira

Data ya utafiti huu imethibitisha kuwa katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*, waandishi wa matini hizi wametumia mtindo wa kiutunzi unaofanana kutokana na jinsi walivyotumia taswira katika matini zao. Taswira katika tamthilia hizi mbili imetumiwa kuonyesha mfanano uliopo baina ya watunzi hawa wawili. Wamitila (2002) anaeleza taswira kama picha inayomjia mwandishi au msomaji akilini anaposoma matini fulani ya kifasihi. Anafafanua kwamba kuna aina mbili za taswira: ambapo kuna taswira za kimaelezo na taswira za uashiriaji. Utafiti huu umebainisha kuwa mwandishi wa matini huwa ameathiriwa na usomaji wa kazi za awali. Mwandishi anaweza akaiga na kuathiriwa kimtindo wakati anabuni kazi yake (Zengin, 2019). Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa na usomaji wa tamthilia ya *Mashetani* ya Ebrahim Hussein. Utafiti huu umetambua kuwa mwendelezo wa kimtindo unasikika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kutokana na jinsi taswira imetumika katika ukuzaji wa maudhui katika kazi teule.

Said Mohamed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, ameiga mtangulizi wake kutokana na jinsi amesawiri elimu katika bara la Afrika. Kwa mtazamo wake, elimu inayopeanwa katika mataifa mengi ya Kiafrika haikidhithi mahitaji ya jamii husika. Anaonyesha kwamba matatizo yanayokumba Afrika yanatokana na elimu duni anayopewa Mwafrika ili kujiendeleza kiuchumi, kisiasa na kielimu. Mwandishi anaonyesha taswira ya elimu kupitia vielelezo hivi. Tazama:

> Mzee Kitarua: **Mpaka sasa hatuwezi hata kutengeneza sindano**! Iko wapo elimu ya matakwa yetu? Iwapi elimu ya falsafa yetu? Kwa nini tunaendelea na mafunzo yanayotoka mbali pasipo karibu yetu? (*Mashetani Wamerudi*, Uk 43)
>
> Kijana 2: Pili uchumi wetu umesakama hauendi mbele, ila kurudi nyuma. Tatu, **hakuna ubunifu wa kuanzisha viwanda vya kutosha.** Tena hakuna mwongozo wala msisitizo wa serikali kuendeleza ajira za sekta ya biashara za makampuni au za watu binafsi. Ikiwa hakuna mipango ya kuendelea ya aina hii, basi ni kama inaelekea usoni mwetu (*Mashetani Wamerudi*, Uk 57)

Katika vielelzo vilivyorejelewa hapo juu, Said Mohamed hajaridhishwa na mfumo wa elimu katika mataifa ya Kiafrika. Anaeleza kuwa hakuna maendeleo ambayo mwafrika anaweza kujivunia kwa sababu elimu anayopokea imeandaliwa na mkoloni. Kulingana na mwandishi, ubunifu haujashuhudiwa kwa sababu elimu tuliyonayo inakidhi mahitaji ya mkoloni. Mtaala wa elimu ya kikoloni unaotumika hadi sasa na mfumo unaoendeleza mfumo wa kibepari unaoathiri taasisi mbalimbali za elimu. Katika mfumo huu, mataifa changa ya Kiafrika yanaendelea kutawaliwa na kuthibitiwa na mkoloni. Inabainika kwamba, uhuru anaojivunia mwafrika ni wa bendera, hana cha kujivunia kutokana na mfumo wa elimu ndio maana asasi za kiuchumi kama vile viwanda havijaanzishwa hadi sasa kutokana na maneno ya mhusika Kijana 2 anasema…*hakuna ubunifu wa kuanzisha viwanda vya kutosha…"*

Data ya utafiti huu imebanisha kuwa tangu Ebrahim Hussein alipotunga tamthilia ya *Mashetani* (1971) hadi wakati wa sasa wa *Mashetani Wamerudi* hakuna hatua ambazo zimechukuliwa kurekebisha mtaala wa elimu unaotumiwa katika bara la Afrika. Elimu inayotolewa ni ya vitabuni tu. Mwandishi wa *Mashetani* anairejelea kama elimu ya kibwege kupitia ndodoo lifuatalo:

> JUMA: Sasa unaniambia nini. Hujaniambia kitu. Kweli inauma bwana. Ukweli…acha yote hayo. Ukweli bwana, ***degree inakupa tonge ya wali na mchuzi, tena mchuzi wa kuku***, badala ya tonge ya ugali na maharagwe.
>
> KITARU: Acha maneno yako. Maneno ya kishetani (*Mashetani*, Uk17)

> Kijana 4: …Kwanza ni elimu tuliyonayo nchini mwetu**.** ***Elimu hii tulirithi kutoka kwa wakoloni***. Bila shaka wakoloni hawakuwa na nia ya kutuelimisha sisi kwa ajili ya kupiga hatua na kwenda mbele katika nchi na maisha yetu. ***Elimu tuliyonayo sasa ni elimu iliyotandazwa kwa wingi wa nadharia kuliko vitendo*** vinavyotumiwa kujenga na kutengeneza vifaa na mashine. Ingawa vyuo vikuu vyetu vinafundisha somo la uhandisi bado hatujaunganisha vitendo vinavyoweza kutupa mapato kwa kutumia mashine na vifaa mbalimbali…" (*Mashetani Wamerudi*, Uk 58-59)

Vielelezo vilivyorejelewa vinadhihirisha uhusiano wa kimatini hivi kwamba vinarejeleana kutokana na jinsi elimu imesawiriwa na watunzi hawa. Kazi za fasihi huwa na sifa ya kimwingilianomatini kwa sababu mwandishi anaweza akaathiriwa na baadhi ya vipengele vya kiutunzi kutoka kwa kazi tangulizi (Walleck na wengine, 1988). Data ya utafiti huu imethibitisha kuwa Said Mohamed alikuwa amedurusu

tamthilia ya *Mashetani* kutokana na jinsi alivyotumia taswira kusawiri elimu inayopatikana katika bara la Afrika. Taswira inayojitokeza hapa ni athari za elimu ya kigeni katika mataifa ya Kiafrika. Said Mohamed anatumia taswira ya "*elimu iliyotandazwa wingi wa nadharia…'* kuonyesha jinsi mataifa ya kigeni yamethibiti nchi za kiafrika kielimu kwa namna inayosawiriwa na watunzi hawa wawili. Mwandishi anaonyesha madhara ya elimu ya kigeni ambayo imejaa nadharia tu. Kulingana Said Mohamed, ukoloni mamboleo unajitokeza kupitia asasi za kielimu. Mwandishi analalamika kwamba, hukuna hatua muhimu zimechukuliwa kubadilisha hali hii.

### 5.1.4 Matumizi ya Mtindo wa Kishairi

Matini ya awali inapojipata katika kazi ya sasa, sehemu ya awali ya matini hiyo inaweza kuathiri matini ya sasa kimtindo na kuwa wigo wa matini ya awali (Bakhtin, 1981). Ingawa maelezo ya Bakhtin yanaonekana kuwa ya zamani, anaeleza kuwa kazi ya fasihi ni uwanja ambao una mwingiliano wa kazi mbalimbali. Uwanja unaorejelewa hapa ni mtindo unaotumika katika utunzi wa matini zinakazokuja baadaye. Haya yanatokana na hali kuwa matini za fasihi huwa kwa namna fulani zimeandikwa tena waandishi ambao mara nyingi hawatambui kwamba kazi zao zinaathiriana kimtindo na kazi za awali (Wamitila, 2003). Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameendeleza kazi ya mtangulizi wake kutokana na jinsi ametumia utanzu wa ushairi katika kazi yake. Data ya utafiti huu imebainisha kuwa ushairi umetumika na mwandishi kama kunga za kiutunzi kuendeleza maudhui katika kazi teule.

Mtindo wa kiutunzi wa tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* unarejeleana kwa kiasi kikubwa. Japo mtindo wa kiutunzi baina ya watunzi hawa sio wa moja kwa moja bali kuna mwendelezo wa mbinu za kiutunzi kutokana na jinsi ametumia kipera cha ushairi kuwasilisha maudhui. Utafiti huu umebaini kuwa Said Mohamed anatumia mtindo wa kishairi uliotumiwa na mtangulizi wake Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Katika kuthibitisha ukweli huu, vielelezo vya ushairi vimerejelewa kama ifuatavyo:

> Mwanambele (Anaingia Mwanamke uwanjani. Kisha sauti inasikika ikifutatwa na wimbo wa ngoma)
>
> Jambo lile la kiho***ro***,
> Lile jambo la kiho***ro***,

Jambo lile la kiwe***we***,
Tena jambo la kiwe***we***,
Jamo lile la kidon***da***
Tena homa ya kidon***da***
Aaa,'ukoloni' ni kiho***ro***,
Ukoloni ni kiwewe na kiho***ro***
Ukoloni homa ya kidon***da***!
Homa ya kidonda ukolo***ni***!
Hasa sasa ukoloni mambol***eo***,
Umepewa jina jip***ya***,
Linaloitwa Utandawa***zi***! (*Mashetani Wamerudi*, Uk 10)

SHETANI: Unajua mimi na***ni***?
Mimi Sheta***ni***.
Siyo jini wala kuha***ni***.
Mimi Sheta***ni***
Uwezo wangu hauhifadhi***ki***
Wema wangu hauhisabi***ki***
Ubaya wangu hauseme***ki***
Ninajen***ga***.
Ninabom***oa***
Ninatuku***za***
Ninadhalilisha nitakav***yo***
Mimi ni nguvu na nguvu ni mi***mi***
Mimi ni uwezo na uwezo ni mi***mi*** (*Mashetani*, Uk 1-2)

Katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* utanzu wa ushairi umejitokeza kama nyenzo ya kupitisha maudhui. Katika matini hizi ushairi umetumika kudhihirisha jinsi ukoloni mamboleo umekidhiri katika jamii. Aidha, watunzi hawa wanaonyesha msimamao wao jinsi mwafrika ni adui katika jamii yake katika kuendeleza uongozi wa Kishetani kama vibaraka. Mwandishi wa *Mashetani* anaonyesha uwezo aliyo nayo shetani katika kuthibiti matukio yanayojiri katika bara la Afrika hata baada ya mapinduzi. Said Mohamed anaeleza kuwa, ijapokuwa shetani aliondoka ukoloni bado ni donda ndugu katika mataifa mengi ya Kiafrika. Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ametumia utanzu wa ushairi kulinganisha ukoloni mamboleo na kidonda. Kwa hivyo, shetani amebuni mbinu mpya ambayo ni utandawazi ili kuendeleza uthibiti wa jamii ya Kiafrika. Kazi ya fasihi huwa na muktadha wa matukio ambayo huwa yanarejeleana kiutamaduni kutokana matukio ambayo mwandishi anawasilishia hadhira yake (Kehinde, 2003). Kwa hivyo, utafiti huu umegundua kuwa Said Mohamed ameendeleza mtindo wa kiutunzi kutokana na jinsi alivyosawiri na kurejelea mhusika shetani katika kazi yake kwa njia inayoingiliana na matini ya awali.

Wamitila (2010), anaeleza kuwa Ebrahim Hussein katika utunzi wake amezingatia mtindo wa kikale cha ushairi huru katika tamthilia za *Mashetani* (1971), *Jogoo Kijijini* (1976) na *Ngao ya Jadi* (1976). Ili kuthibitisha hili Ebrahim Hussein amekumbatia mtindo wa kikale katika utunzi wa ushairi huru. Utafiti huu umebaini kwamba mwandishi hakuzingatia arudhi katika utunzi wake kama inavyodhihirika katika wanamapokeo. Kifungu hiki cha ushairi ni ithibati kwamba Ebrahim Hussein ametumia ushairi huru katika utunzi wa tamthilia ya ushairi. Dondoo hili lina vina vya mwisho japokuwa halina mizani wala beti lakini halina tofauti na umbo la shairi huru. Vina vinavyojitokeza katika shairi hili lina vina: *ni, ni ni,ni, ki,ki,ki* na *a,a,a*. Kupitia vifungu hivi ni kuwa Ebrahim Hussein katika tamthilia ya *Mashetani* amezingatia muundo wa ushairi huru. Katika tamthlia ya *Mashetani Wamerudi* Said Mohamed, amezingatia mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake Ebrahim Hussein. Mtindo huu wa kiutunzi katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* unaibua dhana ya mwendelezo katika kazi za fasihi kutokana na jinsi Said Mohamed ametumia mtindo huu katika tamthilia yake.

Utafiti huu umeonyesha dhana ya mwendelezo katika vielelezo vya ushairi ili kuthibitisha ukweli wa madai haya kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, vina vya mwisho vilivyojitokeza ni: *ro, ro,ro,ki,ki,ki, a,a,a* na *da,da.* Utafiti huu umebaini kwamba, japo vina katika shairi la Said Mohamed havifanani moja kwa moja lakini data ya utafiti imedhihirisha kwamba mtindo wa kiutunzi katika vifungu vilivyorejelewa ni mwendelezo wa mbinu za kiutunzi watunzi kwa sababu wametumia mtindo wa ushairi huru unaofanana katika utunzi wao. Matini yoyote ile huwa na maana kwa sababu baadhi ya vipengele vya kiutunzi vinahusiana na matini hiyo vimetumiwa katika uandishi wa kazi zilizotangulia Wamitila (2002). Kwa hivyo, upekee wa mtindo wa uandishi katika kazi nyingine unategemea matini iliyokwisha kuandikwa.

### 5.1.5 Matumizi ya Nyimbo

Kazi za fasihi huwa zinawasiliana kutokana na utanzu ambao mwandishi anatungia. Mawasiliano baina ya mwandishi huambatana na athari zilizopo baina ya mtindo wa kiutunzi na namna mwandishi ametumia lugha katika kazi ya awali (Nwagbara, 2011). Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kuwa Ebrahim Hussein (1971) na Said Mohamed (2016) wamerejeleana kutokana na matumizi ya mtindo unaofanana hasa jinsi walivyotumia nyimbo ili kufanikisha ujumbe wao. Utafiti huu umedhibitisha kuwa

kuna mwingilianomatini katika kiwango cha nyimbo. Kwa hivyo, mtafiti amebainisha kuwa utanzu wa nyimbo umejitokeza katika tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Kwa upande wa mwandishi wa *Mashetani* ametumia wimbo kuonyesha taswira kuhusu utawala wa jamii ya Kiafrika baada ya mapinduzi kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki cha wimbo kama ifuatavyo:

(*Anapiga vigelegele vya furaha. Anarukaruka na kuizunguka maiti kwa furaha kubwa. Anacheka mpaka michozi inamtoka. Anacheka mpaka furaha na kicheko vinamlevya. Anauendea ule mbuyu kwa haraka na huku anacheka. Anaimba.)*

Wako wapi walio wakijitapa?
Sasa twawataka.
Wako wapi walio wakijitapa
Sasa twawataka.
Tumekwisha (anacheka) wakamata
Wakamata.
Tumekwisha wabwatabwata
Wako wapi waliokuwa juu jana?
Sasa twawataka.
Wako wapi waliokuwa juu jana?
Sasa twawataka.
Tumekwisha waangusha
Waangusha.
Tumekwisha wasasaga
Tumekwisha wakamata
Wakamata.
Tumekwisha wabwatabwata
Tumekwisha waangusha
Waangusha.
Tumekwisha wasagasaga (*Mashetani*, Uk 9-10)

Mwandishi ametumia kielelezo hiki kuonyesha awamu ya tatu baada ya kupata uhuru. Huu wimbo wa Binadamu ni kejeli kwa wazungu. Mwandishi anaonyesha taswira kuhusu kiburi cha Binadamu ambaye anawakilisha viongozi walichukua hatamu za uongozi baada ya mapinduzi. Wimbo huu unaonyesha kujitapa kwa Waafrika waliowakejeli wazungu. Kulingana na Wafrika huu ndio wakati wao kula na kutawala. Binadamu anataja baadhi ya mambo ambayo amekamilisha kutokana na uhuru wake alionyakua kutoka kwa mkoloni.

Mwandishi anadhihirisha kuwa baada ya mapinduzi, mataifa mengi ya Kiafrika yaliongozwa na viongozi waliojawa na tamaa ya mali na unafiki wa mkoloni. Walianza

kuwadhulumu wanajamii wenzao kama anavyosema Binadamu…wako wapi waliokuwa juu jana? Kulingana na kauli wa mwandishi “jana” inawakilisha jamii ya kina Kitaru ilikuwa juu kabla ya mapinduzi. Mwandishi wa *Mashetani* anatumia huu wimbo kuonyesha jinsi jamii ilivyogawanyika katika matabaka. Kwa hivyo, tamthilia ya *Mashetani* inapatikana wakati ambapo jamii ya Kiafrika imegawanyika.

Katika tamthlia ya *Mashetani Wamerudi* Said Mohamed ameendeleza mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kutokana na jinsi alivyotumia kipengele cha wimbo kuwasilisha maudhui yake. Mtindo wa kiutunzi wa Said Mohamed ni mwendelezo hivi kwamba ametumia wimbo kuwazindua wanajamii kuonyesha haja ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi, kisiasa na kielimu katika kazi yake. Mwandishi anaonyesha taswira kuhusu viongozi walipigania mapinduzi katika bara la Afrika na mataifa mengine duniani. Anawarejelea wanaharakati hawa kama njia ya kuwazindua wafrika waliopoteza mwelekeo kuhusu mkondo ambao mataifa yao yalichukua baada ya mapinduzi.

Mwanambele*: (Anaingia na wimbo wa utetezi na ngoma ya utetezi wa sauti ya utetezi…)*
Decolonization…
Amkeni watetezi wa uhuru wa haki
Amkeni Waafrika, Amkeni Waasia
Amkeni Karebian,
Tatizo letu moja,
Amkeni Amerika ya Kusini,
Wawapi vijana wa Mahatma Ghandhi,
Wawapi vijana wa Patrice Lumumba,
Wawapi vijana wa Amilear Cabral,
Amkeni kusimama na Nationahood,
Amkeni kusimamia mataifa kamili,
Upeo wa nationalism,
Uzalendo ni upepo wa mwanzo na mwisho,
Upeo huu ni muhimu! (*Mashetani Wamerudi*, Uk 28)

Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ametumia uliotumika katika *Mashetani* kutambua juhudi za mashujaa wa kihistoria kwa kujitolea katika kutetea haki za Waafrika kutoka kwa wakoloni. Wimbo huu umetumika kuwakejeli viongozi wa kipindi cha sasa kinachoongozwa na tamaa ya mali na ubinafsi. Viongozi waliorejelewa katika wimbo huu ni viongozi waliopigania mapinduzi mapya katika mataifa yao. Viongozi hawa walihusika pakubwa kupigana na utawala wa mkoloni. Kwa hivyo, mwandishi

anatumia wimbo huu kuwazindua wanajamii kuungana pamoja ili kuleta mapinduzi mapya na kujikomboa.

### 5.1.6 Mtindo Katika Kiwango cha Wahusika

Kazi za fasihi huomba mawazo yake kutoka kwa matini nyingine. Matini mbili zinapotangusana huwa zinaathiriana na kuwa na sifa zinazofanana kama vile usawiri wahusika (Kristeva, 1969). Kristeva anadhihirisha kuwa usomaji wa matini fulani unaweza kudhihirika kupitia matini nyingine inayosemezana nayo. Kwa hivyo, waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuathiriana kutokana jinsi walivyokuza wahusika katika kazi zao. Wakati mwandishi anatunga kazi yake hujiingiza katika mwingiliano fulani hasa kwa kurejelea wahusika katika kazi alizowahi kusoma hapo awali (Cuddon, 2013). Utafiti huu ulichunguza athari za mtindo na kubainisha wahusika wa kimwingilianomatini baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Aidha, utafiti huu ulichunguza athari za kimtindo katika kiwango cha wahusika na kubainisha jinsi Said Mohamed ameiga na kuendeleza mbinu ya uhusika katika tamthilia yake.

Mwandishi wa matini ya fasihi anapotunga kazi yake huwa na lengo la kumsawiri mhusika katika kazi yake kwa namna fulani. Kuna uwezekano kuwa katika akilini mwake ana wasifu wa mhusika anayepatikana katika matini alizoduru hapo awali (Allen, 2002). Mhusika atakayesawiriwa katika kazi ya mwandishi atakuwa na wasifu unaofanana na mhusika aliyetangusana naye katika kazi za awali. Waandishi wa kazi za fasihi wanaweza kuathiriana kutokana na jinsi walivyosawiri na kuendeleza wahusika katika matini zao kwa njia inayoibua mfanano wa aina fulani.

Wahusika katika kazi ya fasihi wanaweza kumrejesha msomaji au mwandishi kwenye matini nyingine alizorejelea hapo awali. Hali hii ya urejeleaji wa wahusika katika fasihi huibua mwingilianomatini. Mwingilianomatini wa wahusika unaweza kujitokeza kwa njia mbalimbali kutokana na jinsi mwandishi anavyokuza na kuendeleza wahusika wake kupitia mazungumzo yao, mazingira yao, maudhui yanayoendelezwa. Mwandishi huwa na mbinu ambazo anaweza kutumia katika kusawiri wahusika. Anaweza kuwasilisha wahusika wake kwa njia dhahiri au isiyokuwa dhahiri. Mwandishi anaweza kutumia mbinu zifuatazo kusawiri wahusika katika matini yake.

### 5.1.6.1 Maelezo ya Wahusika Wengine

Msomaji au mwandishi wa kazi ya fasihi hastahii kujifunga katika matini moja pekee ila anafaa kurejelea kazi mbalimbali. Kazi za fasihi zinaweza kuathiriana kutoka na namna mwandishi amekuza wahusika wake (Bosibori, 2016). Mwandishi huwa na uhuru wa kutumia wahusika wa aina mbalimbali katika ujenzi wa maudhui na dhamira katika kazi yake. Data ya utafiti huu imebainisha kuwa kuna athari za kimtindo kutokana na jinsi mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amekuza na kuendeleza wahusika wanaopatikana katika tamthilia tangulizi ya *Mashetani*. Matokeo ya utafi huu yalibainisha kuwa Said Mohamed ametumia Kijana 1 kama mhusika bapa ambaye habadiliki. Utafiti umedhihirisha aina hii ya mhusika katika kazi teule.

Said Mohamed ametumia mtindo huu wa maelezo hutegemea kwa kiasi kikubwa maelezo ya wahusika wengine au maelezo ya mwandishi kuhusu wasifu wa mhusika anayetanguliza. Utafiti huu umebainisha kuwa Kijana 1 ametumiwa kumrejesha msomaji katika wahusika bapa waliotumiwa katika tamthilia ya awali ya *Mashetani* Ilibainika kuwa mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameathiriwa mtindo wa mtangulizi wake Ebrahim Hussein katika mtindo wa urejeleaji wa wahusika. Said Mohamed anatumia Kijana 1 katika kurejelea wahusika katika kazi ya Ebrahim Hussein kama inavyobainika katika vielelezo hivi:

Kijana 1: …alitumia falsafa au itikadi ya maji ya tohara. Mhusika Juma ndiye aliyeongoza tamthilia ya *Mashetani*. Akina Kitaru ndio waliokuwa wadhibiti wa serikali na nchi yetu na sisi tukaongozwa kama punguani au mabwege. Tulibaki kutazama ndoto ya kesho na keshokutwa. Lakini historia inazidi kutufumbua macho na kutuongoza. Hakuna mtu asiyefahamu isipokuwa mwendawazimu. Mwisho ***Juma*** na ***Kitaru*** walimalizia tamthilia yao kwa kuvutana na kuangushana chini kwa mzaha huku wanagombana kwa ukweli. Lakini haya ni ya jana. Kesho yetu itakuwa si kuvutana na kugombana na kuangushana chini. Kesho tutakuwa wamoja. Hatimaye Juma alitoa maneno ya busara- ***mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono…***' (*Mashetani Wamerudi*, Uk 62)

KITARU**:** Kwa nini?

JUMA**:** Sababu mojawapo

KITARU: Mojawapo?

JUMA: Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono (*Mashetani*, Uk 56)

Data ya utafiti imethibitisha kuwa mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* aliwarejelea wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* ili kuonyesha jinsi historia inavyoathiri matukio ya sasa. Said Mohamed alitumia mbinu ya kuegemea maelezo ya wahusika wengine ili kuonyesha uhusiano ulipo baina ya wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* ili kuonyesha uhusiano uliopo na matukio yanayojiri katika tamthilia yake na mkondo ambao historia ya ukoloni ilichukua. Alifanya hivi kuonyesha mgawanyiko wa kitabaka uliokuwa baina ya familia ya ***Kitaru*** na ***Juma*** ambao waligombana kuhusu mstakabali ambao familia zao zilichukua kabla na baada ya mapinduzi. Kuwepo kwa mfanano katika ukuzaji wa wahusika, tamthilia teule unadhihirisha athari za kiutunzi kutokana na jinsi wahusika bapa wametumika kukuza dhamira katika matini teule. Wahusika waliorejelewa katika kazi teule ni ithibati kwamba matini ya awali inaweza kuwa na athari za moja kwa moja kwa matini ya sasa na kuwa wigo unaoendelezwa katika urejelezi na usawiri wa wahusika katika kazi za baadaye (Allen, 2002)

#### 5.1.6.2 Mazungumzo au Matendo ya Wahusika wengine.

Utafiti huu ulibanisha kuwa kazi teule zimesheheni athari za kimtindo kwa sababu watunzi wa matini tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wametumia mbinu ya mazungumzo kuwasilisha wahusika duara. Mhusika wa aina hii hudhihirika kutokana na wahusika wakuu na husaidia katika kujenga dhamira ya mwandishi. Utafiti huu umebainisha kuwa Said Mohamed amendeleza mtindo wa uhusika kutoka kwa mtangulizi wake kutokana na jinsi ametumia wahusika dura katika kazi yake.

Katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wahusika wakuu katika tamthilia tangulizi wamekuzwa na kuendelezwa na Said Mohamed kupitia mbinu ya mazungumzo baina ya Kitarua na Jumai. Utafiti huu umebainisha kuwa wahusika waliorejelewa ni wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mashetani.* Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* wamerejelewa kama wahusika duara ili kuonyesha mabadiliko waliyopitia katika jamii ya sasa kama inavyodhirika katika kielelezo hiki:

> Mzee Jumai: Wewe nani? Naona kama nakujua. Naona kama nakukumbuka tokea zamani. Ninakutambua mimi!
> Mzee Kitarua: Mimi?... Mimi unanijua? Unanijua mimi?... Zamani.
> Mzee Jumai: Wewe ndiyo! Nakujua ndiyo. Kwani wewe si Kitarua? Rafiki yangu wa Zamani?
> Mzee Kitarua: Aaa, wewee rafiki yangu? Wewe rafiki wa zamani? Aha, kweli. Sasa nakuona vizuri juu na chini. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 39)

> Mzee Jumai: ... Kitarua ulikuwa mnara unaong'ara nje na ndani ya madarasa yetu ya kujenga taifa jipya mwanzoni mwa uhuru wa nchi yetu. Hasa ulikuwa mweledi wa somo la historia ambalo tulipenda kulitaja kwa kimombo, *Developmental studies*. Tuliongozwa wakati ule ili kumwelewa shetani...' (*Mashetani Wamerud, Uk 40*)

Matini za fasii huchukuliwa kama mtandao wa ulio na athari za kazi nyingine za fasihi (Lemaster, 2012). Kutokana na mazungumzo hapo juu inadhihirika kuwa Mzee Jumai na Mzee Kitarua walibadilishwa na mwendo na wakati kimaksudi ili mwandishi aweze kufanikisha maudhui ya ujenzi wa jamii mpya. Kwa mfano, Kitarua na Jumai waliongozwa mawazo na fikra za mkoloni lakini katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* mwandishi anawasawiri kama wahusika wanaopenda mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa.

Katika tamthilia hizi mbili, vielelezo hivi vinadhihirisha athari za mwingilianomatini kutokana na mazungumzo baina ya Mzee Jumai na Mzee Kitarua. Mwingilianomatini wa kiwahusika unaojitokeza hapa ni wa kidainkronia, ambapo wahusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* wanajitokeza ili kujenga historia inayounganisha tamthilia hizi mbili kama inavyodhihirisha kutokana na mazungumzo ya Mzee Jumai…. *Kwani wewe si **Kitarua**? Rafiki yangu wa **Zamani**?* Kwa upande wa tamthilia ya *Mashetani*, Ebrahim Hussein alitumia Kitaru kama mhusika mkuu kama njia ya kujenga na kuendeleza mgogoro wa kidhamira na kimaudhui katika kazi yake. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed aliamua kuendeleza wahusika hawa ili kuonyesha kuwa historia iliachwa ya ukoloni mamboleo imechukua mkondo tofauti katika ulimwengu wa sasa unaothibitiwa na utandawazi. Kwa hivyo matendo na mazungumzo ya wahusika hutekeleza dhamira ya mwandishi ni wa kimwingilianomatini.

#### 5.1.6.3 Mbinu ya Kiutohozi

Mwandishi wa kazi ya fasihi anaweza akamtaja au akarejelea mtindo wa kiutunzi wa mtangulizi wake akiwa na lengo la kutumia kazi yake kama msingi wa matini yake (Wafula, 2007). Lengo la Wafula ni kuonyesha kuwa kazi ya fasihi huundwa kama njia ya kuendeleza kazi ya awali. Kwa hivyo, kazi ya baadaye huwa ni ukamilisho wa kazi ya awali. Matini huathiriana katika viwango tofauti ikiwemo urejelezi na uendelezaji

wa wahusika. Kauli hii inaugwa mkono na (Allen, 2002), anaposema kuwa mwandishi wa matini huwa amebadili, kuunda na kueleza upya kazi kwa kiwango cha juu ili kuambatanisha kazi yake iwiane kwa namna fulani na mwandishi aliyemtangulia katika mtindo ili kujenga matini yenye ukamilifu. Vilevile, mwingilianomatini hushikirikia kwamba, kazi moja inaweza kuhusiana na matini tangulizi na kusababisha mwanda wa kimwingilianomatini, mwanda hapa ukirejelea upana wa kimaudhui, uhusuka na mtindo wa kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Hata hivyo, siyo lazima mawanda katika kazi zinazochunguzwa ziingiliane katika vipengele vilivyotajwa.

Wamitila (2003), kazi inayoundwa inatokana na utohozi wa matini tangulizi katika mtindo au muundo. Utohozi ni kule kurejelea au kuchukua matini iliyoko katika utanzu mmoja au tofauti na kuuwasilisha katika mwingine wa fasihi. Kwa hivyo, mwandishi anayeunda matini yake kwa kutohoa anaweza kuwa kama kimelea katika kazi iliyotangulia kwa sababu katika kuunda kazi yake, anabadilisha muundo au mtindo wa kiutunzi uliotumika kuunda matini ya awali.

Utafiti huu umegundua kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amebadili na kueendeleza mtindo uliotumika na mtangulizi wake Ebrahim Hussein katika kujenga wahusika wake. Mtindo uliotumiwa katika uundaji wa wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* umetoholewa na kurejelewa na Said Mohamed katika kazi yake. Mbinu ya usawiri wa wahusika iliyotumiwa kusawiri wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* imeendelezwa katika *Mashetani Wamerudi*. Kwa kurejelea kazi ya Hussein alitumia wahusika wakuu kama vile: *Shetani, Juma, Kitaru.* Data ya utafiti ilibainisha kuwa Said Mohamed na Ebrahim Hussein wameathiriana kutokana na jinsi walivyokuza na kuendeleza mhusika Shetani katika kazi teule. Utafiti umebainisha kuwa Shetani ametumika kama mhusika mkuu ambaye habadiliki kutokana na jinsi alivyowasiriwa ili kukuza maudhui ya ukoloni mamboleo. Athari za kimtindo zinazojitokeza katika utafiti huu ni kuwa tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinaathiriana moja kwa moja kutokana jinsi mhusika Shetani alivyokuzwa. Kwa hivyo wahusika wakuu katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* wametoholewa kwa njia inayoibua mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki. Tazama:

Mzee Jumai: wewe nani unayetuuliza sisi tunaenda wapio…?
Mzee Kitarua: Nani anayetuuliza hivyo wakati hatumwoni?

| | |
|---|---|
| Sheta: | Rafiki yenu wa zamani. (*Atoa kicheko cha tabasamu*) |
| Mzee Jumai: | Sisi? (*Mshangao Mkubwa)* |
| Sheta: | Ndiyo nyinyi rafiki zangu (Bado anachekacheka) |
| Mzee Kitarua: | Tokea lini shetani kuwa rafiki wa mtu? (*Mashetani Wamerudi*, Uk 44) |

Data ya utafiti huu imedhihirisha kuwa wahusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni wa kimwendelezo. Kulingana na utafiti huu, majina ya wahusika yametoholewa ili yaingiliane kimtindo na tamthilia tangulizi ya *Mashetani* kama inavyodhihirika hapa: Shetani (***Sheta***), Kitaru (***Kitarua***) na Juma (**Jumai**). Kwa hivyo, uhusika wa mhusika Sheta, Jumai na Kitarua katika *Mashetani Wamerudi* ni mwangwi katika tamthilia ya *Mashetani.* Utafiti huu umebaini kuwa usawiri wa wahusika hawa umetokana usomaji na urejelezi wa mtindo wa kiutunzi wa Ebrahim Hussein.

### 5.1.7 Mandhari ya Kiutunzi

Utafiti huu umebaini kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameiga mtindo wa kiutunzi kutokana na jinsi alivyorejelea mandhari ya kiutunzi. Kwa mujibu wa Allen (2000), mwandishi wa kazi ya fasihi huathiriwa na kazi alizowahi kusoma, matini inayounda huwa ni kimelea cha kazi tangulizi. Kwa hivyo, mwandishi anaweza akatunga matini yake na kuihusisha na mandhari ya kiutunzi na kazi nyingine aliyodurusu. Naye Wamtila (2002), anaeleza kwamba bali na maudhui, msuko na wahusika waandishi wa matini za fasihi huingiliana kimandhari. Mandhari hutumiwa kueleza mahali au mazingira ambapo matukio fulani hutendeka. Mandhari katika fasihi huwa pana na huweza kuchukua aina tofauti. Kutokana na maelezo haya, mandhari huthibiti wahusika kutokana na majukumu mbalimbali ambayo mwandishi hunuia kueleza kupitia kipengele cha wahusika na maudhui.

Utafiti huu umechunguza kuwa tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zilitungwa katika kipindi tofauti cha kihistoria lakini zinarejeleana katika kipengele cha mandhari. Mandhari ni dhana inayoweza kuvuka mipaka ya kiwakati na kihistoria katika kazi ya fasihi. Said Mohamed amerejelea mtindo wa kiutunzi kutokana na jinsi ametumia mandhari ya mbuyu katika utunzi wake. Imebainika kwamba ametumia mbuyu katika kazi ili kusawiri dhamira yake. Neno Mbuyu limetumika na Ebrahim Hussein anaporejelea bara la Afrika kama taifa moja baada ya mapinduzi. Nadharia ya mwingilianomatini hueleza kuwa kazi za fasihi huibua uhusiano mkubwa kati ya matini

moja na nyingine kimwendelezo na kimwigo kwa njia moja au nyingine (Childs na wengine, 2006). Kwa kufanya hivyo kazi moja inaweza kuzalisha nyingine kwa njia inayofanana katika kiwango cha mandhari. Maudhui atayowasilisha katika kazi yake huwa yaanthiriana na mandhari ya kiutunzi.

Utafiti umebainisha kuwa waandishi hawa wameathiriana kutokana na jinsi wamerejelea mandhari ya kiutunzi katika tamthilia hizi mbili na kunaibua mwendelezo kama inavyodhihirika katika vielelezo hivi:

> Sauti ya Mtu: '…ndani atatoka mtetezi. Atakuja Profesa Hafi-Leo-Wala-Kesho mtetezi. Pole pole ataingia uwanjani-uwanja wa utandawazi. Katikati ya uwanja karibu na kibanda, lipo ***shina la mbuyu***. Linaanza kutoa chipukizi. Zinazoota chipukizi…" (*Mashetani Wamerudi*, Uk 2)
>
> *Onyesho la Kwanza.*
> *Mbuyu wenye pango. Vijana wawili katika matembezi yao wanfika mbele ya* **mbuyu** *huo.*
>
> JUMA: Wananchi kwa mara nyingine chini ya ***mbuyu*** huu mimi Juma, na rafiki yangu Kitaru, tutakuonyesheni mchezo wa Shetani na Binadamu…' (*Mashetani*, Uk 1)

Utafiti huu umebainisha kuwa mbuyu ulikuwa eneo au uwanja wa kisiasa ambapo jamii mbalimbali zilikusanyika ili kujadili masuala muhimu yaliyoathiri jamii zao kisiasa na kiuchumi. Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* alitumia mbuyu kama uwanja wa siasa kuwazindua wananchi kuhusu utawala ya kikoloni. Mbuyu unaibua taswira kuhusu muungano wa wanaharakati wapya waliojitolea kuunganisha jamii ili kujikomboa na utawala wa mkoloni kupitia maneno ya Profesa*…'shina la mbuyu lilikatwa mapema baada ya ukoloni, tene hapo hapo uwanjani. Nguvu zetu zilipungua. (Mashetani Wamerudi Uk,2-3).* Tamthilia hizi zinaathiriana kwa njia sawa katika kuonyesha mbuyu ni eneo la kujijua na kijitathimini upya mstakabali mpya kuhusu utawala unaoshuhidiwa katika mataifa mengi ya Kiafrika. Kwa mtazamo wa waandishi hawa, mbuyu unawakilisha bara la Afrika kama invyodhihirika katika vielelezo hivi;

> Prof: Vijana sasa tuketi chini kwa mduara karibu na shina la mbuyu (*Wanaketi chini kwa mduara karibu na shina la mbuyu*.)
>
> Kijana 1: Kwa nini sasa tuketi kwa mtindo huu wa mduara.?
>
> Prof: Duara ni dunia kijana. Duara linafanyika. Linafinya. Linafumba. Lina taabu kupangua. Linashirikisha. Linalinda. Linafanya tutazamane. Kisha tushirikiane. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 30)

## 5.2 Hitimisho

Lengo la sura hii lilikuwa ni kutathmini athari za mtindo katika tamthilia ya *Mashetani* kwenye *Mashetani Wamerudi* na kuonyesha jinsi Said Mohamed aliathiriwa na kuendeleza mtindo wa kiutunzi wa matangulizi wake. Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* alirejelea tamthilia tangulizi ili kufanikisha ujenzi wa dhamira yake. Mbinu hii ya mwendelezo wa kimatini hutumiwa na waandishi wa kazi za fasihi kuonyesha mkondo ambao kazi zao zimekuchua ili kuwiana na kazi zilizotangulia kazi yake. Data ya utafiti huu ilithibitisha kuwa athari za kimtindo zilizobainika katika utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* zilizotokana na urejelezi wa malighafi ya kiutunzi kutoka kwa kazi ya *Mashetani*. Vilevile, utafiti huu umedhibitisha kuwa Said Mohamed ameiga na kurejelea mbinu zifuatazo kama mtindo wa kiutunzi: matumizi ya utanzu wa fasihi simulizi ambapo utanzu wa majigambo, ushairi, nyimbo na maigizo umejitokeza katika matini yake. Imebainika kuwa Said Mohamed ametumia mazingira ya kiutunzi na taswira kama inavyodhihirika katika matini ya awali ya Ebrahim Hussein. Kwa hivyo, utafiti umefaulu kuonyesha kuwa kazi za fasihi hurejeleana kwa njia mbalimbali katika kuonyesha kuwa fasihi huiga na kuendeleza mawazo yake kutoka kwa kazi moja hadi nyingine. Mihimili ya mwingilianomatini hushikiria kuwa matini ya fasihi ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingine kama ilivyodhihirika katika sura hii.

## SURA YA SITA

## VIWANGO VYA MWINGILIANOMATINI BAINA YA TAMTHILIA TEULE

### 6.0 Utangulizi

Sura hii imebainisha viwango vya mwingilianomatini katika tamthilia teule. Sehemu hii inawasilisha data inayodhihirisha viwango vya mwingilianomatini baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. viwango vya mwingilianomatini vilibainishwa na kuelezwa kwa kina. Uchanganuzi wa kila kipengele ulifanywa kwa kuzingatia nadharia ya mwingilianomatini ili kuafikia malengo ya utafiti huu.

### 6.1 Urejelezi

Urejelezi wa kimatini una misingi yake katika nadharia ya mwingilianomatini. Waandishi wa matini za fasihi wanaweza kurejelea wazo au kazi za waandishi kwa njia mbalimbali. Urejelezi wa matini tangulizi humpa msomaji au mwandishi uelewa zaidi wa dhamira anayowasilishia hadhira yake (Miola, 2004). Hata hivyo, Miola anaeleza kuwa kuna viwango mbalimbali vya mwingilianomatini vinavyoweza kujitokeza wakati matini za fasihi zinarejeleana. Viwango hivyo ni pamoja na: unukuzi, uigaji, urejelezi, utohozi, udurufiano, utafsiri na uathiriano. Utafiti huu umebainisha kwamba tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zimedhihirisha urejelezi wa viwango mbalimbali vya mwingilianomatini. Katika utafiti huu Said Mohamed amedhihirisha kwamba ameendeleza kazi tangulizi ya Ebrahim Hussein. Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* inaonyesha mwendelezo viwango vya mbalimbali vya kimwingilianomatini kupitia njia zifuatazo;

#### 6.1.1 Urejelezi wa Tamthilia Tangulizi ya Mashetani

Kwa mujibu wa Wallace (2006), urejelezi wa matini mbalimbali ni mojawapo wa mihimili ya mwingilianimatini, ambapo watunzi wa tamthilia za fasihi wanatumia mtindo wa kazi za awali na kuzifungamanisha na tamthilia zilizotangulia. Kulingana na Wallace (keshatajwa) urejelezi unaweza kuwa wa moja kwa moja. Kwa kurejelea kwa njia hii, mtunzi huwa anatumia mawazo, au anarejelea matukio yaliyojiri katika kazi tangilizi ili aweze kuwavutia wasomaji wanaposoma kazi moja kwa kuihusisha na kazi nyingine ili kujenga msuko ulio wazi kwa msomaji. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed anaeleza haja ya kurejelea tamthilia ya *Mashetani* (1971), alirejelea tamthilia hii ili kuendeleza historia iliyoachwa wazi na mtangulizi wake

Ebrahim Hussein. Anasema kuwa aliamua kuendeleza tamthilia ya *Mashetani* ili kuziba pengo lililoachwa na Hussien alipotunga *Mashetani*, aligundua kwamba wakati unapita na pengine historia ya utandawazi huenda ikafunikwa milele. Tazama kielelezo:

> …Ili kuendeleza historia ya kisasa, mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameamua kufwatiliza kazi ya Hussein katika tamthilia ya *Mashetani*.Jambo hii limekuwa kubwa na lenye kukera kwa upande wa mwandishi wa *Mashetani Wamerudi*, kwani amugundua kwamba wakati unapita na pengine historia ya utandawazi huenda ikafunikwa milele. Kwa hivyo mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameamua kujitosa kwenye kazi hiyo (Utangulizi *Mashetani Wamerudi*, Uk. v)

Mwandishi wa kazi ya fasihi huwa amerejelea mawazo yanayopatikana katika kazi nyingine ili kumweleza msomaji kuwa mawazo hayo yametokana na kazi tangulizi. Urejelezi wa aina hii huvuta msomaji kwenye matini zilizotangulia. Njambi (2023), anasema kuwa dhana ya urejelezi inatumiwa kuonyesha uhusiano uliopo wa kiusemi katika kazi tofauti za fasihi. Kazi ya Said Mohamed inaonyesha kuwa tamthilia ya *Mashetani* imejikita katika nyanja mbalimbali kwa kurejelea matini za kihistoria, urejelezi wa wahusika na matukio ya kihistoria na urejelezi wa falsafa za waandishi mbalimbali. Tamthilia ya *Mashetani* inarejelea matukio ya kihistoria yaliyowahi kutendeka. Hussein alijadili mkondo ambao nchi za kiafrika zilichukua baada ya kupata uhuru. Kwa upande mwingine, mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ameamua kuchukua mkondo tofauti katika kuendeleza historia iliyoachwa wazi na Hussein, ambayo ni historia ya utandawazi ambayo Shetani anatumia kuendeleza mfumo wake wa unyanyasaji, uporaji na ubadhilifu wa mali katika nchi za Afrika ya Mashariki kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki:

> Hussein katika tamthilia yake ya *Mashetani*, alijadili yale aliyaona mapema kuhusu mwelekeo wa nchi zetu za kiafrika zilivyoanza kupita njia mbaya- hasa njia za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kieleimu, kisanyansi, kiteknolojia na kiutamanduni. Hussein alijikita katika nadharia ya mpito wa ukoloni kuelekea ukoloni mamboleo (Utangulizi, *Mashetani Wamerudi*.Uk iv)

Mwandishi anatumia urejeleaji wa aina hii kulinganisha historia ya jamii wakati wa *Mashetani* (1971) ili kudhihirisha namna historia inavyobadilika na kuangazia yaliyoko katika jamii ya kisasa. Falsafa ya Said Mohamed ni kuonyesha mbinu anazotumia Shetani katika kuendeleza uongozi wake. Mwandishi wa *Mashetani* anashikiria kwamba Shetani bado yuko na anazidi kuwatala wananchi kwa kuwakandamiza. Lengo la Said Mohamed ni kukataa kutawaliwa na mawazo ya kishetani kuwatala kisaikolojia.

Kwa hivyo, mwandishi amezingatia masuala yanayokumba mataifa mengi ya kiafrika katika ulimwengu wa sasa. Urejeleaji wa tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi* unasawiri ukaribiano au mfanano uliopo katika ulimwengu wa sasa na wakati wa ukoloni ambapo katika kila hali kuna matabaka mawili yanayozozania uongozi. Tofauti inayoangaziwa na Mohamed ni kwamba, katika tamthilia ya *Mashetani* (1971), vita vilikuwa ni kupigana na mkoloni, ambapo waafrika waliamini kwamba shida zao zilitokana na Mashetani (Wazungu). Wafrika walishikiria kauli kwamba matatizo yao yalitokana na dhuluma walizopata katika mikono ya mkoloni. Hali hii ndio iliyowachochea kuungana ili kuupinga uongozi wa kidhalimu katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*.

### 6.1.2 Urejelezi wa matini za Kihistoria

Ebrahim Hussein na Said Mohamed wanaonekana kurejelea na kutambua matini za kihistoria kama mtindo wa kuonyesha mkondo wa kihistoria katika bara la Afrika. Lengo la kurejelea matini za kihistoria ni kuhakiki simulizi za historia ya Afrika hasa katika kizazi cha sasa inayoashiria ukale (ukoloni) na baada usasa (ukoloni mamboleo). Kwa mtazamo wa Said Mohamed, anawataka wanajamii wa bara la Afrika kutafakari upya ukweli wa historia inayowazingira kuhusu ukale na usasa katika kuungana ili kuleta mapinduzi katika tasnia ya kisiasa, kielimu na kiuchumi.

Waandishi wa kazi fasihi hutumia nadharia ya mwingilianomatini kama mbinu ya mtindo katika utunzi wa kazi za fasihi kama njia ya kudhihirisha kuwa urejeleaji wa kazi tangulizi umejitokeza katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi.* Matini hizi zinaathiriana kupitia urejeleaji wa matini za kihistoria kwa sababu zinaangazia masuala na matukio yanayoathiri bara la Afrika. Kwa hivyo mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* ametumia malighafi ya tamthilia ya *Mashetani* ili kuendeleza kazi yake. Said Mohamed amerejelea dhana za kikoloni zilizotumiwa katika tamthlia ya *Mashetani*. Mwandishi ametumia mbinu hii kulinganisha jinsi wakati unavyopita na jamii ya Kitaru na Juma ilivyobandirika na kuwa na mtazamo tofauti kuhusu historia inayowaathiri.

Kitaru alikuwa mwelendi wa somo la historia kwa sababu bado alikuwa anaipenda hii hali ya ubwana. Mwandishi anaeleza hivi katika kielelezo hiki:

JUMA; Nasikia unajifungiafungia sana ndani. Nini tena?
KITARU: Ah kuna kitabu, hivi ninasoma
JUMA: kitabu gani?
KITARU*:* ***Outline of African History***
JUMA: Hata sijui mzembe gani aliyeandika. Nani vile?
KITARU: Kitabu gani? (*Mashetani*, Uk 15)
JUMA: ***The Essence of Colonial Heritage***
KITARU: Sielewi namna gani au kwa nini nimesoma *law* katika *university*. Toka kuanza kusoma hivi vitabu vya historia hii, mawazo yangu yamebadilika bwana. Inawezekana, ungebadilisha *faculty*, haki tena (*Mashetani*, Uk 15)

Mzee Jumai: Aaa, wewe Kitaru kila ulikuwa mnara unaong'ara nje na ndani ya madarasa yetu ya kujenga taifa jipya mwanzoni mwa uhuru wa nchi yetu. Hasa ulikuwa mweledi wa **somo la *Historia* na *Somo la Maendeleo*** ambalo tulipenda kulitaja kwa kimombo, ***Developmetal studies*.** (*Mashetani Wamerudi,* Uk 40).

Kitaru na Juma wana mtazamo tofauti juu ya historia, Juma anakisifu kitabu cha: ***The Essence of Colonial Heritage.*** Hali hii inaonyesha jinsi Juma anavyopendezwa na mfumo wa kuwatala kutumia mbinu za mkoloni. Kwa upande wa Kitaru, anaonyesha jinsi alivyobadilika tangu aanze kusoma vitabu vya historia. Kulingana na Kitaru, Chuo Kikuu ni mahali pa kupata elimu, mahali pa kujijua na kujisaka, ni mahali pa kuondoa fikra za kishetani. Mwandishi wa kazi ya fasihi anaweza kurejelea matini nyingine katika kazi yake ili kujenga matini iliyo na msuko unayofungamana na matini yake Lemaster (2012). Kwa hivyo, kazi ya fasihi huundwa kama njia ya kuendeleza kazi ya awali. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed anarejelea na kuendeleza mazungumzo kati ya Kitaru na Juma katika kazi yake ili kuonyesha mabadiliko ambayo jamii ya kina Juma amepitia ili kukubali kwamba wakati ule alikuwa ameongozwa na fikra za mkoloni.

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed anaonyesha jinsi elimu ya kikoloni imeleta mgawanyiko wa kitabaka katika jamii. Kitarua anasema kuwa alikuwa amefundishwa fikra za kishetani ili kwenda mbele na kupalilia uozo wa shetani ambao ulikuwa wa kukandamiza, kudhalilisha, kuchukua vitu vya watu na kuvunja sheria. Wakati umefika sasa wa kukomesha nguvu za shetani. Kitarua na Jumai sasa wanakubaliana sasa ni vyema kushirikiana na wanaharakati wengine kama vile Prof kukomesha utamanduni wa ukoloni mamboleo.

### 6.1.3 Urejelezi wa Moja kwa Moja

Kulingana na Miola (2004), matini za fasihi hurejelena ili kukamilisha wazo fulani la mwandishi wa kazi ya fasihi. Matini za fasihi hurejelea maneno au kauli za kazi zilizotangulia ili kuhusiana na matini mpya. Urejelezi wa matini za awali unaweza kuwa dhahiri au usiwe wa moja kwa moja. Mojawapo wa mihimili ya mwingilinomatini ni kuwa matini huweza kurejeana ili kukamilishana kimawazo. Kwa hivyo, matini za baadaye huweza kupata maana kwa kuhusishwa na kazi tangulizi. Data ya utafiti huu imedhihirisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amerejelea kazi ya Ebrahimi Hussein katika utunzi wa kazi yake. Mojawapo wa mhimili wa mwingilianomatini husisitiza kuwa kazi ya fasihi ni mkusanyiko wa matini zilizotungwa hapo awali. Mwandishi huwa amerejelea na kuiga baadhi ya vipengele vya kiutunzi kutoka kwa matini tangulizi. Tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinarejelea matukio ya kihistoria ili kukamilisha dhamira ya mwandishi kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki:

| | |
|---|---|
| BINADAMU: | Maombi yako yamekubaliwa. Sherehe itafanywa. |
| SHETANI: | Ni vipi tutaisherekea? |
| BINADAMU: | Kwa ***Waltz*** (*Mashetani*, Uk 7-8) |

| | |
|---|---|
| Kijana 1: | Mashetani? Mashetani gani hao? |
| Prof: | Wale wale waliotuzechezea mchezo wa maneno ya dansi ya ***waltz*** huku wakijidai kwamba wangeondoka kwenda kwao. Kumbe wangerudi na sisi tumewaita na kudhani ni wakweli |
| Kijana 1: | Sasa wamerudi au sivyo? Wako tayari kucheza mchezo mwingine mpya au siyo? Na sivyo? Na sisi tunakubali mchezo wao… (*Mashetani Wamerudi*, Uk7) |

Mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* anaonyesha jinsi Mwafrika alivyokeunguka baada ya kupata uhuru. Binadamu anasherekea kifo cha shetani baada ya kujinyakulia uhuru. Dansi ya kikoloni ni ishara ya ukoloni mamboleo. Kulingana na Hussein hii ni dansi ya kishetani, uhuru ambao mtawaliwa anapata ameadaliwa na mtawala (Shetani) mwenyewe. Hii ni njia nyingine ya shetani kuendeleza uongozi wake. Kwa hivyo, densi ya kikoloni inaashiria utamanduni tofauti wa kiafrika. Naye mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anaonyesha jinsi mwafrika alivyoabadilika, anajiuliza maswali kutokana na upekuzi wa historia ya jamii yake. Kulingana na Said Mohamed mkoloni aliondoka lakini alibuni njia mpya ya kuendeleza utawala wake. Mwandishi anaeleza hivi kupitia Kijana 1 anaposema kuwa... hakuondoka kwa sababu amebuni mbinu mpya za

kutawala wafrika. Mwandishi anaonyesha kwamba kuna taasisi ambazo zimebuniwa na Shetani ili kuendelea kukandamiza mataifa ya Afrika, kiuchumi, kijamii na kisiasa. Kijana 1 anawatahadhalisha wananchi kuwa ange kwa sababu uhuru wao uliandaliwa na mkoloni.

Waandishi wa tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* wamerejeleana katika kazi zao kuonyesha dhuluma anazopitia katika juhudi zao kupigania uhuru wake kwa kurejelea mchezo kati ya *Red Indians* na *Cowboys* (Wahindi wa Marekani). Hili linadhihirika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ambapo mwandishi amerejelea kazi ya Alex Heley's "Roots: *The Saga of an American Family*" kuonyesha taashira ya Wafrika walipokuwa wakipigania uhuru wa kujieleza na kupigana na ukoloni mamboleo. Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anaonyesha mwamko mpya kwa sababu Wafrika hamthamini tena Shetani. Katika tamthilia ya *Mashetani,* mwandishi alitumia filamu ya *Red Indians* na *Cowboys* kuonyesha jinsi mwafrika alivyokengeuka na kutawaliwa na fikra za kishetani. Kulingana na Hussein *Cowboy* anawakilisha tabaka la juu au mwenye nguvu huku *Indians* wanawakilisha tabaka tawaliwa ambalo limenyanyaswa. Katika mapambano yanayohusu mkoloni, Kitaru anataka awe ndiye mwenye nguvu. Hapendi sinema za *Cowboys*, wanaowaua Red Indians ili kuonyesha nguvu za mkoloni. Hii ni kuonyesha jinsi Shetani alivyoingia katika fikra zao hata wasiweze kutambua wanatawaliwa na shetani. Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anarejelea filamu ya *Kunta Kinte* ili kuondoa kasumba ambayo imewaathiri Wafrika ambao wanaendeleza fikra za Shetani katika mataifa yao. Said Mohamed anaonyesha kuwa, ili kujikomboa kimawazo, lazima wananchi wasikubali kulazimisishiwa uongozi wa mkoloni.

Tazama kielelezo hiki:

| | |
|---|---|
| JUMA: | Twende sinema basi. Itakusaidia |
| KITARU: | Hakuna sinema nzuri |
| JUMA: | Iko cowboy moja, tikiti juu yangu. |
| KITARU: | Acha kutumia pesa zako ovyo. Zitakufaa mwenyewe. |
| JUMA: | I see (kwa uchungu) I see, Alaa |
| KITARU: | Siyo hivyo inavyochukulia wewe. |
| JUMA: | Kwani mimi ninachukulia aje? |
| KITARU: | Siyo bwana. Mi ***cowboy*** films sipendi |
| | (*Mashetani*, Uk 18) |

JUMA: Sinema yenyewe ninaijua hata kabla ya sijaiona. ***Cowboys*** atawaua ***Red Indians*** wote peke yake. Mimi mchezo ukaonyesha ugomvi au mgongano baina ya mwenye nguvu ***(cowboys***) na asiye na nguvu (***Red Indians***), siupendi.

Sheta: Sisi na mabosi wenu. Pia ni mabosi wa mabosi. Lazima mtakubali

Kijana 1: Mimi sitakubali kulazimishiwa ubosi, kwani ubosi huja kwa matendo ya kuhesimiana. Unakumbuka ***Kunta Kinte*** wa filamu iitwayo ***Roots? (****Mashetani Wamerudi, Uk 49)*

Filamu za *cowboys* na *Kunta Kinte* zilikiwa zinatumiwa na wakoloni kuonyesha uwezo wao dhidi ya Wafrika (mtawaliwa). Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* anaonyesha kuwa wananchi wamegundua mbinu zinazotumiwa na Shetani kuendeleza uongozi wake. Shetani anatumia nguvu kuhakikisha kwamba viongozi waliochanguliwa ni vibaraka wake. Kwa sababu hii, wananchi hawatakubali ubosi wa kulazimishiwa kama ilivyokuwa hapo awali. Uhusiano wa vifungu unadhihirisha kuwa kuna mwingilianomatini baina ya watunzi hawa. Mwingilianomatini katika kazi za fasihi husisitiza kwamba historia huchangia katika uandishi wa kazi zinazoingiliana kutokana na jinsi mwandishi amerejelea matukio ya kihistoria. Urejelezi wa kimatini unaweza kuwa dhahiri au usio wa moja kwa moja (Ponera, 2014)

### 6.1.4 Urejelezi wa Kiutohozi

Data ya utafiti imethibitisha kuwa kuna mwingilianomatini katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kutokana na jinsi amekuza na kuendeleza wahusika wake. Kimsingi matini za fasihi hutegemeana kwa matini mbalimbali ili kukuza dhamira ya mwandishi baina ya kazi zinazorejelewa (Zengin, 2019). Mwingiliano matini hushikiria kwamba, kazi moja inaweza kuhusiana na matini tangulizi na kusababibisha mwanda wa kimwingilianomatini, mwanda hapa ukirejelea upana wa maudhui, uhusika na mtindo wa kuwasilisha dhamira ya mwandishi. Hata hivyo, siyo lazima kazi zinazochunguzwa ziingiliane katika vipengele vilivyotajwa. Kazi za fasihi huenda zinarejelea kipengele kimoja au vipengele zaidi ya kimoja.

Kulingana na Wamitila (2003) utohozi ni kule kurejelea au kuchukua matini iliyo katika utanzu mmoja na kuiwasilisha katika utanzu mwingine. Kazi inayoundwa inatokana na

utohozi wa matini tangulizi katika mtindo au muundo ule ule au muundo tofauti. Mwingilianomatini huhusisha kurejelea mtindo wa kazi za awali katika matini mpya. Mwandishi anayeunda matini yake kwa kutohoa anaweza kuwa kimelea wa kazi iliyotangulia kwa sababu katika kuunda kazi yake, anabadilisha muundo au mtindo uliyotumika kuunda matini ya awali. Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* amerejelea na kuendeleza mtindo uliotumika na matini ya awali katika kuunda wahusika. Kipengele cha uhusika kimerejelewa na kutoholewa na S.A Mohamed katika utunzi wake. Mbinu uliyotumiwa hapo awali ya kusawiri wahusika katika tamthilia ya *Mashetani* imeendelezwa katika *Mashetani Wamerudi* na kuathiri pakubwa usawiri wa wahusika ili msomaji aweze kubainisha ujumbe ulioendelezwa katika matini ya *Mashetani Wamerudi*. Kwa kurejelea kazi ya Hussein alitumia wahusika wakuu kama vile; *Shetani, Juma* na *Kitaru* na mandhari ya *mbuyu*. Vipengele hivi vya mwingilianomatini vimetumika na Said Mohamed katika kazi yake ya *Mashetani Wamerudi*, japo kipengele cha uhusika kimetoholewa, vipengele vingine vimeendelezwa kama vilivyotumika katika kazi tangulizi. Kwa mfano, Kitaru (***Kitarua***), Juma (***Jumai*)**, Shetani (***Sheta***) na Mbuyu (***mbuyu***), mfano katika kielelezo hiki:

| | |
|---|---|
| Mzee Kitarua: | Nani aliyetuuliza hivyo wakati hatumwoni? |
| Mzee Jumai: | Rafiki yetu wa zamani (*Atoa kicheko cha tabasamu*) |
| Mzee Kitarua: | Tokea lini shetani kuwa rafiki wa mtu? |
| Mzee Jumai: | Hujawahi kuwa rafiki zamani utakuwa rafiki wetu leo? |
| Sheta: | Tuyaache ya zamani. Tushikamane leo. (*Mashetani Wamerudi*, Uki 44) |

Mwandishi wa matini ya fasihi anaweza kutumia wahusika katika kazi yake kwa kutumia mbinu ya kimwingilianiomatini. Wahusika hujitokeza katika njia tofauti na huchangia katika kuibua dhamira zinazofanana ingawa sifa hii huwa haijitokezi katika matini zote, zinaingiliana katika kipengele cha uhusika. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* mwandishi ametumia mhusika Shetani (sheta) kama mhusika bapa ambaye habadiliki. Mhusika bapa huwa habadiliki na huonyeshwa kwa upande mmoja tu na hutumiwa na mwandishi kama mhusika mkuu (Saraswati, 2019). Utafiti huu ulidhihirisha kwamba aina hii ya wahusika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ni mojawapo wa mbinu inayotumiwa na mwandishi kuendeleza na kukuza dhana ya umwingilianomatini. Katika tamthilia tangulizi ya *Mashetani*, mhusika Shetani ametumika katika kukuza dhana ya unyonyaji na ukoloni mamboleo, sifa hii pia

imedhihirika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Mhusika huyu alikuza sifa hii anaposema kwamba:

> Sheta: Ukweli wa kwamba hatuko katika mfumo wa zamani wa unyonyaji wa ukoloni mamboleo. (*Mashetani Wamerudi*, Uk 18)

Kulingana na Wamitila (2002), wahusika katika matini za fasihi wanaweza kumrejesha msomaji katika kazi zilizotangulia. Kwa kawaida sauti za wahusika hutumiwa kujenga dhamira ya mwandishi. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* Said Mohamed anatumia wahusika (*Kitarua* na *Jumai*) kuonyesha historia na mahusiano yao yalivyo katika harakati mpya za kijikomboa na kutokana na mawazo na kusumba ya kikoloni (Shetani). Data ya utafiti huu vilevile ilibanisha kuwa Said Mohamed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ametumia Mzee Kitarua na Mzee Jumai kama wahusika huria katika kazi ili kuendeleza na kukuza dhamira yake. Mhusika huria katika matini za fasihi hubadilikabadilika kila wakati kutegemea jinsi alivyokuzwa katika kazi ya fasihi (Garci, 2016). Kwa hivyo, urejeleo wa Mzee Kitarua na Mzee Jumai umetumika na mwandishi kuonyesha mabadiliko yaliotukia wahusika hao katika kufanikisha ujenzi wa maudhui katika matini yake.

Mwandishi anatoa mwanga kuonyesha mabadiliko ambayo wahusika hawa wamepitia, wamejifunza mengi kutokana fikra za ushetani. Hapo awali ilikuwa tu ni kujilimbikizia mali, kukandamiza, kudhalilisha na kuchukua vitu vya watu. Katika *Mashetani Wamerudi*, mwandishi anaonyesha Mzee Jumai kama mhusika ambaye amepitia mabadiliko, amemtwika jukumu la kuendeleza historia na utamanduni mpya. Kwa hivyo, Mzee Jumai ni sauti ya mwandishi inayoonyesha jinsi hali ilivyokuwa zamani baada ya kupata uhuru. Tazama kielelezo hiki:

> Mzee Jumai: Aha, sasa naona tunaanza kutupilia mbali mtindo wa kuzungumza kwa mafumbo. Sasa tunaanza kuzungumza kinagaubaga, kwani wakati wa kuiokoa nchi yetu umefika. Kusema kweli umepita wakati wa zamani, au sivyo wananchi? (*Anaashiria hadhira)*
>
> Mzee Kitarua: Unajua… (*Anamtaza kwa ukaribu rafiki yake Jumai. Harafu anageuza shingo. Akaitazama hadhira*) Aaa, mnajua kwamba mimi nilikuwa na kiburi kisicho na maana. Kwa hali hiyo hata marafiki zangu waliniita majina mengi… mapozi, mpandangazi, limbukeni, kupe, bwanyenye, mla-mali ya -umma…Aaa, orodha ndefu isiyokuwa na mwisho *(Mashetani Wamerudi*, Uk 41)

Urejelezi wa kielelezo hiki ni kuashiria kuwa lugha ya mwandishi inakashifu mtindo na imani ya kikale iliyokuwa inaendeleza ubinafsi miongoni mwa mwananchi. Anatumia Mzee Jumai kuonyesha athari za mkoloni zilizokumba jamii yake baada ya majilio ya mkoloni. Mwandishi anamtumia kuonyesha haja ya mabadiliko kama njia ya kujitambua ili kuunda jamii mpya. Utafiti huu ulibaini kuwa Said Ahmed Mohamed ameiga na kurejelea wahusika katika tamthilia ya Hussein ili kurejelea athari na nguvu za Shetani katika kuendeleza ukoloni mamboleo. Kitaru na Juma katika kazi ya Hussien walikuwa wahusika wakuu. Walipewa nafasi zinazolingana ili kusawiri dhamira ya mwandishi. Mwingilianomatini ni mbinu inayotumiwa na mwandishi katika kutafsiri kazi za fasihi kwa kujikita katika kipengele cha matini moja kuathiriana kimawazo kutoka kwa kazi tangulizi (Eliot, 2015). Urejelezi wa wahusika hawa katika tamthilia *Mashetani Wamerudi* ya Said Mohamed ni ishara kwamba ujumbe unaowasilishwa na watunzi hawa unarejeleana na kukamilishana. Kutokana na matini hii mgogoro unajitokeza katika tamthilia ya *Mashetani* baina ya Kitaru na Juma na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* umetokana na urejelezi wa wahusika kimwendelezo.

### 6.1.5 Urejelezi wa Mila na Desturi za Kigeni

Mila ni suala muhimu katika jamii na huangazia historia na mitazamo ya jamii iliyopita na iliyopo. Historia humsaidia mwandishi kubuni kazi nje ya jamii yake kwa kuzingatia jinsi jamii anayoiandikia inavyoelendeleza shughuli za kila siku (Wamitila, 2003). Kila mila huwa na vipengele ambavyo ni uti wa taratibu za maisha ya kila siku. Mila hujumuisha historia, miiko, matambiko, matibabu na sheria zinazohusu taratibu za jamii. Desturi hujumuisha mavazi, vyakula na namna ya kula na mavazi.

Desturi hubadilika kulingana na mahitaji na matarajio ya jamii. Mila na desturi hurejelea tabia za jamii au kundi la watu fulani. Kila jamii huwa na muundo fulani wa kuwasilisha utamanduni wake katika kurejelea mambo ya kawaida kama vile; lugha, sheria na taratibu zinazotokana jamii kuingiliana na jamii nyingine. Maingiliano haya humfanya mwandishi wa matini ya fasihi kuchanganya mila na desturi za jamii fulani ili kukidhi taratibu za jamii anayoandikia kazi yake. Waandishi wa tamthilia ya *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* walitunga kazi zao kuegemea mazingira mbalimbali yaliyopita na yaliyopo. Kazi yoyote ile ni madadiliko ya mpangilio wa

kazi nyingine, kazi za fasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi ya, matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja ambapo matini tangulizi hufyonzwa na kujibiwa na matini mpya, matini za kifasihi akanukuu, akageuza na kuiga kwa kurejelea matini nyingine Kristeva (1986). Utafiti huu ulibainisha kuwa tamthilia tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinadhihirisha mwingiliano wa urejelezi wa mila na desturi na athari zake. Tazama kielelezo:

ONYESHO LA II

*Hotelini: Juma yuko peke yake mezani. Anakunywa* ***soda.*** *Baada ya muda wanakuja watu wawili. Wanakaa meza ya pili. Pembeni watumishi wawili wanaongea*)

MTUMISHI 1: (*mezani*) Yes sir.

MTU 1: *Aam…yes. Can you fetch one* ***bear*** *and one* ***whisky****?*

MTUMISHI 1: ***Whisky, double*** *or* ***single****?*

MTU 1: No. One bear for him, and one *whisky* for me.

MTUMISHI 1: Ndiyo bwana; hiyo ***whisky*** iwe *double* au *single* (*Mashetani*, Uk 40)

Prof … **togwa** tamu hii. Tamu tokea kinywani mpaka damuni. ***Coca Cola*** itawezaje kutia fora mbele ya togwa? Basi tu-*abrogation* yaani vidonge vya dawa ndani ya sheria ya kufuata na *kukanusha* katika kutuziba vichwa vyetu na kutuchezesha ngoma kwenye TV, ili kibaya kiwe chetu daima na kizuri kiwe chao daima. Kibaya chao kiwe kizuri chetu! *Coca Cola* si kwa siha wala si kwa ladha yoyote ikilinganishwa na tongwa. Usisikie wewe! (*Mashetani Wamerudi,* Uk7-8).

Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa mwandishi wa *Mashetani Wamerudi*, ameandika kazi yake kwa kuegemea mazingira na utamanduni Kiafrika. Mwandishi anakashifu viongozi waliokenguka na kupalilia utamaduni wa kigeni. Aidha, muktadha uliokuwepo wakati wa *Mashetani*, ulisisitiza mila za kigeni kama inavyobainika katika jamii. Mwafrika alikengeuka na kusahau utamanduni wake. Baada ya kufunzwa lugha ya mtawala, mwafrika anaanza kuiga mbinu za mtawala wake. Kwa hivyo Said Mohamed, anaona ni vyema mwafrika kuungana na wenzake ili kufufua utamanduni uliozikwa na mtawala wa wake. Akirejelea ***Tongwa***, neno linalotumika kuwakilisha utamanduni wa kiafrika. Kupitia mhusika Prof, mwandishi anasifu utamanduni wa Kiafrika kuliko utamanduni wa kigeni ambao umewakilishwa na ***Coca Cola, whisky*** na

***beer***. Kulingana Said Mohamed ni kuwa mkoloni anadhalilisha utamanduni wa Kiafrika, mkoloni anajiweka katika nafasi ya kwanza na kukanusha utamanduni wa Mwafrika ambao unaleta faida. Kulingana na Mkoloni, biashara ni muhimu kuliko desturi za kiafrika, lengo lake ni kuhakikisha kwamba hakuna maendeleo yoyote yanayoshuhudiwa katika bara la Afrika kwa sababu biashara zote zinadhibitiwa na mkoloni. Mwandishi anasisitiza kwamba maendeleo huja kwa kuwaza, kujaribu na kutekeleza sio kwa kuiga mienendo ya kigeni tu.

### 6.2 Uigaji

Baadhi ya waandishi wa kazi ya fasihi huiga sehemu au mbinu za uandishi za watunzi wengine katika matini zao. Kulingana na (Allen, 2000), dhana ya uigaji hushikiria kuwa binadamu alianza kuiga vitu ua maumbile halisi yanayomzunguka. Dhana ya uigaji ina misingi yake katika wana-nadharia wa Kirumi. Kazi tangulizi inapojipata katika matini ya sasa, sehemu ya matini tangulizi huwa na uwezo wa kuathiri kazi ya sasa na kuwa wigo wa matini ya awali. Hakuna matini ya fasihi ambayo huwa ni ya asilia; kila mwandishi wa matini huwa ameiga au kurejelea kazi iliyoandikwa hapo awali. Kazi ya fasihi huwa inapata maana inapohusishwa na kazi ziliotangulia.

Tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*, zinadhihirisha uigaji, kwa kiasi fulani kutokana na urejelezi wa kauli za moja kwa moja kutoka kwa kazi tangulizi ya *Mashetani*. Tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, inafuatilia kwa makini nadharia hii ya Uigaji. Said Mohamed ameiga baadhi na kurejelea vipengele vya kiutunzi kutoka kwa tamthilia ya *Mashetani* kama inavyodhihirika katika kielelezo hiki:

KITARU: Kwa nini?
JUMA: Sababu nyingi
KITARU: Mojawapo?
JUMA: ***Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono***
KITARU: Pili?

JUMA: Wewe ***unaishi leo. Mimi ninaishi jana.*** Tutakuwaje marafiki? Na kila leo yako ni kidato cha jana yako. Mimi, ***kila leo yako ni kidato cha jana zangu***. Na kila nikienda huko, nikirudi ninarudi na hadithi…hadithi za Mashetani (*Mashetani* Uk,56)

Kijana 1: (*Anajitokeza kifua mbele*) Sasa tunazijua mbinu za shetani na wala hatuziogopi tutakapokutana mwambani, sisi na yeye

> na wahisani wake. *Kinjeketile* aliwakusanya watu lakini alishindwa na mwelekeo wa ukombozi. Alitumia falsafa au itikadi ya maji ya tohara. Mhusika ***Juma*** ndiye aliyeongoza tamthilia ya ***Mashetani.*** Akina ***Kitaru*** ndio waliokuwa wadhabiti wa serikali na nchi yetu sisi tukaongozwa kama punguani au mabwege. Tulibaki kutazama ndoto ya ***kesho na kesho kutwa***. Lakini historia inazidi kutufumbua macho na kutuongoza. Hakuna mtu asiyefahamu isipokuwa mwendawazimu. Mwisho **Juma** na **Kitaru** walimalizia tamthilia yao kwa kuangushana chini kwa mzaha huku wanagombana. ***Kesho*** tutakuwa wamoja. Hatimaye Juma alitoa maneno ya busara- ***Mpanda gazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mikono'*** Kwa wakati ule ulikuwa msemo wa kungojeana tu, huyu aende huku na yule aendelee kule**. Katika karne hii hatutaki tuendelee kuwa kinyesi cha mbuzi kinachotawanyika. Tunataka tuwe sangara kwenye mlolongo wa pamoja. Kama hatutashikana mikono na kwenda upande mmoja, basi sote tutaanguka chini na kuramba mchanga**! (*Mashetani Wamerudi*, Uk 62)

Vielelezo vilivyorejelewa hapo vinaonyesha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* imeiga na kurejelea moja kwa moja tamthilia ya *Mashetani.* Said Mohamed ameiga wahusika na kuwatumia katika kazi yake. Tamthilia hizi zinaingiliana kwa jinsi zinavyorejelea hali ilivyokuwa hapo awali. Kulingana na Said Mohamed, maendeleo yatapatikana tu wakati wananchi wataweka tofauti zao kando na kuzingatia umoja ili kuzindisha juhudi za kupigana na nguvu za shetani. Akirejelea kazi ya Hussein, anaonyesha mgawanyiko ulikuwepo kati ya Kitaru na Juma. Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* wahusika kama vile Kijana 1 wako katika harakati za kutetea haki zao na kijisaka kwa kusisitiza umoja. Ili kufaulu katika azma yao, lazima waelewe historia ilivyochangia mgawanyiko na kupalilia uongozi wa mkoloni uliogawanya wananchi katika matabaka mbalimbali. Said Mohamed anaamini kwamba uhuru wa kweli una misingi yake katika kujitambua. Anaona kwamba, ikiwa wananchi wanatazamia kujisaka na kujikomboa, hawana budi ila kuzuru machimbo ya historia yao. Hivyo basi, dhamira ya tamthilia ya *Mashetani* inafanana na dhamira inayorejelewa katika tamthilia *Mashetani Wamerudi.*

Katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, Said Mohamed amerejelea tamthilia ya *Kinjeketile* (1969), utepe unaofungamanishwa na maandishi haya ni kwamba mashujaa walioishi zamani wamezaliwa na kuumbwa upya katika tamthilia ya *Mashetani*

*Wamerudi*. Lengo kuu la kuibusha mashujaa katika tamthilia ya *Kinjeketile* ni kwamba mwandishi ana imani kwamba wakati umefika wa kupigania ukombozi mpya wenye kuleta matumaini hapo mbeleni. Ukweli unaojikoteza ni kuwa, jamii imezinduka na imetambua kwamba wana nafasi mpya ya kujenga historia mpya iwapo hawatakubali kugawaywa katika makundi. Kitaru na Juma ni viwakilishi wa raia ambao wametambua kwamba wakati umefika wa kuleta mageuzi katika mataifa yao.

Kusudi la mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* kurejelea historia ya Kitaru na Juma ni kuonyesha kitu kilicho bayana baina yao ni historia na uchumi, kwa hivyo mkono wake wa urafiki umemchopoka Juma. Mgongano wao, ambao ni wa kitabaka unachangiwa na ubinafsi na kuchangia mgongano wa umma unaoletwa na vibaraka wa mkoloni kama anavyosema…***Katika karne hii hatutaki tuendelee kuwa kama kinyesi cha mbuzi kinachotawanyika,….Tunataka tuwe sangara kwenye mlolongo wa pamoja…(****Mashetani Wamerudi****, Uk 62)*** Kwa mtazamo wa Said Mohamed, ni wazi kuwa tatizo la utabaka baina ya wanajamii limesabisha mgawanyiko katika mataifa mengi ya Kiafrika. Kwa hivyo, mwandishi anahimiza kuwa mataifa ya Afrika yatapa maendeleo iwapo wananchi watashirikiana pamoja.

Data ya utafiti huu imebainisha kwamba Said Ahmed Mohamed ameiga mtangulizi wake ili awasilishe ujumbe wake kwa kufungamanisha kazi yake na historia katika tamthilia ya *Mashetani*. Mwandishi wa *Mashetani Wamerudi* amedhihirisha urejelezi wa historia ili kuonyesha japo mkoloni aliondoka, hakufukuzwa bali aliondoka kwa hiari yake lakini kivuli chake bado kinatawala mataifa changa ya Afrika. Imebanika kuwa mwingilianomatini hujitokeza katika kazi za fasihi na humpa mwandishi nafasi ya kubuni matini yake kwa misingi ya kazi za awali (Eagleton, 1983). Mwandishi anaweza akaiga na kutaja mwandishi wa kazi ya awali. Kwa mfano, Said Mohamed katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameiga na kunukuu Hussein katika tamthilia ya *Mashetani*, Mhusika Juma na Kitaru wanajitokeza katika kazi ya Said Mohamed. Utafiti ulidhihirisha kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* ameiga na kurejelea kazi ya Hussein moja kwa moja kama inavyodhihirika katika kielelzo hiki.

> JUMA: 'Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono..." (*Mashetani*, UK 56). Kijana 1: …**Mpanda ngazi na mshuka ngazi hawawezi kushikana mkono**..." (*Mashetani Wamerudi*, 62).

> ***Kijana 1…kwa nini Ebrahim Hussein unamleta kwenye karne hii iliyokwisha na Kinjeketile?*** *(Mashetani Wamerudi, Uk 5)*

Mwandishi huwa na uhuru wa kuiga kazi ya awali ambaye analenga kutumia kazi yake kama msingi wa kuzalisha matini mpya (Kristeva,1986). Mwandishi wa matini mpya anaweza kutaja mwandishi pia anaweza kurejelea wahusika na akutumia mandhari sawa ili kuonyesha kuwa matini imeathiriwa na kazi tangulizi. Suala la uigaji hurejelea na kuegemeza uelewa wa matini husika katika mpya ili kukamilishana kimawazo kama inavyodhihirika katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Data ya utafiti huu ilidhihirisha kwamba kuna uigaji wa vipengele vya kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* (1971) vimekuzwa na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi (2016).*

### 6.3 Hitimisho

Sehemu hii imebainisha na kujadili baadhi ya viwango vya kimwingilianomatini kwa njia ya urejelezi na uigaji katika tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Mhimili wa nadharia ya mwinglianomatini ulibainisha kuwa kuna mawasiliano baina ya mwandishi wa kazi ya fasihi huambatana na namna kazi ya awali ilivyorejelewa na kufumwa katika kiwango cha urejelezi na uigaji.  Kwa hivyo, kazi ya fasihi inajihusiha na kugeuza kazi ya awali ili iwiane na matini ya sasa ulikuwa muhimu katika uchanganuzi wa data katika sehemu hii.

Imebainika kwamba tamthilia hizi mbili zinadhihirisha mwingilianomatini katika ukuzaji wa mtindo wa kiutunzi. Aidha, tamthilia hizi zimedhihirisha mwingilianomatini kwa kurejelea matini za aina mbalimbali kama vile; urejelezi wa moja kwa moja, marejeleo ya kihistoria, Urejelezi wa mila na desturi za kigeni, urejelezi wa kiutohozi na urejelezi wa tamthilia ya *Mashetani*. Vifungu vilivyorejelewa hapo juu vinadhihirisha kuwa, matini hizi zinaingiliana na kukamilishana. Wahusika na matukio ya kihistoria yamerejelewa ili kukuza na kuendeleza dhamira ya mwandishi. Utafiti huu umebainisha kuwa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*, imeiga, imenukuu na kurejelea mtindo ya kiutunzi wa Hussein kwa njia zilizobainishwa hapo awali.

# SURA YA SABA

# MUKTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 7.1 Muktasari

Utafiti huu ulikuwa wa kuchungunza mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) katika *Mashetani wamerudi* (2016). Madhumuni yalikuwa ni kuchunguza mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi*. Vilevile utafiti huu ulitathmini athari za kimtindo katika tamthilia ya *Mashetani* kwenye *Mashetani Wamerudi*. Kadhalika, utafiti huu ulibainisha viwango vya mwingilianomatini baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Umuhimu wa utafiti huu ulikuwa ni kuchangia katika maandishi ya kitaaluma kwa wataalamu kwa kuonyesha jinsi waandishi wa kazi za fasihi wanavyofaidi mbinu za kiutunzi kutokana waandishi waliotangulia. Utafiti huu ulifanywa maktabani.  Mbinu ya kimaelezo ilitumika katika ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* ziliteuliwa. Data kutokana na matini hizi ilisaidia kufikia malengo ya utafiti.

Ripoti katika utafiti huu imepangwa katika sura saba. Sura ya kwanza inahusu mada ya utafiti ambapo usuli wa mada hiyo umejadiliwa. Sura hii inahusu suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, upeo na mipaka ya utafiti na maelezo ya istilahi mbalimbali zilizotumika katika utafiti. Sura ya pili inahusu mwauo wa maandishi na nadharia ya utafiti. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti na uchangunuzi wa data. Sura ya nne, tano na sita zimeangazia mwendelezo wa kimaudhui, athari za kimtindo baina ya matini teule na kubainisha viwango vya mwingilianomatini. Ufafanuzi umetolewa kuonyesha jinsi tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* zinavyoathiriana kwa kuegemea malengo ya utafiti. Sura hii pia imeeleza jinsi Said Mohamed amerejelea na kufaidi mbinu za kiutunzi kutoka kwa mtangulizi wake Ebrahim Hussein. Vilevile, sura hii imeonyesha jinsi tamthilia zinavyoingiliana na kuendeleza maudhui kwa njia inayoshabiana kutokana na jinsi masuala makuu yaliovyokuzwa na kuendelezwa katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi*. Sura ya saba ilihitimisha kwa kutoa muktasari, matokeo, na mapendekezo ya utafiti.

## 7.2 Matokeo ya Utafiti

Madhumuni ya kwanza ya utafiti huu yalikuwa ni kuchunguza mwendelezo wa maudhui ya tamthilia ya *Mashetani* katika *Mashetani Wamerudi*. Ilibainika kwamba kuna mwendelezo wa kimaudhui baina ya tamthilia teule ambao unapatikana katika kiwango cha wahusika na dhamira. Utafiti huu umegundua kwamba wahusika katika matini hizi wamekuzwa kwa njia ambayo inawasilisha dhamira ya mwandishi. Katika uchunguzi wa maudhui, Said Mohamed amerejelea kazi ya mtangulizi wake kama mbinu ya kukuza na kuendeleza mgogoro uliopo baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Mgogoro huu umejengeka kwa misingi kwamba Said Mohamed ameamua kuunganisha historia iliyoachwa wazi kwa kurejelea kazi ya Hussein. Kwa hivyo, matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kwamba, tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* imekuzwa kutokana na urejelezi wa ki-mwingilianomatini. Kauli ya utafiti huu ni kuwa kuna ukuruba wa kimaudhui baina tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi* kwa sababu utunzi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* umetokana na udurusu wa kazi tangulizi ya Ebrahim Hussein.

Matokeo ya utafiti huu ya yamethibitisha kuwa kuna athari za kimtindo baina ya tamthilia za *Mashetani* na *Mashetani Wamerudi*. Hili limetokana na jinsi Said Mohamed na Ebrahim Hussein walivyoingiliana katika mbinu zao za kiutunzi. Utafiti huu umedhihirisha kwamba Said Mohamed amekumbatia na kuendeleza utanzu wa fasihi simulizi katika kazi yake. Mbinu hii imetumika katika kukuza na kuendeleza maudhui.  Kwa mujibu utafiti huu, utanzu wa majigambo na maigizo umetumika kama mbinu ya kuonyesha jinsi shetani anavyodhulumu na kuendeleza uthibiti katika mataifa ya Kiafrika. Vilevile, majigambo yametumika kuonyesha jinsi Mwafrika alivyokengeuka baada ya kupata uhuru. Aidha, majigambo yametumika katika tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* kuonyesha historia iliyomzingira binadamu katika kuonyesha jinsi ukoloni mkogwe upo katika kipindi cha sasa.

Kadhalika, utafiti huu umebainisha kuwa tamthilia za *Mashetani* (1971) na *Mashetani Wamerudi* (2016) zinarejeleana kupitia viwango vya ki-mwingilianomatini. Imebainika kwamba mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani Wamerudi* amerejelea na kuendeleza kazi ya Ebrahim Hussein kwa njia mbalimbali kama vile: urejelezi wa wahusika (kiutohozi), urejelezi wa moja kwa moja wa tamthilia ya *Mashetani*, urejelezi wa matini

za kihistoria na uigaji. Kazi ya Hussein imerejelewa kutokana jinsi Said Mohamed alichota na kunukunuu baadhi ya vipengele vya kiutunzi kwa njia ya moja kwa moja au isiyokuwa ya uwazi lakini mwangwi unasikika kutokana na urejelezi huu.

### 7.3 Mapendekezo ya Utafiti wa baadaye

Utafiti huu ulichunguza mwendelezo wa tamthilia ya *Mashetani* (1971) katika *Mashetani Wamerudi* (2016). Kwa kuwa upeo wa uchunguzi huu ulijikita katika tamthilia ya Kiswahili, mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kuhusu mabadiliko ya kimtindo hasa kipengele cha fani na mbinu za lugha. Utafiti mwingine ufanywe kuhusu suala la usimulizi na muundo katika mwanda wa ki-mwingilianomatini kwa sababu kipengele cha usimulizi kina umuhimu na upana mkubwa katika kuchunguza kazi za fasihi zilizoendelezwa.

Mwisho, itafaa kuchunguza jinsi utanzu wa tamthilia unavyoingiliana na hadithi fupi hasa kwa kuangazia ikiwa kuna mfanano au ukuruba wa kimtindo uliopo baina ya tamthilia na hadithi fupi. Kwa hivyo, hili pia ni eneo ambalo halijaangaziwa zaidi kiutafiti ili kuweka wazi suala hili. Matokeo ya uchunguzi huu yamebainisha kuwa mwendelezo wa kimatini ni dhana ya mwingilianomatini na hutumika kama njia ya kuonyesha jinsi kazi za fasihi zinavyoathiriana na mawazo ya waandishi waliotangulia. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe ili kubainisha jinsi dhima ya wanaubaadausasa inavyoathiriana na nadharia ya mwingilianomatini hasa kwa kuangazia kipengele cha ujenzi wa uhusika.

## MAREJELEO


Ahmadian, M. & Yazdani, H. (2013). A study of the effects of intertextuality awareness on reading literary texts: The case of short stories. *Journal of Educational and Social Research*, *3*(2), 155-166.

Ahmadian, M. (2010). The effects of intertextuality awareness on literary text translation: A case study. In *3rd Conference on Linguistics, Language, and Literature. Athens* (pp. 12-15).

Allen, G. (2000). *Intertextuality*, London, Routledge.

Bakhitin, M. (1981). *The Dialogic Imagination: Four Essays.* Austin. University of Texas Press.

Bakhtin, M. (1986). *Speech* & *Genres* & *Other Late Essays*. Austin: University of Texas Press.

Bosibori, B. (2016). Mwingilianomatini kati ya *Mkaguzi Mkuu* wa *Serikali* na *Mstahiki Meya* (Doctoral Dissertation, University of Nairobi).

Childs, P. & Fowler, R. (2006). *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. London: Routledge.

Clayton, J. (2012). *Some Common Themes and Ideas within the Field of Postmodern Thought*. A Handout for HIS 389. http://webs.wofford.edu/whisnantcj/his389/ postmodernism.pdf. Last modified Nov 19, 2022.

Cuddon, J. (2013). *A dictionary of Literary Terms and Literary* Theory.Wiley: Blackwel.

D'Angelo, F. (2010). *The Rhetoric of Intertextuality*", In *Rhetoric Review*. Vol. 29, No. 1, 31-47. London: Taylor & Francis Group

Deigner, L. (2005) *Intertextuality in the Contemborary Swahili Nove*l: Euphrase Kezilahabi's *Nagona* and William E. Mkufya's *Ziraili* na *Zirani*. *Swahili Forum*

Eagleton, T. (1983). *Literary Theory: An Introduction.* Oxford: University of Minnesota Press.

Eliot, T. (2015) *Tradition and Individual Talent*. The Sacred Wood, Retrieved August 10,2915 from http://www.bartleby.com.200.sw4.html

Halliday, M. (2003). *On Texts and Discourse*, vol.2, Edited by Webster, J. Continuum. London and New York

Hussein, E. (1969). *Kinjeketile*, Nairobi: Oxford University Press

Hussein, E. (1971). *Mashetani. Dar es Salaam:* Oxford University Press.

Hussein, E. (1976). *Jogoo Kijijini.* Nairobi: Oxford University Press

J. Korir, & Mwanzandi, I. & Kisurulia, S. (2019). vipengele vya mwingilianomatini katika ujenzi wa maudhui ya umaskini: Mfano *Musa Leo* na *Bina-Adam. East Africsn Journal of Swahili Studies,4(1, 2019)*

Kehinde, A . (2013) Intertextuality and Contemporary African Novel. *Nordic Journal of African Studies* 12(3) page 372-386

Kevogo, A. (2018) Taswira ya utandawazi katika riwaya mpya ya Kiswahili.Mfano wa riwaya ya *Dunia Yao*.Kioo cha lugha 15(1)

Kilingo, I. (2019). Mwingilianomatini katika Utenzi *wa Fumo Liyongo* na tamthilia ya *Kifo Kisimani*. Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

King'ei, G. (2018). Usanifu wa lugha katika uandishi wa Ebrahim Hussein. *Mulika Journal*, *1*(1).

King'ei, Kitula G. (1987). Mwongozo wa Mashetani: East African Educational Publishers, Nairobi

Kiprotich, P., Obuchi, S. & Mohamed, M. (2021). Mwingiliano wa Kisimulizi katika Tenzi za *'Fumo Liyongo'*,'*Gilgamesh*,'*Mikidadi* na *Mayasa* pamoja na'Simulizi ya Samsoni'(SS). *Mwanga wa Lugha*, *6*(1), 27-42.

Kothari, C. (2009). *Research Methodology, Methods and Techniques*, (2nd Edition). New Delhi: New Age International, (p) Limited Publisher

Kristeva, J. (1969). *Intertextuality Theory*, Columbia Universiyy Press, New York

Kristeva, J. (1986). The Kristeva Reader, edited by T. Moi. Oxford: Basil Blackwel

Leitch, V. (1983*). Decostructive Criticism: An Advanced Introduction*: New York: Columbia University Press

Lemanster, T. (2012). *What is intertextuality*? Great World Text: A programme of the centre for Humanities, University of Wisconsin- Madson, Wisconsin.

Lukamika, M. (2022). Je, Kuna Matapo katika Fasihi Simulizi? East African Journal of Swahili Studies, 5(2), 58-68. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.948.

Macha, N. (2013). Matumizi ya mtindo wa Mwingilianomatini kwenye Tendi Makala katika chombez.blogspot.de/2013/05/800x600-normal-0-21-false false-false-23.html?m=1

Maggati, C., Wafula, R. & Osore, M. (2022). Athari za Mazingira Asilia ya Mtunzi katika Ukiukaji wa Kaida za Uhalisia kama Kipengele cha Uhalisiamazinga ombwe katika Riwaya za Shaaban Robert na za Euphrase Kezilahabi. *Mwanga wa Lugha*, *7*(2), 203-214.

Masatu, F. Hyera, V., Ndunguru, O. & Ponera, A. (2020). Mwingilianomatini katika Tamthilia ya *Utangamano Wetu Ushindi Wetu* (2017) ya Anitha E. Mgimba. *East African Journal of Swahili Studies*, 2(2), 128-143. https://doi.org/10. 37284/eajss.2.2.217

Matundura, E. (2012). *Mashetani ni Tamthilia ya Upeo wa Juu*. Taifa Leo. Narobi: Nation Media Group

Miola, S. (2004). *Seven types of intertextualities*. London. Routledge.

Nkwera, F. (1977). Ebrahim Hssein Mwandishi wa Tamthiliya. Katika Mulika Na. 11, TUKI, Kur. 38-45, Dar es Sala

Mningo, R. (2015). Tathmini ya mwingilianomatini katika utunzi wa Emmanuel Mbogo: Utafiti Linganishi wa Tamthiliya ya *Ngoma ya Ng'wanamalundi na Fumo Liongo* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Mohamed, S. A. (1974). Pungwa. Nairobi: Longhorn Publishers.

Mohamed, S. (2016). *Mashetani Wamerudi*. Spotlight Publishers (EA) Ltd.

Mose, E., Obuchi, S., Mosol, & Kandagor, M. (2020). Taswira ya tanzu za sanaa za maonyesho ya jadi katika tamthilia ya Kiswahili: Mfano wa *Mashetani*, *Pungwa*, *Ngoma ya Ng'wanamalundi* na *Mashetani Wamerudi*. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences*, 4(2), 31-59

Mugambi, P. (1982). Uhakiki wa Maudhui katika tamthilia za Kiswahili za Kikenya zilizochapishwa. M.A Thesis: University of Nairobi

Nduti, S. (2000) Uingilianomatini Katika Filamu za Drama Nchini. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi

Ngesa, A., Matundura, E. & Kobia J. (2015). *Mwingilianomatini katika Tamthilia za Kiswahili: Mashetani na Kijiba cha Moyo*. Katika, Swahili Forum

Njambi, M. (2023). Mwingiliano Matini kama Kunga ya Uandishi katika Riwaya za SA Mohamed:" *Dunia Yao*"(*2006*) na" *Nyuso za Mwanamke*"(2010). *Mwanga wa Lugha*, *8*(1), 111-120.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Njoroge, H. (2007). Mwingilianomatini katika riwaya za *Tata za Asumini* na *Rosa Mistika*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Njoroge, S., Meitamei, A., & Kodak, B. (2022). Intertextuality of Themes in the Plays of *Kinjeketile and Majira ya Utasa*.

Nkwera, F. (1977). Ebrahim Hussein Mwandishi wa Tamthiliya. katika Mulika Na. 11, TUKI, Kur. 38-45, Dar es Salaam

Nwagbara, U. (2011). *Intertextuality and The Truth of Achebe's Fiction*: Militarised Nigerian Postcolony in Anthills of the Savannah. *The African Symposium 11*, 2: 85-98.

Nzuki P. (2003). Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika Ushairi wa Kithaka wa Mberia. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi

Ongarora, S. (2020). *Usasa Katika Ushairi Wa Kithaka Wa Mberia: Uchanganuzi Wa Maudhui Na Mtindo* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Peter A. (2015). Intertextuality Essay writing by Students in High Schools in Tharaka Nithi County Kenya. Chuka University. Unpublished thesis.

Plett, H. (1991). Intertextualities, *Intertextuality*. Walter de Gruyter and Co. Berlin and New York.

Plottel, J. & Charney, H. (1978). *Introduction to Intextuality New Perspective in Criticism.* New York: Literary Forum.

Ponera, A. (2014*). Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salam: Karljamer Print Technology.

Ricard, A. (2000). Ebrahim Hussein. *Theatre and Individualism Swahili*. Nairobi: Mkuki wa Nyota Publishers.

Saleem, M. (2013). Maudhui na fani katika tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthilia za *Mashetani* na *Kivuli Kinaishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Saleh, K. (2015). Ufasihi simulizi katika riwaya za Shaaban Robert: Mifano kutoka *Adili* na *Nduguze* na *Wasifu wa Siti Binti Saad* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania.

Salum. A. (2018). Kutathmini vipengele vya fasihi simulizi katika uandishi wa Ebrahim Hussein: Mfano kutoka *Ngano za Jadi*, *Jogoo Kijijini* na *Mashetani.* Tasnifu ta Uzamili Chuo Kikuu cha Tanzania.

Saraswati, K. (2019). *Analysis of character and characterization in the compilation of Malay Poetry:* “Mirror. University of Negeri Semarang.

Senkoro, E. (1987). *Fasihi na Jamii*. Dar es Salaam: Press and Publicity centre.

Wafula, R. & Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakika wa Fasihi*: Nairobi, The Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. (1999). *Uhakiki wa Tamthiliya: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Wallek, R. & Warren, A. (1988). *Theory of Literature*. Penguin Books. New Zealand Auckland

Wallace, C (2006). *Reading*. Oxford: Oxford University Press

Wamitila, (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers

Wamitila, K. (2003). “*Influence or Intertextuality?* A Comparative Study of Kezilahabi’s *Nagona* and *Mzingile* and Juan Rulfo’s Pedro Paramo,” in *Kiswahili.* pp. 49-58.

Wamitila, W. (2010). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Yanjela, W. (2015). Pathway to African Feminism and Develooment: *Invoking memeories of legendary African Women's Studies Centre*. Katika journal of African Women's Studies Centre Vo. 1, No, 3 University of Nairobi.

Zengin, M. (2016). An introduction of Intertextuality as Literary Theory: *Definitions, Axioms and the Originators*. Sivas Cumhurlyet University.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho 1: Barua ya Kumtambulisha Mtafiti kutoka Chuo kikuu cha Chuka

CHUKA UNIVERSITY

Knowledge is Wealth *(Sapientia divitia est)* Akili ni Mali

**OFFICE OF THE DIRECTOR**
**BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES**

Telephones: 020-2310512/18
Direct Line: 020-268 7625
postgraduate@chuka.ac.ke
P. O. Box 109-60400, Chuka
Website: www.chuka.ac.ke

**REF: AM12/51106/20**

**15th August, 2024**

**Director**
**National Commission for Science Technology and Innovation**
**Off Waiyaki Way, Upper Kabete**
**P O Box 30623, 00100**
**Nairobi.**

Dear Sir / Madam,

**KENNETH MUGAMBI MUTUMA**

The above-named person is a *bona fide* student of Chuka University pursuing MA in Kiswahili proposal titled: **Mwendelezo wa Tamthilia ya Mashetani(1971) Katika Mashetani Wamerudi (2016): Uhakiki wa Kimwingilianomatini**

Mr. Mugambi has defended at the Faculty level and is now expected to conduct research.
Any assistance accorded will be highly appreciated.

Yours sincerely,

Prof. Moses Muraya, Ph.D.

**DIRECTOR**
**BOARD OF POSTGRADUATE STUDIES**

**Kiambatisho 2: Barua ya Idhini ya Kamati ya Maadili ya Chuo Kikuu cha Chuka**

**CHUKA UNIVERSITY**

**Knowledge is Wealth *(Sapientia divitia est)* Akili ni Mali**

**CHUKA UNIVERSITY INSTITUTIONAL ETHICS REVIEW COMMITTEE**

Telephones: 020-2310512/18 P. O. Box 109-60400, Chuka
Direct Line: 0772894438 Email: info@chuka.ac.ke, Website: www.chuka.ac.ke

**13th August, 2024**

**REF: CUIERC/ NACOSTI/606**
TO: **Kenneth Mugambi Mutuma**

**RE: Mwendelezo wa Tamthilia ya Mashetani (1971) Katika Mahetani Wamerudi (2016): Uhakiki wa Kimwingilianomatini**

This is to inform you that *Chuka University IERC* has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is *NACOSTI/NBC/AC-0812.* The approval period is 13th August, 2024 – 13th August, 2025.

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including (informed consents, study instruments, MTA) will be used
ii. All changes including (amendments, deviations, and violations) are submitted for review and approval by *Chuka University IERC.*
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affected safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to *Chuka University IERC* within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions.
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal.
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to *Chuka University IERC.*

Prior to commencing your study, you will be expected to obtain a research license from National Commission for Science, Technology and Innovation (NACOSTI) https://oris.nacosti.go.ke and also obtain other clearances needed.

Yours sincerely

**Dr. Benjamin Kanga**
**SECRETARY**

**Kiambatisho 3: Kibali cha Utafiti cha NACOSTI**

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: 211955

Date of Issue: 21/August/2024

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. KENNETH MUGAMBI MUTUMA of Chuka University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Tharaka-Nithi on the topic: MWENDELEZO WA TAMTHILIA YA MASHETANI (1971) KATIKA MASHETANI WAMERUDI (2016): UHAKIKI WA KIMWINGILIANOMATINI for the period ending : 21/August/2025.**

License No: NACOSTI/P/24/39272

211955

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**